

## BUNGE LA TANZANIA

---

### MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA KUMI NA MBILI

---

**Kikao cha Saba - Tarehe 4 Septemba, 2013**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Waheshimiwa Wabunge, tumshukuru Mungu tumeamka salama tunaendelea na shughuli za Kikao cha Bunge katika Mkutano huu wa Kumi na Mbili na leo ni Kikao cha Saba. Kabla hatujaanza shughuli yoyote, naomba nimwite Katibu atuongoze katika shughuli yetu ya leo. Katibu!

### MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ajenda yetu ya leo ni ajenda ya Maswali na Swali la kwanza linakwenda Ofisi ya Waziri Mkuu na linaulizwa na Mheshimiwa

Muhammed Amour Chomboh, Mbunge wa Magomeni, kwa niaba yake Mheshimiwa Murtaza Ally Mangungu.

Na. 81

**Ukiukwaji wa Sheria ya Ujenzi wa Mipango  
Miji katika Jiji la Dar es salaam**

**MHE. MURTAZA ALLY MANGUNGU (K.n.y. MHE.  
MUHAMMED AMOUR CHOMBOH) aliuliza:-**

Kumekuwa na ukiukwaji mkubwa wa ujenzi ambao haifuati taratibu na Sheria zilizowekwa na mpango miji katika Jiji la Dar es salaam.

Je, Serikali ina mikakati gani kukomesha utovu huo nidhani dhidi ya waliopewa dhamana kusimamia Sheria hiyo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA  
MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Muhammed Amour Chomboh, Mbunge wa Magomeni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kumekuwa na ukiukwaji wa ujenzi ambao haifuati Sheria, Kanuni na taratibu zilizopo, hususani katika Jiji la Dar es salaam. Maeneo yanayohusika na ukikwaji ni kwenye utoaji wa

vibali vya ujenzi; Ukiukwaji wa Sheria za ujenzi wa maadili ya kitaaluma usiozingatia Sheria na Mipango Miji Na. 8 ya mwaka 2007 na Kanuni ya udhibiti na uendelezaji Miji Na. 242 ya mwaka 2008. Kwa mujibu wa Sheria ya Mipango Miji uendelezaji wowote Mijini sharti upate idhini kutoka kwa Mamlaka ya upangaji ambayo ni Jiji, Manispaa, Mji na Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuchukua hatua za Kisheria na Kinidhamu dhidi ya watendaji wanaoshindwa kusimamia Sheria, Kanuni na taratibu za Mipangomiji na ujenzi.

Kwa mfano kufuatia kuperomoka kwa ghorofa katika kiwanja Na. 2032/72 mtaa wa Indhira Ghandhi Mkoani wa Dar es salaam watumishi watatu wamesimamishwa kazi ikiwemo kufunguliwa mashtaka dhidi ya watendaji wote waliohusika.

Aidha ili kusisitiza msimamo wa Serikali katika kusimamia Sheria na taratibu za ujenzi katika Jiji la Dar es salaam, OWM TAMISEMI na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam waliitisha kikao cha watendaji wote wa Mkoa kuanzia ngazi ya Kata, Tarafa, Halmashauri za Manispaa na Jiji tarehe 8 Julai, 2013 kuwakumbusha wajibu wao wa kusimamia Sheria za ujenzi mijini na usafi pamoja na kuwaonya wale wote watakaoshindwa kutimiza wajibu huu.

Serikali hivi sasa inapitia Sheria ya Mipango Miji na utaratibu wa utoaji vibali na usimamizi hasa katika Jiji la Dar es salaam ili kuboresha na kuhakikisha kwamba zoezi zima

la utoaji wa vibali vyatya ujenzi linakuwa na udhibiti wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika mwaka wa fedha 2013/2014 imeanza kutekeleza mpango utakao imarisha na udhibiti wa takwimu za kijiografia za matumizi ya ardhi; takwimu za kijiografia za maeneo yaliyopimwa; takwimu za mipaka ya maeneo ya utawala, takwimu za nyumba, takwimu za maeneo yaliyotwaliwa kwa ajili ya fidia kwenye Halmashauri za Majiji, Manispaa na Miji.

Mpango huu unatekelezwa kuitia miradi ya *Tanzania Strategic Cities Program (TSCP) Urban Local Government Support Program (ULGSP)* na *Dar es salaam Metropolitan Development Program (DMDP)* kwa mkopo wa Benki ya Dunia na Msaada toka Serikali ya Denmark (*DANIDA*).

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Pamoja na majibu yanayowiana ya Mheshimiwa Waziri ningependa nimwulize maswali ya nyongeza. Kwanza tatizo la uangukaji wa majengo limeanza siku nyingi sana, kama tunakumbuka Mtaa wa Msimbazi, eneo la Keko majengo yamekuwa yakianguka.

Lakini hatua Ambazo zinachukuliwa dhidi ya watendaji hawa bado hazijathibitika mbele ya wananchi kwa maana kuwa vitendo hivi vimekuwa vikijirudia rudia. Ni nini ahadi ya Serikali kwa watendaji hawa ambao hawajasimamia ipasavyo ndipo swali la Mheshimiwa Mbunge lilipokuwa limelenga hilo la kwanza.

La pili, kumekuwa na hali ya ubomoaji wa majengo ya wananchi tangu alipoanza kujenga mpaka amehamia Tanzania ni nchi ambayo ina mfumo wa watendaji kuanzia katika ngazi za vitongoji, watendaji hawa wanakuwa wapi mpaka mtu anamaliza kujenga mwisho unaenda kubomolea wananchi?

Kwa nini Serikali isichukue wajibu kwa watendaji wake kuzembea pale ambapo mwananchi maejenga katika eneo lisilo staili Serikali iwajibike kuwalipa wananchi hawa kwa utendaji mbovu kwa watendaji hawa wa Serikali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kuwa Serikali inachukua hatua gani kwa kuendelea kuporomoka kwa majengo, kama nilivyotangulia kusema kuwa tumekuwa tukichukua hatua ikiwemo pamoja na kuwachukulia hatua za kinidhamu na kuwapeleka katika Mahakama ili haki pia iendelee kutendeka.

Pili, kuhusu suala la wananchi kujenga mpaka wanamaliza ndipo wanakuja kubomolewa majengo ninadhani wote sisi ni mashahidi mara nyingi Watanzania mtu akianza kujenga na akiambiwa kuwa hilo eneo halihusiki wanakimbilia Mahakamani na wakati Kesi ikiendelea ujenzi huo huenda haraharaka. Kwa hiyo, wakati mwingine inapelekea kesi inapokwisha badala ya kuzuia ujenzi kinachofuata ni kwenda kubomoa ujenzi uliopo.

Ninapenda kuchukua fursa hii kuwaomba Watanzania wahakikishe kwamba kabla hawajatumia pesa zao kuingia gharama ambazo zinaweza kupelekea kuwa hasara baadaye ni vizuri kufuata Sheria Kanuni na Taratibu za Mipango Miji.

**MHE. HAROUB MOHAMMED SHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niulize swali moja la nyongeza. Katika suala hili, tataizo la kuporomoka majumba katika nchi yetu linaonekana kuwa hakuna *Collective Responsibility* ya Serikali, kwa sababu kuna vyombo vingi lakini kila chombo kikiulizwa kinasema hakihusiki.

Kwa mfano kuna *Engineers Registration Board* ambayo ni Bodi ya Wahandisi, kuna *Contractors Registration Board* ni Bodi ya Wakandarasi lakini wote hawa majumba yakianguka hawachukuliwi hatua kwasababu wanasema hawahusiki sasa anayehusika ni nani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nani anayehusika inategemea ni aina gani ya kosa.

Kama ni Mhandisi *site* amefanya uzembe na jengo likaporomoka huwezi ukasema kuwa huenda *Engineers Registration Board* inahusika. Ndiyo maana mara tu yanapotokea matatizo ya namna hiyo huwa inaundwa Tume kufanya uchunguzi kama tulivyofanya kwa jengo lililoporomoka Dar es salaam na waliohusika na uzembe

wamebainika na wamepekwa mbele ya vyombo vyा Sheria. (*Makofi*)

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nitakuwa siyo mwingi wa fadhila kama nisipokukushukuru wewe uliyoniona huku katika Bunge hili lako Tukufu ili niulize swalı la nyongeza kwa mara ya kwanza.

Mheshimiwa Waziri utakubaliana na mimi kuwa Wizara yako inafanya kazi kwa ubaguzi kinyume cha Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ikiwa wengine wanapewa vibali na wengine hawapewi vibali kuhusu ujenzi na ninao ushahidi wa kutosha kuthibitisha suala hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jaku, sasa swalı lako hapo ni nini? Mheshimiwa Waziri sijui kama umemwelewa?

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yake hufanya kazi kwa ubaguzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, sasa swalı ni nini?

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara isitende kazi ya ubaguzi wengine waruhusiwe na wengine wasiruhusiwe.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo kweli kuwa Wizara yangu inafanya kazi kwa ubaguzi kama kuna suala lolote ambalo amekumbana nalo ambalo

anahisi amefanyiwa ubaguzi basi anakaribishwa kuja katika ofisi yangu, nimsikilize na niweze kumtatulia kero yake.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Moses Machali, Mbunge wa Kasulu Mjini.

Na. 82

**Uuzwaji wa Viwanja Zaidi ya Mara Moja  
Kwa Watu Tofauti Kasulu**

**MHE. MOSES J. MACHALI** aliuliza:-

Kumekuwa na malalamiko mengi kwa wananchi juu ya Maafisa wa Ardhi, Kasulu Mjini kuuza viwanja zaidi ya mara moja kwa watu tofauti na kusababisha migogoro kati ya wananchi wasio na hatia.

(a) Je, Waziri haoni haja ya kutembelea Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu Mjini ili kuona kasoro hizo zinazofanywa na watendaji wa Wizara yake na kutatua migogoro iliyopo?

(b) Je, ni lini Waziri atafanya ziara hiyo?

(c) Je, ikibainika kuwa ni kweli watendaji wa Wizara yake wanahusika ni hatua gani zitachukuliwa dhidi yao ili kukomesha tabia hiyo isiyofaa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Moses J. Machali, Mbunge wa Kasulu Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia uzito wa hoja zilizowasilishwa na Mheshimiwa Mbunge naomba nichukue fursa hii kumweleza Mheshimiwa Mbunge kuwa niko tayari kufanya ziara Mkoani Kigoma na hususani Wilayani Kasulu mara baada ya Bunge hili kuahirishwa.

Hata hivyo OWM- TAMISEMI itaunda timu maalumu itakayowajumuisha wataalamu kutoka OWM - TAMISEMI na Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa wa Kigoma kwa ajili ya uchunguzi wa hoja zilizowasilishwa na Mheshimiwa Mbunge. Baada ya uchunguzi huo taarifa itawasilishwa OWN - TAMISEMI ili kuiwezesha ofisi yangu kuchukua maamuzi kwa kuzingatia hoja zitakazokuwa zimejitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kuwa endapo itabainika kuwa kuna watumishi wanaohusika na tabia hizo, Ofisi ya Waziri Mkuu, - TAMISEMI haitasita kuwachukulia hatua stahiki za Kisheria.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimwulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa baadhi ya malalamiko ya wananchi hususani wa Jimbo la Kasulu Mjini na Maeneo mengine ya Wilaya ya Kasulu, Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa wa Kigoma inayo na imeshindwa kuyashughulikia kwa muda mrefu. Je, Ofisi yako

haioni kuwa ni busara isiwahushe katika Tume au Kamati maalumu itakayoundwa na Wizara yako katika kushughulikia matatizo hayo? Kwa kuwa hawataweza kuwa *fair*.

Swali la pili, nimekuwa nikiahidiwa mara kadhaa na Mawaziri mbalimbali hasa Waziri wa Ardhi ninasikitika kuwa bahati mbaya hayupo Professor Anna Tibaijuka, Naibu Waziri yupo kwamba watafanya ziara kuja kuangalia migogoro hii. Lakini toka mwaka juzi, mwaka jana na mpaka sasa hakuna Waziri yoyote ambaye amekuja kuangalia migogoro hii.

Ningependa unipe *commitment* yako ni lini hasa umesema baada ya Bunge hili, maana hata wengine walipata kuniambia hivyo hivyo, ina maana umeshajipanga sasa! Ni lini hasa uniambie kuanzia tarehe ngapi pengine unaweza ukaja ili kusudi isije ikawa ikawa kama Mawaziri wengine ambavyo wamekuwa wakiahidi lakini hakuna kinachofanyika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu. Mheshimiwa Machali unataka tarehe unataka kujiardaa vizuri zaidi? Haya Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sidhani kama ni busara Ofisi ya Mkuu wa Mkoa kutoishirikisha kabisa kwa sababu Tume tunayoiunda ni sisi Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI. Lakini hatuwezi kwenda Kigoma tukakosa mwenyeji. Ninapenda

nikuhakikishie kuwa pamoja na kuihusisha Ofisi ya Katibu Tawala, Mkoa wa Kigoma, haki itatendeka.

Kuhusu suala la pili kuwa nimirrie tarehe rasmi nilitegemea nianze ziara katika Mkoa wa Kigoma tarehe 9 Septemba, 2013 lakini nikaambiwa kuwa watakuwa na harambee katika tarehe hiyo tisa ambayo itakuwa inafanyika Dar es salaam. Kwa hiyo, ninategemea yeye kwanza amalize Bunge na aweze kwenda Kigoma na Uongozi wa Kigoma uweze kurudi Kigoma ndiyo na mimi niende.

Lakini pia ninapenda niwahakikishie kabla ya Bunge linalofuata kuanza nitakuwa nimekwenda Kigoma kutembelea Jimbo lake na Wilaya nyingine zote. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nilimwona Mheshimiwa Omari Rashid Nundu.

**MHE. OMARI R. NUNDU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa kuwa tatizo hili haliko Kigoma tu peke yake Tanga limejaa tele. Sasa Serikali ina mikakati gani badala ya kwenda Kigoma tu lakini kulishughulikia tatizo hili kikamilifu kwa nchi nzima.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kumekuwa na migogoro mingi ya ardhi na utekelezaji wa Mipango Miji katika maeneo mbalimbali nchini. Sasa hivi kuanzia Bajeti ya mwaka 2013/2014, tumeanza kutekeleza mpango ambao takwimu zetu za

Mipango Miji tunaziweka katika mfumo wa kijiografia ambapo itatuwezesha kuweza kuviona viwanja vyote na hatua zilizopo. Hatua ambayo itatuwezesha kuweza kuchukua hatua haraka iwezekavyo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nimemwona Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Kigoma.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kila Mwananchi anayo haki ya kupimiwa kiwanja pindi anapokuwa anahitaji kupatiwa huduma hiyo na watalaamu katika Halmashauri husika, lakini katika Wilaya ya Kasulu wapo wananchi ambao wamekuwa wakihitaji kupatiwa huduma hiyo lakini wanapewa masharti ya kwamba wawagawie kwanza wataalam wa Wilaya ya Kasulu viwanja ndipo waweze kupatiwa huduma ya kupimiwa viwanja.

Kwa mfano, kuna mwalimu mmoja anaitwa Mwalimu Michael na jirani yake watu hawa wamepakana na Kanisa, wamekuwa wakitafuta huduma hiyo mpaka hivi sasa wameshachoka, ninaomba kumwuliza Waziri ni lini Serikali itawasaidia wananchi hao ili waweze kupatiwa huduma kwasababu wana haki ya kimsingi ya kupatiwa haki ya kupimiwa ardhi pindi wanapohitaji huduma hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa

Mwenyekiti, ninapenda kujibu swalii la Mheshimiwa Genzabuke, Mbunge Viti Maalum Mkoa wa Kigoma na Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Kigoma kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa wananchi wana haki ya kupimiwa na kupata viwanja pale wanapohitaji. Lakini pia kwa kuchangia gharama za kufanya hivyo. Niseme tu kwamba siyo halali kuwa ili upimiwe ni lazima utoe chochote kwa wale wanaotaka kupima.

Kwa kuona kuwa baadhi ya Halmashauri uwezo wao wa kuweza kupima viwanja ni mdogo Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI tumekuwa na makubaliano na Benki ya *TIB* ya kuweza kuziwezesha Halmashauri kwa makubaliano maalumu kuweza kupima mijii yao na kuendeleza miundombinu katika maeneo hayo.

Kwa hiyo, niseme tu kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu kama ina matatizo ya kifedha basi wafuate utaratibu ambao tumewaelekeza waweze kuwapatia wananchi viwanja bila kulazimika kutoa rushwa au kutoa chochote kwa wapimaji wa viwanja.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swalii linalofuata linaulizwa linaenda Wizara ya Maji na linaulizwa na Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita, Mbunge wa Kondoa Kaskazini, Mheshimiwa Zabein.

Na. 83

**Tatizo sugu la Maji Kondoa**

**MHE. ZABEIN M. MHITA** aliuliza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swal la Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita, Mbunge wa KondoaKaskazini, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa dhati wa kutatua tatizo la maji aambalo limekuwa sugu Wilayani Kondoa?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuondoa tataizo la maji katika Wilaya ya Kondoa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swal la Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita, Mbunge wa KondoaKaskazini, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutatua tatizo la maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa, Serikali inatekeleza miradi ya maji ya vijiji kumi (10) katika vijiji vya Soera, Madisa, Choka, Kwadelo, Makirinya na Kirere cha Ng'ombe. Ujenzi wa Miundombinu ya maji unaendelea katika vijiji vya Kwadelo, Choka, Madisa na Soera. Katika vijiji vya Makirinya na Kirere cha Ng'ombe viro katika hatua ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi.

Aidha, kupitia mpango wa Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa, Serikali inatekeleza miradi ya maji katika vijiji vya Kinyasi, Majengo na Masange na kupitia ruzuku ya Maendeleo kwa Serikali za Mitaa (*LGCDG*), Serikali inaendelea na upanuzi wa mradi wa maji Mjini Kondoa, ukarabati wa Bwawa la Kisaki lililopo katika vijiji vya Kisaki na Itaswi Wilayani Kondoa. Mradi wa usambazaji maji katika kijiji cha Mongoroma na kitongoji cha Fai kilichopo katika Kijiji cha Ntomoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa imetengewa kiasi cha shilingi bilioni 1.9 kupitia mfuko wa pamoja (*basket fund*) shilingi bilioni 1.2 kutoka fedha za nyongeza bilioni 184.5 ili kukamilisha miradi ya vijiji kumi, na shilingi milioni 924.2 kupitia miradi yenyе kuleta matokeo ya haraka.

Aidha, Serikali imeanza kutekeleza ahadi ya Waziri Mkuu ya kukarabati mradi wa maji Ntomoko ambako shilingi bilioni moja zilitumwa mwishoni mwa mwaka wa fedha 2012/2013 na katika mwaka wa fedha 2013/2014 shilingi bilioni mbili (2) zimetengwa kwa ajili ya mradi huo.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishukuru Serikali kwa kuona tatizo la maji katika Jimbo la Kondoa Kaskazini na kututengea fedha. Sasa nina maswali mawili madogo ya nyongeza:-

(a) Waziri ameeleza kwamba katika zile fedha za nyongeza kuna bilioni 1.2 ambayo imetengwa. Je, ningependa kufahamu bilioni 1.2 itanufaisha vijiji gani.

(b) Kwa kuwa, Mji wa Kondoa bado una tatizo kubwa la maji na katika jibu la Waziri ameeleza kuwa Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi katika Mji wa Kondoa. Je, ni miradi gani hiyo? Watu wa kondoa wangependa kufahamu miradi hiyo itakamilika lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza uniruhusu nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia sana miradi ya maji katika Jimbo lake la Kondoa na hasa ukizingatia kwamba Kondoa ni moja ya maeneo ambayo yana shida sana ya maji. Baada ya maelezo hayo naomba kujibu maswali yake kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vijiji vitakavyofaidika na mgao wa shilingi bilioni 184.5 ambao umepaleke wao kupata milioni 924 ni kama ifuatavyo:-

Kijiji cha Kinyasi Majengo, ambacho kitapata milioni 477.2; Kijiji cha Masange ambapo kitapata milioni 447.0. Hivi vijiji ndivyo vipo kwenye matokeo ya haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu nini kinafanyika Mjini Kondoa, kutokana na maelezo yangu ni kwamba sasa hivi tunafanyakazi kubwa mbili. Kazi ya kwanza tunafanya upanuzi wa mtando uliopo.

Katika upanuzi huu tunanunua mabomba na kuyalaza na kuwafikishia wananchi wapate maji. Kazi ya pili pale pana visima viwili ambavyo vilichimbwa mwaka 2012 kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa maji pale Mjini kwa

sababu maji ni ya shida. Kwa hiyo, katika visima hivi tunaweka miundombinu ya maji na baada ya kuwafikishia wananchi tumetenga fedha za kufunga mita kwa kuanzia mia tano (500).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ni lini miradi hii itakamilika ile ya vijiji kumi Septemba tunategemea miradi ya vijiji vitatu itakuwa tayari ambayo nimevisoma kwenye jibu la msingi, na Novemba tutakuwa na mradi wa kijiji kimoja na kwa maana kwamba Halmashauri ya Kondoa imegawanyika katika Halmashauri mbili ya Nchemba na Kondoa wao wanatekeleza vijiji sita. Kwa hiyo, vinne vitakamilishwa kabla ya Novemba na viwili vitakaimilishwa kabla ya Juni, mwaka kesho. Ahsante sana.

**MHE. MWIGULU L. N. MADELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana. Kwa kuwa, matatizo ya maji ya aina hii yapo sehemu nyingi hapa nchini ikiwemo Wilaya ya Iramba pale Kiomboi, Ulemo na Kinampanda.

Je, Naibu Waziri atakuwa tayari baada ya Bunge ama katika muda mwingine wa haraka kufika Kiomboi kufanya ziara na kuharakisha utekelezaji wa miradi hiyo ili wananchi wasiendelee kupata shida ya maji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru kwanza kwa shughuli anazozifanya za kufuatilia miradi ya maji katika Jimbo lake. Ni kweli pale tuna miradi katika vijiji kumi na mojawapo ni Ndago ambao umekamilika, Kiomboi imeshatangazwa, tunasubiri kupata wakandarasi waanze kufanyakazi. Kwa kuwa tumesema

kwamba kufikia Septemba, 2013 tutapata miradi mitano kila Halmashauri na kufikia Juni mwaka kesho 2014 tuwe na miradi mingine mitano jumla kumi.

Tumepanga mikakati ya kuona kwamba lazima tuwe tunatembelea kila Halmashauri kujionea utekelezaji wa miradi hii iliyokamilika na ambayo haijakamilika ili kuweza kusimamiana nini kiweze kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninamhakikishia Mhehsimiwa Mwigulu Nchomba, kwamba tutapanga ziara ya kwenda Mkoa wote wa Singida na Halmashauri zote mara baada ya kukamilisha shughuli za hapa Bungeni.

Na. 84

### **Matumizi ya Mabomu ya Machozi**

**MHE. HUSSEIN MUSSA MZEE** aliuliza:-

Matukio mengi ya vurugu ya hivi aribuni yameonyesha Askari Polisi wakitumia mabomu ya machozi ili kutawanya wanaofanya vurugu hizo:-

(a) Je, mabomu haya hayana madhara kwa binadamu?

(b) Je, Polisi hawana mbinu au silaha nyingine wanazoweza kutumia ili kuепusha madhara yanayotokea?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee, Mbunge wa Jang'ombe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, mabomu ya machozi hayana madhara endelevu. Silaha hizi zinafanyiwa utafiti wa kimaabara na kukubalika kimataifa ambapo zikitumika vizuri hazina madhara makubwa kwa bianadamu zaidi ya kuwasha macho na athari hizo hudumu kwa muda mfupi tu.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa sheria na kanuni za uendeshaji wa Jeshi la Polisi sambamba na mikataba ya kimataifa juu ya matumizi ya nguvu katika kudhibiti vurugu za kijamii (*Public disorder*), Polisi hutumia mbinu na silaha za aina nyingi zikiwemo virungu, maji ya kuwasha, risasi baridi, mabomu ya machozi, mabomu ya kishindo, mbwa na farasi kutegemea na aina ya vurugu, wingi wa watu na aina ya silaha walizonazo. Silaha hizi zinatumika kwa lengo la kutawanya au kudhibiti watu kwa urahisi wanaofanya vurugu. Mbinu kubwa za Polisi hata hivyo katika kuzuia madhara ni kutoa elimu na makatazo. Suala la utii wa sheria ndiyo jambo muhimu linalotakiwa.

**MHE. HUSSEIN MUSSA MZEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana. Katika jibu lake la msingi amesema kuwa mabomu ya machozi hayana madhara endelevu.

Je, kuna tofauti gani kati ya mabomu ya machozi na maji ya kuwasha.

Swali la pili; amesema kwamba mbinu za Polisi katika kuzuia madhara ni utii wa sheria.

Je, nini mikakati ya Serikali katika kuhakikisha kuwa elimu hiyo inawafikia walengwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ya kuwasha na mabomu ya machozi yote ni silaha baridi, tofauti yake kubwa ni vipi yanaondolewa kutoka pale yalipo kwenda kufikia kwenye eneo ambalo linatakiwa litumike.

Mabomu ya machozi yanayotumika ni aina ya milipuko ambayo ni lazima inasukumwa kwa ajili ya kwenda kwenye kundi kwa ajili ya kuwasha macho na kuwaondoa wafanyakaji vurugu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *chemical* fulani ambazo zinaitwa *AC SMOKE PROJECTAIL* ndiyo sana zinatumika na maji ya muwasho ni miyeyuko ya kikemikali ambayo tofauti kubwa ni aina ya kemikali na mashine zinazotumika katika kuyasukuma.

Kuhusu elimu ya utii wa sheria bila shuruti tuna *program* nyingi zikiwemo za runinga, redio, pia kuna mikutano ambayo huwa inaitishwa, kuna vipindi vyta wanafunzi mashulenii pia tunashiriki katika makongamano kuwaita watu tofauti, kwenye mafunzo ya Polisi Jamii na jamii kwa

ujumla katika kutii sheria. Pia katika makongamano au katika majukwaa ya kisasa.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matukio ya mapambano ya askari na raia yamekuwa ni mapambano endelevu, na katika mapambano haya tumefika hatua ambayo sasa siyo mabomu tena ya machozi yanatumika ila zinatumika risasi za moto na yanatumika hata mabomu ya kivita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu tumekuwa tukilalamika kuhusu matukio haya hasa yanapokuwa yanahusu mikutano na mikusanyiko ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo CHADEMA, na tumeiomba Serikali mara nyingi ione umuhimu wa kuunda Tume huru ya Kimahakama ili iweze kuchunguza uhalisia wa matukio haya na wale wote wanaohusika waweze kuchukuliwa hatua za kisheria, lakini Serikali hadi sasa imesita kuchukua hatua hiyo.

Serikali inatoa tamko gani kuhusiana na jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ni swali moja tu kwa mujibu wa kanuni kwa maswali ya nyongeza ni swali moja tu, naomba sana.

### **NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, Askari Polisi wanakabidhiwa silaha za aina tofauti na kinachotegemewa ni kwamba kwa kawaida na ndiyo utii wa sheria bila shuruti uwepo wa Askari ungetosha kuwafanya watu ambao wana nia ya kufanya vurugu watawanyike. Kwa sababu hili halifanikiwi wanaangalia njia nyingine ya mwanzo ya awali kwenye ile continuum ya kutumia nguvu.

Nguvu za Polisi na aina ya silaha zinategemea aina ya vurugu na wafanyakaji. Hata hii ya maji ya kuwashaa kuna *concentration*, tunaweza tukaanza *concentration* ndogo kwa kuona hawa siyo wafanyakaji vurugu wazoefu, lakini *concentration* inaongezwa pale ambapo inaonekana ni wazoefu.

Vivyo hivyo matumizi ya silaha ya mipira mpaka kwenye silaha zinategemea kwamba Polisi pale kwenye tukio wanahisi madhara gani yanaweza kutokea ikiwa hawakutumia nguvu za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu matumizi haya kwa kweli si jambo ambalo linapendelewa na kwa kiasi chote Askari wanafunzwa namna ya kudhibiti. Udhibiti unavyokuja mpaka kutumika risasi ya moto ni kwamba umetokana na wafanya vurugu kuliko Polisi wenywewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la kuunda Tume huru, suala la matukio ambayo tunayo mpaka sasa tunatumia uchunguzi wa kawaida na tunatuma *task force*

ambazo tunazo. Haja ikiwepo jambo ambalo litaonekana ni zito zaidi basi tunaweza tukafika huko haja ikiwepo.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante. Mwaka 1992, kwa mara ya mwanzo mauaji ya kisiasa yalifanyika katika kijiji cha Shuma Mjini Pemba kwa Askari Polisi kusema wamepiga risasi juu ikarudi chini na kumwuua Mzee Omari Ali Haji.

Maelezo haya ya Polisi yamekuwa yakiulizwa mara kwa mara lakini tunataka kujua ni silaha gani Serikali imeagizia zinazopiga juu ikarudi ikaua wananchi chini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, matukio ya kawaida ya risasi kupigwa juu ikaja chini halafu ikaua ni jambo kidogo geni, isipokuwa katika kulenga kuna kitu kinaitwa shabaha, unaweza ukalenga juu ukapiga chini. (*Makofu/Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swali linalofuata, *Order Order!*

Na. 85

**Vyombo vyatya Usajili Kusajili Watoto Wanaosafiri**

**MHE. SABREENA H. SUNGURA** aliuliza:-

Vyombo vingi nya nya usafiri havina utaratibu wa kusajili watoto pindi wazazi wao wanapokata tiketi jambo ambalo hupoteza takwimu pale inapotokea ajali kama jinsi ilivyokuwa kwenye ajali ya meli ya *MV-SKAGIT*:

Je, Serikali ipo tayari sasa kuamrisha vyombo nya usafiri kusajili watoto ili kusaidia kupata takwimu sahihi za wahanga wakati wa ajali?

### **NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kusajili watoto kwenye orodha ya majina ya abiria wanaosafiri kwa kutumia meli za abiria ni utaratibu uliokuwepo hapa kabla ya ajali ya *MV Skargit*.

Hivi sasa utaratibu wa kusajili watoto umeimarishwa na utekelezaji wake unasimamiwa kwa karibu na *SUMATRA* ili kuhakikisha kuwa utaratibu huo unafuatwa. Wamiliki na waendeshaji wa meli za abiria wanaokiuka utaratibu huo wanachukuliwa hatua ikiwemo kuzuia chombo kuendelea na safari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu la kuimrisha usalama wa vyombo nya usafiri majini ni letu sote, hivyo naomba kutumia fursa hii kutoa rai kwa abiria kufuata taratibu za

kuorodhesha majina yao kamili na ya watoto wao, umri na sehemu wanakotoka kwa sababu za usalama wao.

Aidha, wamiliki na waendesha vyombo vya majini wanatakiwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za usalama wa usafiri majini.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana.

Kwa kuwa, tatizo hili limekuwa ni sugu licha ya kwamba si kwenye vyombo tu vya majini lakini hata kwenye mabasi na hususani treni. Kwa kuwa kumekuwa na tatizo sugu la baadhi ya watendaji wa shirika la reli kurusha tiketi hususani katika Mkoa wa Kigoma na Tabora hivyo basi hata yule mtu anayerushwa tiketi anakuwa labda ana watoto watatu au wanne na anaporushwa tiketi anarushwa tiketi ya kwake peke yake.

Lakini wale watoto ambao wameambatana nao wanakuwa hawajawa *registered*, Serikali sasa haioni kwamba pindi inapotokea ajali inakosa takwimu sahihi kwa sababu tu usajili haukufanyika katika vyombo hivi vya mabasi na treni?

Swali la pili. Kwa kuwa, Serikali iliweka msisitizo kwamba abiria wote watakaopanda mabasi wapewe *safe belt* (mikanda ya usalama).

Je, Serikali sasa haioni kwamba kuna haja ili kulinda haki za watoto na watoto waweze kuzingatiwa katika agizo

hilo ili inapotokea ajali basi na wenyewe waweze kuwa *protected?* Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili la watu kutotii sheria kwa hiari, siyo tu la Watendaji bali pia ni la wananchi. Wananchi masharti haya wanayafahamu kwa sababu ni sheria. Kwa hivyo kusema kwamba hawajui wajibu wao pia siyo sahihi.

Kwa hivyo ndiyo maana katika jibu langu la msingi nimesema kwamba wananchi wenyewe wajue wajibu wao wakati wanaposafiri, wawasajili watoto na wao wenyewe na hasa kununua tiketi za safari katika vituo rasmi vyatununulia hizo tiketi.

Wengi wa abiria wanaotumbukia katika mtego huu ni wale ambao hawataki kununua tiketi katika vituo rasmi vyatununulia hizo tiketi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, niombe tu kwamba, abiria wa treni, wawe abiria wa vyombo vyamajini, wawe abiria wa mabasi, wawe abiria wa ndege, wajitahidi kununua tiketi katika vituo rasmi na kwa hivyo suala la kutosajiliwa halitakuwapo. Wale wanaotafuta tiketi za mkato, ndiyo mara nyingi majina yao hayaonekani katika orodha za abiria wanaokuwa katika safari husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mikanda ya usalama, mikanda ya usalama ni sheria ya nchi ambayo pia abiria wanatakiwa kuitii kwa hiari. Kwanza ni kwa manufaa yako mwenyewe abiria kufunga mikanda ya usalama. Dereva

au mhusika wa chombo akisahau kukumbusha ujeu kwamba ajali hiyo ikitokea wewe ndiyo utapata madhara zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo Sheria kwa sasa kwamba mabasi yote yanapaswa kuwa na mikanda kwa ajili ya abiria wanaotumia mabasi hayo ingawa lilitolewa wazo kwamba na wasafiri wa meli nao wafunge mikanda. Nachelea kusema kwamba, huko msiende kwa sababu itawafanya *trapped* zaidi kwenye hivyo vyombo kuliko kujuua kwako kwa haraka. Ahsante.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa masuala yake.

**MBUNGE FULANI:** Majibu yake.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Kwa majibu yake, samahani. Naomba kumwuliza swali dogo sana. Mheshimiwa Waziri tunapotaka kusafiri kwenda Visiwa vya Unguja na Pemba, tunahitajika kwenda na kadi zetu ambazo zinafahamika kwa kumbukumbu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bahati mbaya sana unafika pale pa kununua tiketi unaambiwa hamna tena. Ukitoka nje kuna watu zaidi ya 50 wana tiketi wanakuuzia bei ya juu. Je, usalama ambao unauzungumza utapatikanaje ikiwa utaratibu ni kama huu ambao unafanywa na yale mashirika ambayo yanauza tiketi hizo?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali muda wote imesisitiza kwamba, wasafiri wanunue tiketi kwa kuonesha vitambulisho vyao. Lengo lake ni kuhakikisha kwamba, jina linaloorodheshwa kweli ni la yule anayekuwa katika safari. Kwa sababu umekuwepo ulanguzi kwa mfano kwenye treni ambako mtu anakwenda ananunua tiketi, halafu anatoka nje anaanza kulangua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumedhibiti hili jambo kule Kigoma ambako lilikuwa linajitokeza sana. Sasa hili la usafiri wa Dar es Salaam kwenda Zanzibar au Unguja kwenda Pemba, vyombo hivyo vyote ni vya watu binafsi. Nitumie tu nafasi hii kuwasihhi wamiliki wa vyombo hivi wadhibiti urushaji wa tiketi, kwa sababu hili ni jukumu lao kuhakikisha kwamba tiketi zinauzwa kwa watu na siyo wasiokuwa wasafiri, bali ziuzwe kwa watu ambao wanasafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu nalisikia kwa mara ya kwanza jambo hili mimi binafsi, basi niombe kusema kwamba tutalifanyia kazi na tutakupa majibu Mheshimiwa Kombo nini tunachofanya kuhusu jambo hili.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swali linalofuata, linaulizwa na Mheshimiwa Said Mohamed Mtanda, Mbunge wa Mchinga. Kwa niaba yake Mheshimiwa Faith Mitambo.

Na. 86

**Maendeleo Duni ya Elimu - Lindi**

**MHE. FAITH M. MITAMBO (K.n.y. MHE. SAID M. MTANDA)**  
aliuliza:-

Mkoa wa Lindi ni mionganini mwa Mikoa iliyo nyuma katika maendeleo ya elimu Kitaifa ikilinganishwa na Mikoa mingine:-

- (a) Je, Serikali inaweza kulieleza Bunge kwa nini hali hii iko hivyo?
- (b) Sababu mojawapo za kuporomoka kwa elimu  
Mkoa wa Lindi ni pamoja na hali ya uchumi na ya kihistoria. Je, Serikali iko tayari kuja na mpango wa dharura wa kukabiliana na hali ya elimu katika Mikoa huo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**  
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Mohamed Mtanda, Mbunge wa Mchinga, kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu wakati wa ukoloni ilitolewa kwa ubaguzi ili kukidhi mahitaji ya uchumi wa kikoloni, kama vile kupata vibarua na makarani wa kufanya kazi katika mashamba yao. Wazungu walipendeleta kwa kupata elimu bora zaidi yaani (Daraja la I) wakifuatiwa na Waasia na mwisho walikuwa ni Waafrika ambao walipewa elimu duni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, maeneo ya nchi pia yalibaguliwa ambapo Ukanda wa Kaskazini mwa Tanzania ambao ulikuwa na vivutio vingi kama vile ardhi yenye rutuba pamoja na hali ya hewa inayofanana na kwao, wakoloni hao walijenga shule nyingi kuliko Ukanda wa Kusini na Magharibi ambao ukanda huo ulifanywa kuwa vyanzo vyaa vibarua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya uhuru Serikali imechukua hatua mbalimbali za kuondoa tofauti za utoaji wa elimu kwa nchi nzima ukiwemo Mkoa wa Lindi. Mwaka 1967 Serikali ilichukua hatua ya kutaifisha shule za watu na mashirika binafsi, mwaka 1974 Serikali ilianzisha Mpango wa Elimu kwa Wote (*Universal Primary Education – UPE*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Serikali ilianza kuwachagua wanafunzi wanaojiunga shule za sekondari kwa kutumia mfumo wa (*quarter system*) ambapo kila mkoa ulipewa mgawo wa nafasi za sekondari ili kuwapa fursa ya elimu ya sekondari watoto watokao sehemu zenye maendeleo duni kielimu ikiwemo Mikoa ya Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM awamu ya III) na Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari (MMES awamu ya II) Serikali inatoa upendeleo maalum katika upangaji wa Walimu kwa maeneo yaliyo nyuma kielimu ikiwepo Mikoa ya Lindi, Mtwara, Shinyanga, Katavi, Kigoma, Ruvuma, Tabora na Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2011/2012 na mwaka 2012/2013, jumla ya Walimu wa sekondari 549 na Walimu wa msingi 441 walipangwa Mkoani Lindi. Serikali pia imejenga madarasa 3022, nyumba za Walimu 1247 na kununua madawati 46,385 kwa ajili ya shule za msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali imejenga nyumba za walimu 328, madarasa 820, matundu ya vyoo 1,023 na maabara 52 kwa shule za sekondari. Katika mpango wa MMES II, Mkoa wa Lindi umepangiwa kukarabatiwa shule 45 na katika hizo, shule 22 tayari zipo katika maeneo yasiyofikika na zinaendelea kukarabatiwa. Vile vile kupitia chenji ya rada, Serikali imenunua zaidi ya vitabu 401,941 kwa ajili ya shule za msingi za Mkoa wa Lindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudhi hizi za Serikali na wananchi wa Mkoa wa Lindi kwa pamoja zimesaidia sana kuongeza idadi ya shule za msingi kutoka shule 72 mwaka 1961 hadi shule 485 mwaka 2013 na kutoka shule mbili za sekondari yaani (Lindi Sekondari na Mkonge sekondari) mwaka 1961 hadi kufikia shule 115 za Serikali mwaka 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na juhudhi hizo, mwaka 1976, Serikali ilianzisha Chuo cha Ualimu, Nachingwea kilichopo Mkoani Lindi ili kupata Walimu wa kutosha. Aidha, mwezi Aprili mwaka jana, mwaka 2012, Chuo cha VETA cha Mkoa wa Lindi kilifunguliwa ili kuwasaidia vijana wengi kupata stadi za fani mbalimbali za ufundu.

**MHE. FAITH M. MITAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa Walimu wengi wanaopangiwa kufundisha ndani ya Mkoa wa Lindi wanaripoti na kuondoka mara baada ya kuripoti. Je, Serikali iko tayari kutengeneza mpango maalum wa motisha kwa ajili ya Walimu ambao wamepangiwa kufundisha Mkoa huu wa Lindi ili waweze kwenda kufundisha mikoa hiyo? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri amesema kwamba Mkoa huu umepangiwa pesa za kutosha, lakini pamoja na hali hiyo shule za msingi na shule za sekondari bado zina hali mbaya katika majengo na vifaa vyta kufundishia. Je, Serikali iko tayari kutengeneza mpango wa makusudi ili hizi shule ziweze kufanyiwa ukarabati na ziweze kupata vifaa vyta kufundishia pamoja na vifaa vyta maabara?

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Faith, Mbunge kutoka Mkoa wa Lindi. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu!

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli baadhi ya maeneo Walimu wanafika, Serikali inawapanga, wanaripoti wanarudi. Lakini si wengi sana, ndiyo maeneo ambayo nimeyataja, maeneo ya mazingira magumu na ambayo labda sehemu zingine hayakuweza kupata nafasi za kufanyiwa mambo mazuri ya elimu kama Mikoa ya Tabora, Shinyanga, Kigoma, ikiwemo na hiyo mikoa anayotaja Mheshimiwa Mbunge Mikoa ya Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inachokifanya kama alivyosema kwamba inatoa upendeleo maalum, tumesema kwamba tutakarabati shule 1,200 kwenye bajeti ya mwaka jana na mwaka huu na mwaka ujao mpaka mwaka 2015 na Mikoa ya Lindi au na Mikoa ya Mtwara na mingine ambayo nimeitaja hapo imo katika mpango huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni kwa ajili ya kupendelea na tunaposema kwamba tunapanga Walimu wengi na tunapeleka madawati mengi na hata hivi vifaa vyta maabara vile vile tunapendelea mikoa kama hii. Kwa hiyo, nataka tu nihamhakikishie Mbunge kwamba Serikali inafanya upendeleo katika kupeleka huduma hizo katika mikoa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lingine amesema kwamba, masuala ya majengo vifaa, vifaa vyta maabara na vingine, vitabu vyta kufundishia na kujifunzia. Jibu ni hilo hilo kwamba, tunatoa upendeleo katika Mikoa hiyo ya Kusini ili angalau iweze kulingana na mikoa mingine ambayo tayari ilishaendalea hata kipindi kabla ya uhuru.

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Serikali inalitambua tatizo kubwa sana la ukosefu wa Walimu wa masomo ya sayansi kwa mikoa hii ya pembezoni. Je, Serikali imejipanga namna gani kuhakikisha inatuletea Walimu wa kutosha wa masomo ya sayansi ili kuepuka kuendelea kuuliza maswali haya Bungeni? Ahsante. (*Makofî*)

### **NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kushukuru sana kwa swali hili kwa sababu ningeweza hata kutoa tangazo hapa kwa ajili ya kutoa ufahamu wa vijana wa kidato cha sita, ambapo sasa ili namna ya kupata Walimu wa sayansi, Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa na Timu ya Wizara tumekubaliana kwamba, kwa mwaka huu baada ya kuona ufaulu wa vijana wa sayansi wote angalau tumewachukua wengine kwenda Vyuo na wengine kwenda *Diploma*, wanaopata *principal* moja na *subsidiary II*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumesema vijana hawa wanaosoma masomo ya *PCB*, *PCM*, *CBG*, wakipata *subsidiary* tatu, zile *SSS* zikiwa tatu. Tunataka wafanye *application* pale Wizara ya Elimu kwa mwezi wa Nane na mwezi huu wa Tisa ili angalau tuwapeleke miezi mitatu kwenye vyuo ambavyo tumeshavifanyia *identification* waweze kuripoti pale. Vijana hawa tuwape mafunzo ya miezi mitatu ili kwenye mwezi wa Kumi na Moja tena, wakaungane na vijana wengine ambao tayari watakuwa walishaanza tayari masomo ya *diploma* kwa masuala ya sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni namna moja ambapo tunataka tusukume vijana wengi wakasome sayansi ili baadaye waje kuwa ni Walimu wa sayansi. Tukizingatia kwamba mwaka jana tulajiri Walimu takribani 27,000 na kitu. Lakini Walimu wa sayansi walikuwa 2,019. Kwa hiyo, inakuwa ni ngumu kugawanya kwa kweli tunapogawa Walimu wa sayansi. Namshukuru sana

Mheshimiwa Kawambwa kwa kuliona hilo na hivi tumeshaanza mgawanyo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka tutoe mwaliko kwa vijana na Wabunge wote kama mna vijana ambao wana hizo alama SSS kwenye *PCM*, *CBG*, *BCB* walete maombi Wizarani tuwachukue wakasome miezi mitatu masomo ya sayansi, halafu baadaye tuwapeleke kwenye Vyuo vya Ualimu wakaungane na wale wa *diploma* ambao walishaanza tayari.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Festus Bulugu Limbu, Mbunge wa Magu, kwa niaba yake Mheshimiwa *Engineer Mntangi!*

Na. 87

### **Kuunganisha Mikoa kwa Barabara za Lami**

**MHE. HERBERT J. MNTANGI (K.n.y. MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU)** aliuliza:-

Ni sera ya Serikali kuunganisha Makao Makuu ya Mikoa kwa barabara za lami:-

- (a) Je, Serikali inapanga kuunganisha Makao Makuu ya Mkoa wa Mwanza na Mkoa wa Simiyu (Bariadi) kupitia njia ama Vijiji vipi katika ya Salama-Kasoli, Ng'haya au Mahaha?

(b) Je, ni lini mradi huu utaanza kutekelezwa?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Dkt. Festus B. Limbu, Mbunge wa Magu, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti suala la wapi barabara ipitie itategemea ushauri wa Mikoa husika (Mwanza na Simiyu). Wizara inashauri Mheshimiwa Mbunge awasilishe mapendelekezo hayo katika vikao vya Kamati za Ushauri za Mikoa husika kwa ajili ya majadiliano ili wafikie muafaka wa barabara itakapopita ili hatimaye mapendelekezo ya vikao tajwa yawasilishwe Wizara ya Ujenzi kwa hatua zaidi.

Hata hivyo, uwepo wa barabara kuu iliyokuwa karibu na Makao Makuu mapya izingatiwe katika mapendelekezo ya wapi iunganishwe.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu utaanza pale hatua zote za maandalizi zitakapokamilika. Hatua hizo ni pamoja na uamuzi wa wapi barabara itapita, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na upatikanaji wa fedha za kufanya kazi za usanifu na ujenzi.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru kwa majibu mazuri kutoka kwa Mheshimiwa

Waziri. Hata hivyo, ninaamini kabisa Mheshimiwa Mbunge amekwishatekeleza mapendekezo haya ya kuitisha maombi Mkoani. Kikubwa ni maandalizi gani yanafanywa ili fedha ziweze kupatikana na hatimaye barabara hiyo ikishakubaliwa iweze kujengwa bila kucheleweshwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Mheshimiwa Rais ana ahadi nyingi sana za barabara, ujenzi wa barabara katika Mikoa na hata katika Wilaya. Je, Wizara inafanya maandalizi gani hasa ya fedha ili kutekeleza baadhi ya au ahadi hizo zote. Maana zingine ni za miaka tangu mwaka 2005 ikiwemo barabara ile ya kutoka Muheza kwenda Amani?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa swali la msingi alikuwa anataka kujua barabara ambayo wanataka kuunganisha Makao Makuu ya Simiyu na Makao Makuu ya Mkoa wa Mwanza ndiyo lilikuwa swali la msingi na kwamba angetaka ijengwe kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kitu cha kwanza ni kwamba kuna barabara ambazo ni barabara kuu na tumeshaanza kujenga kwa lami. Kwa mfano, barabara inayotoka Lamadi kwenda mpaka Mwigumbi tumeshaanza kujenga barabara hiyo kwa lami ambayo inapitia Bariadi. Sasa barabara kuu hizi ndiyo tulizoanza kujenga kwa kiwango cha lami kwa maana kwamba ndiyo zinaunganisha Makao Makuu ya Mikoa mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hicho ndiyo kipaumbele. Lakini haina maana kwamba barabara zingine ambazo ni za mikoa hazitajengwa kwa kiwango cha lami, bali itategemea na upatikanaji wa fedha. Mpango ambao tumeshauweka tuna mpango wa maendeleo wa miaka mitano kutoka 2011 mpaka 2016. Kwa hiyo, kuna barabara ambazo zimeainishwa kwamba hizi ni kipaumbele na zitajengwa kwa kiwango la lami, tutaanza na hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi Wizara yangu inashughulikia kujenga kilomita elfu kumi na moja nchi nzima kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo maandalizi haya pia yatategemeana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ahadi za Rais, ahadi ambayo ipo ndani ya llani ya Uchaguzi zote hizi tumeziainisha na kuweza kujua kiasi gani cha fedha tunahitaji. Kwa hiyo, Serikali itahakikisha kwamba inapata fedha zake ili tuweze kutekeleza ahadi hizi pamoja na ahadi za Mheshimiwa Rais ambazo Mheshimiwa Mntangi anazungumza zilizo katika eneo lako.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kujua tu kwa sababu kule kwetu kati ya Mkoa wa Singida na Mbeya kuna kitu kinachoonekana kuendelea, lakini kinachukua muda mrefu. Sasa ningependa kujua utekelezaji wa hii ahadi ya Rais ya kuunganisha Mkoa wa Singida na Mkoa wa Mbeya kwa maana ya ile barabara inayotoka Makongorosi kuja Rungwa, Itigi na Mkiwa, utaanza lini? (*Makofî*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa niseme tu kwamba, utekelezaji wa ahadi ya Rais wa barabara hiyo anayoizungumza kutoka Makongorosi-Itigi mpaka Mkiwa umeshaanza. Kwa sababu barabara za lami lazima tuanze na usanifu. Usanifu wa barabara tayari umeshafanyika. Sasa kinachofuata ni kupata fedha tuweze kuanza kujenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hatua ya kufanya usanifu pia ni utekelezaji wa ahadi ya Rais ambayo ameshaitoa. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa namna zozote zile kusudi barabara hiyo iweze kujengwa kwa kiwango cha lami.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali linalofuata. Sasa linaulizwa na Mheshimiwa Salum Khafani Barwany, Mbunge wa Lindi Mjini. Mheshimiwa Barwany!

Na. 88

### **Ulipaji wa Fidia kwa Wananchi Waliobomolewa Nyumba**

**MHE. SALUM K. BARWANY** aliuliza:-

Mwaka 2002 kulikuwa na mradi mkubwa wa ujenzi wa barabara ya Kibiti kuitia Lindi Mjini hadi Mingoyo ambapo baadhi ya nyumba za wananchi zilivunjwa na kustahili kulipwa fidia na kuna malalamiko kuwa fidia hiyo hairidhishi.

- (a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kufanya uchunguzi ili walalamikaji wapate malipo stahili?

- (b) Je, Serikali haioni kuwa wananchi hao wanastahili kulipwa gharama za ziada kwa usumbufu waliouputa kwa kuwa nyumba zao zilikuwa kwenye viwanja walivyomilikishwa kihalali?
- (c) Je, kwa nini hatu baada ya barabara kujengwa bado kuna nyumba zimebekwa alama za X ya kuvunjwa bila fidia na sio kwamba vipimo vimekosewa au mipaka ya barabara imepanuka?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salum Khalfani Barwany, Mbunge wa Lindi Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa kuanzia mwaka 2002 hadi 2007, Serikali ilitekeleza mradi wa ujenzi wa barabara ya Kibiti-Lindi-Mingoyo kwa kiwango cha lami. Aidha, baadhi ya nyumba na mali zilivunjwa ili kupisha ujenzi huo na hivyo wananchi husika kulipwa fidia stahiki.

- (a) Kumbukumbu tulizonazo zinaonesha kuwa, mali zote zilizoathiriwa na ujenzi wa barabara hiyo zililipwa fidia kwa mujibu wa sheria na hivyo hakuna sababu ya kufanya uchunguzi.
- (b) Hakuna malipo ya ziada yanayostahili kufanyika kwa vile fidia iliyolipwa ilizingatia Sheria ya mwaka 1967.

(c) Alama mpya za *X* zilizowekwa baada ya barabara kujengwa ni kwa ajili ya kuzingatia mipaka mipy ya eneo la Hifadhi ya Barabara kutokana na Sheria ya barabara ya mwaka 2007 ambapo eneo hili limeongezeka kwa mita 7.5 kila upande zinazostahili kulipwa fidia na alama mpya ya *X* ilizowekwa katika eneo hilo zina madhumuni ya kuwakumbusha wananchi kuwa wataondoa mali zao katika eneo hilo wakati wowote baada ya kulipwa fidia kwa mujibu wa Sheria.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kabla sijakwenda katika maswali yangu ya nyongeza, nitoe ombi kwanza kwa Mheshimiwa Waziri, kwamba, ni vema akatembelea Lindi akaona hali halisi, kwa sababu, haya majibu ambayo ameyatoa ni majibu ambayo ametengenezewa akaletewa, hajafahamu hali halisi ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende katika maswali yangu ya nyongeza mawili; swali la msingi ni malalamiko ya wananchi ambao tayari walilipwa fidia ambayo haikuzingatia taratibu na kanuni za ulipaji wa fidia ambazo wananchi wanapeleka malalamiko yao kama wanavyodai. Kwa maana hiyo basi, ni wajibu wa Serikali sasa, kuhakikisha kwamba, malipo ambayo wananchi wanalipwa kwa mujibu wa fidia yao, yanafuata taratibu zilizopo kwani, wananchi wa maeneo yale au maeneo mengi katika nchi yetu, hawajui taratibu za fidia zinalipwaje. Hivyo, ni vema

Serikali, ikatoa kauli yake; je, ipo tayari kuhakikisha kwamba, maeneo yote ambayo fidia inalipwa, inalipwa fidia stahili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili la nyongeza ni kwamba, kuna mkanganyiko sasa hivi katika hizi Wizara mbili, Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Ardhi. Wizara ya Ardhi ndio yenye dhamana ya ardhi katika nchi hii; ni Wizara ambayo tayari inatoa Hati Miliki kwa wamiliki wa ardhi katika maeneo mengi, lakini Wizara ya Ujenzi inapokuja, hatuna hakika kama kunakuwa na mashirikiano kwa kiasi gani katika Wizara mbili hizi katika kuendeleza maeneo ambayo yanatakiwa kwa miradi ya maendeleo.

### **MWENYEKITI:** Mheshimiwa Swali?

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, Wizara hizi mbili; Wizara ya Ardhi na Wizara ya Ujenzi, zina mashirikiano gani hasa katika kuhakikisha kwamba, maeneo ambayo yanapangwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo wanashirikiana katika kuhakikisha kwamba, maeneo hayo ni maeneo ambayo wananchi walimilikishwa ardhi Kisheria?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa katika kulipa fidia tunafuata Sheria ya Ardhi, kwa hiyo, ushirikiano wa Wizara ya Ujenzi na Ardhi upo. Hatuwezi sisi Ujenzi tukalipa fidia kama ile Sheria ya Ardhi ya Mwaka 1999, Sheria Namba (4), ndio inayofuatwa katika kuangalia namna gani uthamini unafanywa ili wananchi waweze kulipwa fidia stahiki. Kwa hiyo, fidia zote ambazo zinafanywa zinazingatia Sheria hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la hifadhi ya barabara, toka mwaka 1967, hifadhi ya barabara ilikuwa mita 45. Sasa mwaka 2007 tumeongeza kuwa 60. Kwa hiyo, kama Serikali, inafanya mpango wa maendeleo, wale wote ambao wako ndani ya mita 45, wale wanatakiwa wasilipwe fidia, lakini wale wa hizi mita saba ambazo zimeongezeka zile ndio lazima walipwe fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndio maana tumeweka alama za *X* za aina mbili, kuna *X* nyekundu ili kuonesha kwamba, wewe uko ndani ya hifadhi ya barabara na kuna *X* za kijani, kuonesha kwamba, hukuwa kwenye hifadhi ya barabara, lakini sasa Serikali, ina mpango wa kupanua barabara. Kwa hiyo, utastahili kulipwa fidia katika muda ule ambapo Serikali, itahitaji kufanya maendeleo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni, ninayo mamlaka ya kusimama wakati wowote na kutoa tangazo lolote ama taarifa yoyote. Sasa nasimama hapa kwa heshima kubwa sana, kwanza kabisa kutambua uwepo wa Mheshimiwa Balozi wa Marekani nchini Tanzania, yuko katika Ukumbi wa Bunge hapa ndani. (*Makofi*)

*Your Excellency, could you please stand up so that the Tanzanians recognise your presence? Thank you so much. (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lakini ili Watanzania waelewe hiki kitu; Mheshimiwa Balozi, amemaliza muda wake wa kazi

nchini Tanzania na sasa anarudi kwao Marekani, yeye na Wamarekani wengine. Kwa kweli, kwa kipindi cha kazi cha Mheshimiwa Balozi huyu katika nchi yetu ya Tanzania, sisii Waheshimiwa Wabunge, kwa niaba ya Watanzania wote, tunayo haki na heshima kubwa kumshukuru sana yeye na Serikali yake. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, yako mambo makubwa sana yamefanywa na Serikali ya Marekani kwa nchi yetu ya Tanzania na hasa kipindi hiki ambacho Mheshimiwa Balozi alikuwa hapa katika nchi yetu ya Tanzania. Yako mengi, lakini nitasema machache.

Wote tunafahamu nchi yetu ya Tanzania imefaidika na mradi mkubwa sana wa *MCC* / na //. Barabara nyingi katika nchi hii ya Tanzania zimejengwa kwa mradi huo wa *MCC* I, lakini sasa hivi tayari makubaliano na mikataba ya kuendeleza mradi wa *MCC* // yanaendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Balozi, kwa kweli tunakushukuru sana, lakini sio hivyo tu, kipindi hiki ambacho Mheshimiwa Balozi huyo yuko hapa, tumefanikiwa kupata ugeni mkubwa sana wa Rais wa Marekani, Mheshimiwa Obama kuja kutembelea nchi yetu ya Tanzania. Tulikuwa naye hapa na tuliona Watanzania kwa kweli, tulivyojisikia urafiki wetu mkubwa kati ya nchi yetu na Marekani kwa ujio wa Rais Obama. Lakini hiyo, haitoshi mafanikio mengine tuliyoyapata kwa ujio huo. (*Makofi*)

Tumepata mradi mwingine mkubwa wa *Power for Africa*, ni mradi mwingine mkubwa sana, lakini hayo yote

hayatoshi, urafiki wetu na nchi ya Marekani, umeimarishwa zaidi na masuala mengi zaidi yamefanyika na hata hivi juzi mmeshuhudia Mheshimiwa Balozi, akisaidia Wizara yetu ya Mambo ya Ndani kwa vifaa vyatya kisasa kabisa kwa ajili ya kufanya shughuli za ulinzi na usalama. (*Makof*)

Sasa sisi kama Wabunge, kwa kweli, kwa niaba ya Watanzania wote tunamtakia safari njema, maisha mrefu, lakini vilevile tunampa salamu zetu za dhati kwanza kwa Rais Barak Obama na Wamarekani wote. Vile vile tunaahidi kwamba, urafiki huu utaendelea kwa manufaa ya nchi hizo zote mbili. (*Makof*)

Mheshimiwa Balozi, kwa kweli, tunakushukuru sana *and we feel very much honoured for your presence today in our National Assembly and we wish you all the best, karibu tena.* (*Makof*)

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, niliona nikatishe shughuli hizi kidogo, tutambue uwepo wa Mheshimiwa Balozi na niyaseme hayo mambo machache. Sasa tunaweza kuendelea na Mheshimiwa Balozi, atawenza kuendelea na ratiba yake kama alivyoipanga. Ahsante sana. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na maswali. Sasa tunaenda..., bado mnataka maswali ya nyongeza?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Basi tumpe Mheshimiwa Riziki Lulida, swali la mwisho la nyongeza.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swali la nyongeza kuhusu Wizara ya Ujenzi. Katika Barabara ya Kibiti – Lindi, wananchi wa Mandawa na Kilanjelanje, walichukuliwa eneo lao ambalo kwanza, barabara iliwafuata wao wananchi wa Kilanjelanje, wakafanyiwa tathmini na wakapigwa picha kila kitu, lakini mpaka leo wale wananchi hawajalipwa fidia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri, kwanza aoneshe nia kwangu na Mheshimiwa Barwany, aende Lindi akaone ukweli na uhalisia wa hilo jambo, ili wananchi wa maeneo yale wapate haki zao za msingi. Je, Waziri atakuwa tayari kufuatana na mimi na Mheshimiwa Barwany, twende Lindi tukaiangalie hiyo hali, ili angalau wale wananchi waweze kupata haki zao? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, uko tayari kufuatana na Mheshimiwa Barwany na Riziki Lulida kwa pamoja? Majibu kwa ufupi?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwenye jibu la msingi kwa sababu, watu wanasema hawakupata fidia stahiki, nimesema tu kwamba, fidia waliyopata ni kulingana na Sheria ya Ardhi Namba 4 ya Mwaka 1999. Kwa hiyo, naweza nikaenda Lindi kwa maana ya kuangalia maendeleo ya utengenezaji wa barabara katika Mkoa wa Lindi, si kwa sababu ya kuchunguza hili. Kwa sababu, hili naamini lilitfanywa kwa kuzingatia Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitaenda Lindi kwa maana ya kutembelea barabara na miradi mingine, lakini katika hili suala kama kuna mtu ambaye anaona hakutendewa haki, basi aende Mahakamani, ndio haki iko pale.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali linalofuata, linakwenda Wizara ya Katiba na Sheria na linaulizwa na Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 89

### **Utetezi wa Wenye Mashtaka Mahakamani**

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA** aliuliza:-

Pamoja na kuamini kwamba, Mahakama zinatoa haki, lakini pia ukweli ni kwamba, upatikanaji wa haki unategemea jinsi mtu anavyojitetea au kutetewa na Wakili wake, hasa kwa wale wenye uwezo wa kifedha.

Je, ni lini Serikali, itaweka utaratibu wa kuwawezesha wasio na uwezo wa kifedha kutetewa na Mawakili?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali, inatambua umuhimu wa haki ya kuwakilishwa Mahakamani kama haki ya msingi ya raia wake. Haki hii inaanzia pale mtu anapokamatwa hata kabla ya kufikishwa Mahakamani, hata kabla ya kufikishwa Mahakamani, ambapo anapaswa kushauriwa vyema kabla ya maelezo yake kuchukuliwa kwa kupewa ushauri wa namna ya kujitetea Mahakamani, wakati shauri lake linaposikilizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nchini tunayo Sheria ya Msaada wa Kisheria katika makosa ya Jinai, yaani *Legal Aid (Criminal Proceedings) Act, Cap 21 of 1969*. Sheria hii ndio inayotumika kwa sasa katika kutoa msaada wa kisheria kwa watu wasio na uwezo kulipia gharama za ada za Mawakili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria hii imekuwa ikitumika kwa Mashauri ya Jinai yenye adhabu kubwa pekee, yaani adhabu ya kifo. Serikali, inatambua umuhimu wa kupanua huduma za Msaada wa Kisheria, ili huduma hizi ziweze kutolewa si kwa makosa makubwa tu katika Mashauri ya Jinai, bali pia kwa mokosa mengine yote na Mashauri ya Madai kwa wale wasio na uwezo wa kifedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali, iko katika mchakato wa kukamilisha taratibu za upatikanaji wa Sheria Mpya, ambayo itahusisha kuifanyia marekebisho Sheria ya sasa iliyopo, ili kuwa na Sheria moja itakayosimamia na kuratibu utoaji wa huduma ya Msaada wa Kisheria hapa nchini kwa watu wasio na uwezo wa kifedha kwa kulipia ada za Mawakili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato wa uandaaji wa Muswada wa Sheria hiyo unaendelea vizuri na muda wowote Muswada wa Sheria hiyo, utawasilishwa hapa Bungeni, ili uweze kujadiliwa na Wabunge na baadaye kupitishwa kuwa Sheria.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini napenda niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza; kwa kuwa, kwa watu wasiofahamu Sheria mambo mengi na taratibu za uendeshaji wa kesi Mahakamani ni kama zinakwenda kimizengwemizengwe. Je, Serikali, ina mpango gani wa kutoa Elimu ya Kisheria, ili watu waweze angalau kama msaada tu wa kwanza waweze kuelewa taratibu mbalimbali zinavyoendeshwa zilizopo katika uendeshaji wa kesi Mahakamani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kwa kuwa, Mheshimiwa Naibu Waziri, ameeleza kwamba, upo mchakato wa kuandaa Muswada wa Sheria, ili ziwepo taratibu za watu kupata msaada wa Kisheria, lakini kama tunavyoolewa mchakato unaweza ukachukua hata miaka 20. Sasa, je, ni lini hasa kwa kutaja, hata kama si tarehe, lakini atwambie katika Bunge hili, yaani kufikia 2015 tunaweza tukawa tumeipata hiyo Sheria?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la kwanza kwamba, Serikali ina mpango gani wa kutoa elimu ya sheria kwa wananchi, ili waweze kuelewa taratibu mbalimbali za uendeshaji wa kesi Mahakamani; kwanza kabisa napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge, kwamba, Wizara kupitia Taasisi zake mbalimbali kama vile Tume ya Kurekebisha Sheria pamoja na watoaji wengine wa huduma ya Msaada wa Kisheria wamekuwa wakifanya kazi nzuri sana katika kuelimisha umma kuelewa taratibu mbalimbali za masuala ya Kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, hivi sasa tunao Mfuko ujulikanao kama *Legal Service Facility*, ambao unatoa ruzuku kwa watoaji wa huduma mbalimbali za msaada wa kisheria, lakini pia kwa wasaidizi wa kisheria ili waweze kutoa huduma hizi nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba, hadi hivi sasa Mfuko huu wa *LSF* umekwishatoa ruzuku ya takribani Dola za Kimarekani milioni sita na laki mbili na nusu na huduma hizi zimeshafika hadi katika Wilaya 108.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Wilaya nne tu za Tabora na Wilaya tatu za Kagera pamoja na Mikoa mitatu ya Geita, Simiyu na Njombe, ndio bado haijafikiwa. Kwa hiyo, ni imani yetu kwamba, tutaendelea na huduma hii na kwa kadiri bajeti itakavyokuwa ikitiruhusu, tutajitahidi kuendelea na mpango huu wa elimu kwa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusiana na swali la pili, kuhusiana na mchakato wa Sheria ya Huduma ya Msaada wa Kisheria; napenda tu kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba, tayari maandalizi yameshafanyika. Hivi sasa rasimu ya Muswada huu iko katika ngazi ya Serikali, kuitia Baraza la Mawaziri na tunaamini ifikapo Januari, 2014 basi Muswada huu utakuwa umeshafikishwa katika Bunge lako, tayari kwa kupitishwa na Bunge.

**MHE. MOZA A. SAIDY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Nataka kumuuliza Mheshimiwa Waziri, Serikali inasemaje kuhusu Mahakama, watoto wanapotoa ushahidi Mahakamani, wanaposhuhudia matendo ya uhalifu na wanapofika Mahakamani ushahidi ule unaonekana kwamba, ni dhaifu na hauna uwezekano wa kuweza kumtolea mtu hukumu. Je, Serikali, sasa inasemaje kuhusiana na ushahidi wa watoto mbele ya Mahakama, ili wahalifu watiwe nguvuni?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kwenye ushahidi huu wa watoto inategemea ni kosa la aina gani. Kama ni masuala ya makosa ya kujamiihana kwa kweli, ushahidi wa mtoto unachukuliwa kwa uzito wa kipekee na unaweza kabisa kumtia hatiani mtuhumiwa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swali linalofuata, linakwenda Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na linaulizwa na Mheshimiwa Jasson Rweikiza.

Na. 90

### **Ajira kwa Wahitimu Wasomi wa Kilimo**

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA** aliuliza:-

Chuo cha Kilimo kilichopo Maruku katika Jimbo la Bukoba Vijiji ni kimetoa zaidi ya wahitimu wasomi 120 wa kilimo kwa mwaka 2010 na mwaka 2011 wamehitimu wasomi wa kilimo (*General Agriculture*) ngazi ya cheti lakini hawajaajiriwa licha ya kuwa na uhaba wa Maafisa Ugani nchini:-

Je, ni lini wataalam hawa wataajiriwa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA**  
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jasson Samson Rwekiza, Mbunge wa Bukoba Vijiji ni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Kilimo cha Maruku kimetoa wahitimu wa mafunzo ya kilimo katika ngazi ya

cheti tangu mwaka 2010. Mwaka 2010 idadi ya wahitimu ilikuwa 105 na mwaka 2011 idadi ya wahitimu ilikuwa 155. Hivyo jumla ya wahitimu katika miaka hiyo miwili ni 260.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnamo mwezi Septemba, 2011 Wizara ilipata kibali kutoka ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma cha kuajiri wataalam wa kilimo wapatao 4,499. Wahitimu hawa walipangiwa kazi katika Wizara, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia kibali hicho, wahitimu kutoka Chuo cha Kilimo Maruku na Vyuo vingine vyote vya Kilimo ikiwa ni pamoja na vyuo vya taasisi zisizo za Serikali walijiriwa. Aidha, kwa mwaka 2012/2013, Serikali haikutoa kibali cha ajira mpya kwa wataalam wa kada za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka huu 2013/2014, Serikali inatarajia kutoa kibali cha kuajiri wataalam wapya 1,800 wa kada mbalimbali za kilimo. Hivyo kibali hicho kitakapotolewa, utaratibu wa ajira kwa wahitimu hao utaanza. Nachukua fursa hii kuwaomba na kuwashauri wahitimu wote wa Vyuo vya Kilimo nchini kuendelea kuwa na subira wakati utaratibu huu wa ajira unaandaliwa.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na napenda kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini nina hakika kwamba kuna baadhi ya wahitimu wa miaka hii aliyoitaja ambao bado mpaka leo hawajaajiriwa, wako Jimboni kwangu ambao wanasubiri mpaka leo kupatiwa ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama anasema kwamba mwaka 2012/2013, Serikali haikutoa kibali cha kuajiri wataalam hawa haoni kwamba hili ni jambo la hatari katika kada hii ya kilimo, wakati tunasema kilimo ni uti wa mgongo na hawa vijana wamesomeshwa kwa fedha nyingi sana za walipa kodi, halafu wanakaa bila ajira. Haoni kwamba ni vizuri kuwa na utaratibu wa kudumu wa kuwaajiri siyo kuomba kibali mwaka hadi mwaka, kwamba kuwe na utaratibu ambao wahitimu hao wakitoka waajiriwe, mahitaji yao ni makubwa ili sekta ya kilimo iweze kuendelezwa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Rweikiza kwamba, ni kweli kwamba, kwa umuhimu wa sekta ya kilimo nchini ingekuwa ni vyema kwamba hawa Maafisa Kilimo ambao wanakwenda kufanya kazi za ugani huko vijijiini wawe wanapata ajira ya moja kwa moja, lakini uwezo pia wa kibajeti na siyo sisi tu Kilimo, kuna watu Nishati na idara zingine ambao nao nafahamu kwamba wana tatizo la kupokea vibali vya ajira kutoka utumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama tulivyosema kwanza, ni kweli kwamba, kuna watu wa miaka ya nyuma hawajapata ajira wako Jimboni kwake na mimi kwangu wapo. Naomba nimhakikishie tu kwamba, katika hizi 1,800 zinaweza zisitoshe, lakini tutawapa kipaumbele wale ambao wamekaa kwa muda mrefu wakisubiri ajira hiyo.

**MHE. CHARLES J. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kuzingatia hali ya ugonjwa wa mnyauko katika Wilaya ya Muleba na Bukoba, wanafunzi waliohitimu Maruku ambao Mheshimiwa Rweikiza amewazungumzia na wale wa Igabiro wamekuwa wakisaidiana na wananchi kukabiliana na ugonjwa huu wa mnyauko kwa kipindi cha miaka miwili kwa kujitolea. Je, Serikali haioni ni busara sasa ili kuhimiza moyo wa kujitolea waniruhusu wale vijana waliokuwa wakijitolea kusaidia wananchi basi wapewe kipaumbele katika hawa wafanyakazi 1,800?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikubaliane naye kwamba ugonjwa wa mnyauko ni ugonjwa ambao ni janga, lakini pia unataka ufahamu wa karibu. Sasa hawa wahitimu ambao wameweza kukabiliana na ugonjwa huo kwa maana ya kuzuia *spread* ya mnyauko kwenye Kanda ya Ziwa, tutawapa *priority* kwa sababu tayari wana ufahamu na ugonjwa huu tunafahamu kwamba, unatoka sasa Bukoba unakwenda maeneo ya Biharamulo, unataka kuzunguka mpaka kufikia maeneo ya Mkoa wa Mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni muhimu kwamba hawa wenyewe utaalam wa ugonjwa huu tutawapa kipaumbele kupambana na ugonjwa huu ambao unaathiri maisha ya watu Kanda ya Ziwa.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nina swali moja dogo la nyongeza. Pamoja na vijana wanaohitimu katika Vyuo vya Kilimo kukosa ajira, pia kumekuwa na malalamiko ya muda

mrefu sana kwa wanataaluma na watumishi wanaofanya kazi ya kufundisha katika Vyuo vya Kilimo nchi nzima. Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu wanataaluma wanapokwenda kuijendeleza, lakini wanaporudi hawapewi mishahara yao kutokana na elimu ambayo wameipata? Hawa ni pamoja na wanataaluma wanaofundisha pamoja na watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali inajua tatizo hilo na inatoa tamko gani kwa wale ambao wana malalamiko ya muda mrefu nchi nzima?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Christowaja hilo ni swali jipya kabisa, linakwenda sasa Wizara ya Utumishi. Kwa hiyo, naomba ulileté sasa kwa utaratibu rasmi ili lipate majibu ya kikamilifu kabisa kwa sababu linakwenda Wizara ya Utumishi, masuala ya ajira. Basi nimpe Mheshimiwa Devotha Likokola swali la mwisho la nyongeza.

**MHE. DEVOTHA M. LIKOKOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa katika Wilaya ya Namtumbo, Kijiji cha Msindo kuna Chuo cha Kilimo ambacho kinawasaidia sana vijana wasio na uwezo kujifunza kilimo cha mbogamboga na kilimo kingine. Je, Serikali inaweza kutambua Chuo hiki na kukisaidia ili kiweze kuimarisha masuala ya kilimo katika Mkoa wa Ruvuma?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru Mheshimiwa Devota, suala hilo Mheshimiwa Vita Kawawa alishatupatia pale kwa sababu hasa ya mahitaji ya *horticulture* na

mboga hizi za majani majani wakati mgodi huu mkubwa wa *uranium* utakapoanza, tumetaka kukipa kipaumbele maalum kilimo hicho cha mbogamboga na mambo mengine mengine ya kilimo pale kwa ajili ya kukabili hili soko la mgodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili jambo limeshatufikia, nakushukuru pia Mheshimiwa Devotha umelileta, lakini na Mheshimiwa Kawawa alishalileta, tutalifanyia kazi kwa pamoja ili kuangalia namna litakavyofaa.

Na. 91

### **Hitaji la Soko la Mahindi Kijiji cha Ntuchi – Nkasi**

**MHE. IGNAS A. MALOCHA (K.n.y. MHE. DESDERIUS J. MIPATA)** aliuliza:-

Kutokana na kauli mbiu ya Kilimo Kwanza sambamba na utoaji wa ruzuku ya pembejeo, uzalishaji wa mahindi kwa wakulima wa Kata ya Isale katika Vijiji vya Ntuchi, Kitosi, Ifundwa, Mshilihofu, Mtapenda na Isale umeongezeka sana, lakini kumekuwepo na hitaji la soko la mahindi.

Je, Serikali iko tayari kuwapunguzia wakulima hao adha kwa kuwasogezea kituo cha kununulia mahindi katika Kijiji cha Ntuchi ambacho tayari kina ghalu kubwa liliokarabatiwa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA**  
alijibu:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mbunge wa Nkasi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (*NFRA*) ni moja ya masoko makuu ya nafaka nchini. Katika mwaka huu wa fedha 2013/2014, Wakala umepanga kununua kiasi cha tani zisizopungua 200,000 za nafaka nchi nzima ambapo kati ya tani hizo Mkoa wa Rukwa unakadiriwa kutoa wastani wa tani 50,000. Aidha, katika msimu wa mwaka 2013/2014, Wakala umepanga kutumia njia mbalimbali za ununuzi ikiwemo kununua kutoka kwa vikundi vya wakulima *SACCOS* na vituo vya ununuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua uzalishaji mkubwa wa mazao ya kilimo hasa mahindi Wilayani Nkasi, Wakala umefungua jumla ya vituo vitano vya kununulia mahindi ambavyo ni Namanyere kwa Mheshimiwa Ally Kessy kule, Ntalamila, Mtenga, Kasu na Swaila.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo ya Wakala ni kununua tani 15,500 za mahindi katika Wilaya hiyo ya Nkasi kwa msimu huu ambapo wakulima wa vijiji vya karibu kama Ntuchi, Kitosi, Ifundwa, Mshilihofu, Mtapenda na Isale wanashauriwa kutumia kituo cha Ntalamila kilichopo umbali kama wa kilomita 12 kutoka Kijiji cha Ntuchi au kituo cha

Namanyere kilichopo umbali wa kama kilomita 10 hivi kutoka kijiji hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa kuweza kufikisha huduma ya ununuzi wa mahindi karibu na maeneo ya uzalishaji kila mwanzo wa msimu *NFRA* hufanya tathmini ya ufanisi wa vituo kwa msimu uliopita. Aidha, Wakala unajipanga ili uweze kuwa na vituo vyatia ununuzi vinyavyohamishika kwa maana ya *mobile collection centers* ambapo vijiji vingi zaidi vitafikiwa katika kifupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, utekelezaji wa mpango huo utazingatia gharama za uendeshaji wa vituo hivyo, pamoja na uzalishaji wa mahindi katika maeneo hayo husika.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri ninayo maswali mawili ya nyongeza. Mkoa wa Rukwa ulipangiwa kununua tani 50,000 za mahindi, lakini hadi sasa zimenunuliwa tani 30,719 na kati ya hizo wakulima wanaidai Serikali karibu bilioni nane hazijalipwa. Je, Serikali inapeleka lini fedha hizo ili kulipa deni hilo pamoja na kukamilisha tani 50,000 zilizobakia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa tani 50,000 zilizopangwa kununuliwa na Serikali ni kidogo sana ukilinganisha na uzalishaji mkubwa wa Mkoa wa Rukwa. Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza lengo hilo zaidi ya tani 50,000 ili kukidhi mahitaji ya wakulima? (*Makofii*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, Bunge lako Tukufu lilipitisha bajeti kwa ajili ya NRFA kununua mahindi katika msimu huu na ni kweli kwamba, Serikali imeshatoa fedha za awali za kununua mahindi hayo zaidi ya shilingi bilioni 30, lakini kutokana na kasi ya uuzaji, NRFA wamenunua zaidi na ni kweli wamekopa kidogo na wiki hii Serikali imeongeza tena fedha shilingi bilioni 25 kwa ajili ya kukamilisha madeni hayo na mwezi ujao watakamilisha bajeti yao kwa ajili ya NRFA kununua. Ni lengo la Serikali kununua zaidi ya tani 200,000 kwa ajili ya hifadhi ya chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, madeni haya yanalipwa, lakini Serikali itaendelea kununua mahindi hayo kwa kadiri ya bajeti yote ya fedha zilizotengwa na Bunge lako Tukufu.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii. Nami pia katika Vijiji vya Jimbo la Namtumbo na Jimbo la Peramiho, Vijiji vya Muungano, Zomba, Lugagala nao hawajalipwa fedha zao na Jimbo la Namtumbo katika Kituo cha Namabengo na vijiji vinavyozunguka hawajalipwa fedha zao walizonunuliwa mahindi kwa kipindi cha mwezi mzima. Je, katika huu mpango wa pili aliosema Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu na wao watalipwa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, madeni tunayodaiwa sasa mpaka leo ni shilingi bilioni 27, tunatoa shilingi bilioni 25,

lakini hizo 27 tunazodaiwa ni pamoja na madeni ya huduma fulani fulani kama za magunia na nini. Kwa hiyo, fedha hizi tulizotoa zinatosha madeni yote pamoja na ya huko kwa Mheshimiwa Kawawa na wananchi wote ambao wamekusanya mahindi yao kupeleka kwenye vituo vya NRFA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni katika wiki hizi mbili za mwisho ndiyo tumechukua haya mahindi kwa sababu tulijua kabisa Wizara ya Fedha itatoa fedha za kulipa, lakini mwezi huu tutakamilisha bajeti yetu yote ya fedha zilizotengwa kwa bajeti ya mwaka huu kwa ajili ya NRFA ili tuweze kununua mahindi kwa lengo tulilokusudiwa.

**MWENYEKITI:** Nashukuru sana Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Lukuvi, kwa kweli hilo ni suala la msingi sana. Nafikiri kama mtaweza kutusaidia Wabunge kupata angalau taarifa ya mwenendo wa shughuli hiyo, mtakuwa mmetusaidia sana. Kama ulivyosema, Serikali ikifanya kazi ya kununua chakula hicho kwa hifadhi ya chakula nchini kwa sasa, itasaidia sana kupunguza tatizo la kununua chakula nje baada ya kushindwa kununua chakula hicho ndani ya nchi kwa msimu huu.

Kwa hiyo, nafikiri Serikali ikituletea taarifa hizo, Wabunge wengi nadhani watafurahi kuzipata kwa sababu matatizo haya yako kwingi tu, hata kule kwangu hali ni hiyo hiyo, magunia hakuna, fedha hakuna.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na swali linalofuata, linaulizwa na Mheshimiwa Aliko Nikusukuma Kibona, Mbunge wa lleje.

Na. 92

### **Sera ya Ujenzi wa Zahanati na Upatikanaji wa Wataalam**

**MHE. ALIKO N. KIBONA** aliuliza:-

Katika llani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 Watanzania waliahidiwa kujengewa Zahanati/Vituo vya Afya kila Kata na kupatiwa wataalam, hata hivyo kuna upungufu mkubwa wa Waganga na Waugazi na Serikali inazidi kuweka masharti magumu ya watu wanaotaka kusomea fani hizo:-

Je, Serikali inafahamu kuwa inapaswa kutekeleza ahadi hiyo iliyo ndani ya llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) (K. n.y. WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aliko Nikusuma Kibona kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kuitia mpango wa maendeleo wa Afya ya Msingi MMAM imeendelea na

ujenzi pamoja na ukarabati wa vituo vya kutolea huduma za afya kwa lengo la kuboresha huduma ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010. Kuanzia 2005/2006 hadi 2011/2012, kumekuwa na ongezeko la vituo 1,284 vilivyojengwa na kufikia jumla ya vituo 6,663 nchini ikilinganishwa na vituo 5,680 vilivyokuwepo mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, tangu mwaka 2005/2006 hadi 2011/2012, Halmashauri ya Wilaya ya Illeje kuitia MMAM, imekarabati jumla ya Zahanati 22, hospitali moja na Kituo cha Afya kimoja. Halmashauri inaendelea na ujenzi wa Vituo vya Afya vinne kuitia nguvu za wananchi. Kati ya vituo hivyo, kimoja ni Zahanati ya Lubando ambayo inapanuliwa kuwa Kituo cha Afya. Serikali hutoa fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi ikiwemo kuezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa wataalam wa Afya, kuanzia Julai, 2005 hadi Juni, 2013, Wizara imepewa vibali vya kuajiri jumla ya watumishi 40,084. Hadi sasa Wizara imewapangia vituo vya kazi watumishi 30,704 sawa na 76.6%. Watumishi hawa wamepangwa kufanya kazi katika Sekretarieti za Mikoa yote, Halmashauri za Majiji, Manispaa, Miji na Wilaya zote. Idadi ya wahitimu wa kada ya afya wanaopangiwa vituo vya kazi imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Illeje kuanzia mwaka 2008/2009 hadi 2012/2013, ilipata vibali vya kuajiri watumishi 161 kati ya hao walioripoti na kupangiwa kazi ni 71. Halmashauri inashauriwa kuendelea

kutenga katika bajeti ya kila mwaka bajeti ya watumishi na Serikali itaendelea kupanga watumishi kadiri itakavyopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuongeza idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa katika vituo vya afya, lengo ikiwa ni kuongeza idadi ya wataalam wa afya nchini. Idadi ya wanafunzi watarajali (*Pre- Service*) imekuwa ikiongezeka kutoka 1,013 mwaka 2005/2006 hadi kufikia 7,956 mwaka 2012/2013. Ongezeko hili limetokana na ujenzi na ukarabati wa Vyuo vya Umma na kuiongezeka kwa vyuo binafsi vitoavyo mafunzo ya kada mbalimbali za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea na utekelezaji wa mpango wa MMAM ikiwemo ujenzi wa vituo vya kutolea huduma, kutoa mafunzo pamoja na kuajiri watumishi wa afya kulingana na upatikanaji wa rasilimali fedha.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, Halmashauri zetu nyingi hapa nchini zina uhaba mkubwa wa Waganga, mfano, mahitaji ya Wilaya ya Illeje ni Waganga 50 katika mwaka huu wa fedha, lakini walioripoti ni Waganga sita. Madaktari wanatakiwa watatu, aliyepo ni mmoja naye yupo masomoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii imesababisha huduma za afya kudorora kwa kiwango kikubwa. Je, Waziri kupitia Serikali anaweza kunisaidia au kuwasaidia Watanzania

walioko lleje namna gani anaweza akatusaidia kukabiliana na dharura hii ya upungufu wa Waganga?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, shule zetu nyingi za Kata hazina miundombinu ya kuwezesha kufaulu masomo ya sayansi na hivyo kusababisha watoto wengi kushindwa kufaulu masomo ya sayansi ambayo ni sifa ya kuingia vyuo vya uganga. Kwa maana hiyo, wanafunzi wengi wanaodahiliwa katika Vyuo vya Uganga hapa nchini wanatoka katika miji, ambao wakiajiriwa wanashindwa kufika vijijini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa swali sasa.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni kwamba, Serikali haioni uwezekano wa kupunguza ugumu au masharti ya kujiunga na Vyuo vya Uganga ili wale walioko vijijini wapate nafasi ya kusoma na baadaye waajiriwe huko vijijini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) (K.n.y. WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la watumishi kwenda katika maeneo ya lleje na kuondoka, ningeomba tu Mheshimiwa Mbunge akishirikiana na Halmashauri yake kuweka mazingira mazuri ambayo kwa kweli watumishi wakifika watacaa. Mojawapo ni kuwa na nyumba ambazo zitaweza kuwavutia watumishi katika maeneo ya kukaa. Serikali pia imekuwa ikitenga bajeti katika kusaidia suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ukiangalia kwa kweli Wizara ya Afya wamejitalidi kupunguza kwanza muda wa kukaa shulenii haswa kwa Wauguzi na kwa upande wa Waganga pia wameangalia vigezo vya kujiunga na vyuo hivyo. Kwa upande wa cheti ni 'D' tu zinazotakiwa, ukipata 'D' tatu katika masomo ya Sayansi ya Fizikia, Biolojia na Kemia unaweza kujiunga na chuo na kwa upande wa stashahada ni 'D' na 'C' mbili unaweza kujiunga.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nitampa nafasi Mheshimiwa Dkt. Mbasa, mtaalam wa afya.

**MHE. DKT. ANTHONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa moyo wa dhati. Kwa kuwa katika jibu la msingi, Mheshimiwa Waziri amesema kwamba Serikali inategemea kwamba nafasi ya wanafunzi watakaodahiliwa itaongezeka na vyuo vimeduwa vikiendeshwa na mashirika ya dini. Serikali ina mpango gani kuongeza idadi ya Walimu katika Vyuo vya Uuguzi vilivyopo Murugwanza, Ndorage na Rubya na pia kuwasaidia ruzuku?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) (K.n.y. WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeduwa ikisaidia vyuo vyake vya Serikali na vyuo binafsi kwa makubaliano maalum. Sasa kama vyuo alivyovizungumza ni vya sekta binafsi, nadhani upo mchakato ambao Serikali na vyuo binafsi vinaweza vikafanya kazi kwa pamoja. Kwa hiyo, kwa kuwa na yeye

amebobea katika eneo hili, naimani kabisa utaratibu huo anaufahamu.

Na. 93

### **Vifaa na Dawa za Walemavu Kutotozwa Ushuru**

**MHE. JITU V. SONI (K.n.y. MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYR)**  
aliuliza:-

Serikali ilitangaza kuwa dawa za walemavu hasa wa ngozi (*sun screen lotion*) havitatozwa ushuru pale vitakapoingizwa nchini:-

Je, kwa nini kumekuwa na kigugumizi mpaka sasa na hakuna uwazi katika milango ya kuingiza mizigo bandarini na viwanja vyta ndege kwa wanaoingiza vifaa na dawa hizo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) (K.n.y. WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Al-Shaymaa John Kwegyr, Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, imekamilisha mapitio ya orodha ya Taifa ya dawa muhimu ya mwezi Julai, 2013 na kujumuisha dawa za walemavu wa ngozi yaani *sun screen lotion* katika orodha

mpya. Aidha, malighafi na vifungashio vyatengenezea dawa hizo navyo vimejumuishwa kwenye orodha hiyo mpya ya mwaka 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa orodha hii mpya imewasilishwa rasmi Wizara ya Fedha tangu Agosti, 13, 2013 ili kuomba msamaha wa kodi pale vitakapoingizwa nchini na Serikali, mashirika, taasisi au watu binafsi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa sasa hospitali ya rufaa ya *KCMC* imeanzisha kitengo maalum cha kutengeneza dawa hizo hapa nchini. Wizara ya Afya, kuitia bohari ya dawa inaendelea kununua na kusambaza dawa hizo muhimu kwa wale mavu wa ngozi. Jukumu la kuzigawa dawa hizo, ni la Bohari ya Dawa kulingana na mahitaji ni la Waganga Wakuu wa Wilaya Halmashauri na uagizaji hufanywa kama inavyofanyika kwa dawa nyingine.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Niipongeze Serikali kwa juhudhi hizo lakini naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Moja, tokea tupitishe *Finance Bill* ni muda mrefu sasa, ni lini sasa Serikali itapeleka orodha hiyo katika vituo vyote vyatengeneza?

Pili, je, tunaweza kupata hiyo orodha ili tuwapelekee hao wataalam ambao wanatengeneza dawa hizo ili kama kuna dawa nyingine ambazo hazijawekwa na Wizara ya Afya waweze kuongeza ili dawa zote ambazo zinaweza kusaidia wenzetu wenyewe ulemavu wa ngozi ziwekwe kwenye orodha hiyo ili waweze kunufaika?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) (K.n.y. WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema kwamba orodha hiyo mpya imekabidhiwa Wizara ya Fedha tarehe 13 Julai, 2013 na ukikabidhi Wizara ya Fedha ndiyo kusema wao wenyewe na *TRA* ni kitu kimoja, kwa hiyo, mimi nina uhakika kabisa kwamba Wizara ya Fedha ikiifikishia *TRA* itafikisha katika kila kituo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kupatiwa orodha hiyo, tutafanya utaratibu wa kumpatia Mheshimiwa Mbunge ili aweze kuiangalia.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa watoto wenyewe ulemavu wa ngozi na hasa walio katika shule za sekondari na shule za msingi, licha ya kuwa na mahitaji ya *sun screen lotion*, lakini pia husoma kwa taabu sana kwa sababu ya tatizo la macho. Je, Serikali katika kutekeleza haki za watoto, imejiwekea mpango gani wa kuhakikisha kwamba watoto wenyewe ulemavu wa ngozi hawashindwi kuendelea na masomo na hivyo kuwapatia miwani ya bure? (*Makofii*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) (K.n.y. WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema kwamba tumeweke utaratibu wa kuwahudumia watoto ambao wana matatizo maalum. Ni suala la kila Halmashauri kama Serikali, kwanza, kuwatambua watoto wa aina hiyo na kutambua mahitaji yao na kuona ni kwa kiasi gani kwa kuanzia pale Halmashauri inaweza kuwasaidia. Pia si jukumu la Serikali peke yake, hata wazazi wanalo jukumu la kufanya hivyo kwa sababu si watoto wote ambao wana matatizo hayo wazazi wao hawana uwezo. Sasa mtoto kuzaliwa na matatizo ya ulemavu, haiondoi dhamana au dhima ya mzazi kumhudumia mtoto wake kama anavyowahudumia watoto wengine. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na maswali kwa sababu nilitumia kama dakika kumi na mbili hivi kumtambulisha Mheshimiwa Balozi lakini pia kuchukua nafasi ya Bunge kumuaga, kwa hiyo tutaendelea tumalize haya maswali.

Sasa tunaenda swali la Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, linaulizwa na Mheshimiwa Abdul Jabil Marombwa, kwa niaba yake Mheshimiwa Juma Njwayo.

Na. 94

**Mawasiliano ya Simu Delta ya Mto Rufiji**

**MHE. JUMA A. NJWAYO (K.n.y. MHE. ABDUL J. MAROMBWA)** aliuliza:-

Maeneo yote ya Delta ya Mto Rufiji na Kata za Mchukwi, Dimani na Mwambao hayana kabisa mawasiliano ya simu na baadhi ya makampuni yalishaahidi kupeleka mawasiliano:-

Je, ni lini utekelezaji huo utaanza?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa, Mbunge wa Kibiti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanzisha Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*UCAF*), kwa lengo la kufikisha huduma za mawasiliano hususan kwenye maeneo yasiyo na mvuto wa kibiashara. Aidha, Serikali kupitia Mfuko huo, imeainisha maeneo ya vijijini na kata zilizo katika bonde la Mto Rufiji ikiwa ni pamoja na kata za Mchukwi, Dimani na Mwamba na kuyaingiza katika zabuni ya awamu ya pili ya mradi wa Benki ya Dunia ambayo zabuni yake inategemewa kutangazwa mwezi Desemba, 2013 na kutekelezwa ndani ya mwaka huu wa fedha 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara yangu, kwa dhati kabisa inaendelea kuwahimiza watoa huduma

za mawasiliano kupeleka huduma hizo kwenye maeneo yenye shida ya mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kwa kutambua kwamba, kutokana na sababu zilizo nje ya uwezo wa Serikali, kumekuwa na urasimu mkubwa katika utekelezaji wa mradi wa *UCAF* unaofadhiliwa na Benki ya Dunia, Wizara yangu inazungumza na Wizara ya Fedha ili kupata mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya India wa dola za Kimarekani milioni 154 sawa na shilingi bilioni 246 kwa ajili ya kujenga minara kote nchini na kupeleka mawasiliano katika vijiji zaidi ya 2000 nchini kwa mpigo. Tukipata mkopo huu na tukikamilisha mradi wa Benki ya Dunia, tutafanikiwa kupeleka mawasiliano katika maeneo yote ambayo Wabunge karibu wote wamekuwa wanaomba yapate mawasiliano.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza, naomba kumpongeza Naibu Waziri kwa kuonyesha jitihada za kutafuta pesa ili kupunguza tatizo la mawasiliano hapa nchi kwetu lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwanza, kwa kuwa maeneo haya ya *Delta* ya Mto Rufiji, ni maeneo magumu sana kimawasiliano, hivyo kudumaa kiuchumi na kibiashara. Je, kwa nini Serikali isitoe kipaumbele maalum kwa kuyaagiza makampuni ya simu kuyaangalia maeneo haya kwa jicho la huruma kabisa hasa ukilia maanani kwamba baadhi ya makampuni hayo yalitoa ahadi?

Pili, Serikali kupitia swali langu mwaka jana, mwanzoni mwa mwaka iliahidi kwamba itajenga minara saba Jimboni Tandahimba lakini hapa navyouliza swali leo, naomba kushukuru kwa kiasi fulani kwamba hadi sasa wameshajenga minara mitatu, kwenye kata za Nanyanga, Kitama na Lyenje. Je, kata zile nne za Mihambwe, Mkoreha, Naputa na Michenjele wategemee kupata huduma hii ya mawasiliano kuanzia lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kwamba yako maeneo maalum ambayo yanahitaji upendeleo maalum kwa ajili ya kupata mawasiliano ikiwemo maeneo ya visiwa lakini vilevile maeneo ya mipaka ya nchi yetu kwa sababu yako maeneo kwenye Majimbo ya Ngara, Manyovu na maeneo ya kule ya Ziwa Tanganyika na kwingine, ambapo kwa usalama ni muhimu yapate mawasiliano na hivyo ndivyo tulivyokuwa tumefanya. Tulizungumza na makampuni ya simu yaharakishe kupeleka mawasiliano kwenye maeneo hayo hata pale ambapo mipango yake iko mbele zaidi. Kwa hiyo, napenda kumhakikisha Mheshimiwa Mbunge kwamba hilo la kutambua kuna maeneo maalum tumelifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kumshukuru Mheshimiwa Njwayo kwa kutupongeza kwa kufanikisha kupeleka minara mitatu katika maeneo saba ambayo tuliahidi. Napenda nimhakikishie kwamba wale wananchi wake wa Mihambwe, Michenjele, Mkoreha na Namaputa, wasiwe na wasiwasi, maeneo hayo yameingizwa kwenye

awamu ya pili ya mradi ya Benki ya Dunia ambapo tenda yake itatangazwa mwezi Desemba, 2013.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tumalizie swalii liliobaki, tumebakia bado na swalii moja na muda umeisha sana na linaulizwa na Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba.

Na. 95

### **Utekelezaji wa Mpango wa Mawasiliano (UCAF)**

**MHE. LOLESIA J.M. BUKWIMBA** aliuliza:-

Tatizo la mawasiliano ya simu katika kata za Nyamalimbe, Bujula, Nyamigota, Kamena, Nyachiluluma na Kaseme Wilayani Geita ni la muda mrefu, licha ya ahadi ya kutekelezwa katika Mfuko wa UCAF:-

Je, utekelezaji wa mpango huu umefika wapi na wananchi wategemee kuanza kupata huduma hiyo lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua uwepo wa matatizo ya mawasiliano katika kata mbalimbali za Wilaya ya Geita. Miongoni mwa maeneo yaliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge, yapo kwenye maeneo yenye mawasiliano hafifu na yapo yale ambayo hayana mawasiliano kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya awamu ya kwanza na awamu ya kwanza (a) ya zabuni ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, Serikali kuitia Mfuko huo inaendelea kuyaainisha maeneo yanayohitaji mawasiliano kwa kuangalia idadi ya wakazi, ukubwa wa eneo na kiwango cha ruzuku kinachohitajika. Kata za Nyamalimbe, Bujula, Nyamigota, Kamena, Nyachiluluma na Kaseme zimeingia kwenye awamu ya pili ya mradi wa Benki ya Dunia inayotarajiwa kutangazwa mwezi Desemba mwaka huu na kutekelezwa katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengine ambayo yana mawasiliano hafifu, Serikali itaendelea kuhimiza kampuni binafsi za simu za mkononi kuboresha mawasiliano katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa kutambua kwamba kutokana na sababu zilizo nje ya uwezo wa Serikali, kumekuwa na urasimu mkubwa katika utekelezaji wa mradi wa *UCAF* unaofadhiliwa na Benki ya Dunia, Wizara yangu inazungumza na Wizara ya Fedha ili kupata mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya India wa dola za Kimarekani 154 sawa na shilingi bilioni 246 kwa ajili ya kujenga minara kote nchini na kupeleka mawasiliano katika

vijiji zaidi ya 2000 nchini kwa mpigo. Tukipata mkopo huu na tukikamilisha mradi wa Benki ya Dunia, tutafanikiwa kupeleka mawasiliano katika maeneo karibu yote ambayo Wabunge wamekuwa wanaomba yapate mawasiliano kabla ya mwaka 2015 kama ilivyoahidiwa.

**MHE. LOLESTIA J.M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwanza, nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri kwamba wananchi wa Jimbo la Busanda hasa katika kata zilizotajwa wataweza kupata mawasiliano hasa katika awamu hii ya pili na tenda zitatangazwa mwezi Desemba. Sasa napenda kupata uhakika kutoka Serikalini, je, itakuwa tayari kupokea ushauri wangu kwamba mara tu baada ya tenda hizi kutangazwa na kufunguliwa rasmi, Serikali itakuwa tayari sasa kuharakisha mchakato wa kuweza kujenga minara hii ili wananchi hao ambao wako katika maeneo ya Nyachiluluma, Kaseme na sehemu mbalimbali zilizotajwa waweze kupata mawasiliano sasa maana wamesubiri sana kwa muda mrefu bila mawasiliano? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ipo tayari kupokea na inapokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge wa kwamba pale ambapo tenda hizi zitatangazwa, tutahimiza makampuni ya simu ili kuharakisha mchakato wa kupeleka mawasiliano kwenye maeneo ya kata za Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongeze tu kusema kwamba Serikali inajitahidi, licha ya changamoto nyingi zilizopo, kwa sababu ni muhimu kutambua kwamba kazi ya kupeleka mawasiliano inafanywa na sekta binafsi, haya ni makampuni ya simu binafsi. Kwa hiyo, Serikali inachowea kufanya ni ushawishi kwa upande mmoja na upande wa pili ni kutumia ruzuku ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, ambayo wakati wote huwa haitoshi na bado hatujafika mahali pa kuishurutisha kampuni kujenga mnara pale ambapo haioni haja ya kujenga mnara. Ndiyo maana tumeamua sasa kwa kutambua kwamba kuna ucheleweshaji na urasimu, tutafute fedha zetu wenyewe nyingi ili tuweze kujenga minara sisi wenyewe kwa kutumia Mfuko ili tumalize tatizo hili kwa wakati mmoja ili kabla ya mwaka 2015 kama tulivyoahidi, tuweze kuwa tumefanya mapinduzi makubwa ya kuhakikisha kwamba kila pale ambapo hakuna mawasiliano basi yapo mawasiliano. Ni imani yangu kwamba sisi ndani ya Serikali tutamalizana na kwamba dhamana ya mkopo huo itatoka ili fedha zipatikane ili itakapofika mwishoni mwa mwaka ujao, tuwe hatuulizani tena maswali ya mitandao.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, matangazo. Mheshimiwa Silinde, Katibu wa Kambi Rasmi Bungeni, ananiomba niwatangazie Wabunge wote wa CHADEMA kwamba mara baada ya kikao hiki kuahirishwa siyo kuahirishwa Mheshimiwa Silinde, mchana huwa nasitisha, kuahirisha ni jioni. Sasa ukinitaka niahirishe sasa hivi, unanifanya nivunje Kanuni. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wa CHADEMA, mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge, muda wowote basi mnaombwa kukutana

kwenye kikao kwenye ofisi ya Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Magdalena Sakaya, ambaye ni Katibu wa Wabunge wote wa CUF ndani ya Bunge, anaomba niwatangazie Wabunge wote wa *CUF* kuwa wanatakiwa kuhudhuria kikao kitakachofanyika leo baada ya kuahirisha. Mheshimiwa Sakaya na wewe sijui ni kuahirisha ama kusitisha? Wewe ni kuahirisha usiku?

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Saa saba mchana.

**MWENYEKITI:** Ni kusitisha.

Waheshimiwa Wabunge, mchana tunapomaliza shughuli za asubuhi tunasitisha Bunge na tunapomaliza shughuli za jioni ndiyo tunaahirisha. Sasa nafikiri hawa Makatibu wenzangu wawili hawa, basi kambi hizo zote mbili zitakutana baada ya kusitisha Bunge na siyo baada ya kuahirisha. Waheshimiwa Wabunge wa *CUF* tutakapositisha kikao cha Bunge kwa asubuhi hii na nyie mtakuwa na kikao chenu. Hayo ni matangazo kutoka kwa Makatibu wa Kamati za Vyama ndani ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo ndani ya Ukumbi wa Bunge, kwanza ilikuwa ni Mheshimiwa Balozi na timu yake lakini Mheshimiwa Balozi tumeshamtambua na tumemwaga rasmi. Kama nilivyosema, tunamtakia kila la kheri, Mwenyezi Mungu amsaidie, azidi kuimarisha undugu wetu.

Wageni wengine ni wanafunzi 90 kutoka shule ya sekondari ya Jamhuri Dodoma, ningeomba wasimame, karibuni sana vijana wetu, tunawatachia kila kheri katika masomo. Dunia hii ni ya sayansi na teknolojia, bila elimu itakuwa ni sayansi na teke litakalowajia. Kwa hiyo, jitahidini sana kusoma na kuzingatia masomo kuliko kitu kingine chochote. Karibuni tena siku nyingine katika ukumbi wa Bunge, mjifunze kazi zinazofanywa na wawakilishi wenu, ahsanteni sana, mnaweza kuketi. (*Makofi*)

Ninao wageni 14 kutoka Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu wakiongozwa na Dkt. Khoti Kamanga. Nyie wenzetu mnashughulikia masuala ya haki hayatofautiani na masuala ya utungaji wa sheria yanayofanywa na Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, karibuni sana. (*Makofi*)

Ninao Wanahabari tisa kutoka kikundi cha Wataalam wa Habari wakiongozwa na Bi. Asha Bani, karibuni sana. Hawa wanahabari wote ni akina mama, kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wanawake, tunatakiwa kuwapongeza sana hawa wanahabari wanawake wenzetu kwa kazi nzuri na kuamua leo kututembelea Bungeni, akina mama tunaweza na wala siyo lazima tuwezeshwe, tunaweza wenyewe. Hongereni sana kwa kazi nzuri za kuwahabarisha Watanzania mambo mbalimbali, tunathamini sana ugeni wenu, karibuni tena na siku nyingine mnaweza kuchukua nafasi kukutana hata na Wabunge wanawake ili kubadilishana mawazo zaidi, karibuni sana. (*Makofi*)

Wako wananchi wanne, kutoka Babati, Mkoani Manyara wakiongozwa na Bwana Steven Manda. Karibuni sana wananchi kutoka Babati, tunawashukuru na siku nyingine karibuni sana kwenye Bungeni hili. (*Makofi*)

Tunao Wakufunzi watatu kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania ambao ni Bi. Rose John, Ndugu Mussa Omary na Ndugu Meshack Katisho. Vilevile yuko Rais wa Chuo Kikuu Huria ambaye ni Bwana Mussa Omar, Waziri wa Habari, Bwana John na Waziri wa Michezo, Meshack Katisho. Karibuni sana kwenye shughuli zetu, mmeona Mawaziri wenzenu humu ndani wanavyofanya kazi, tunaamini na nyie kwenye Baraza lenu mko imara kabisa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, wakati naendelea na shughuli za kuendesha kikao hapa, kuna Wabunge kadhaa wameniandikia wakisema kwamba hii Miswada ambayo inaendelea ndani ya ukumbi wa Bunge hawana nakala ya Miswada hiyo. (*Makofi*)

Naomba tu niwaarifu Waheshimiwa Wabunge, Miswada hii yote tulishagawiwa kabla hatujamaliza Mkutano wa Bunge uliopita na iliwekwa yote kwenye *pigeon hole* zetu. Sasa kama kuna mtu kwa bahati mbaya au kwa namna moja ama nyingineyo, hakufanikiwa kupata nakala ya Miswada hiyo basi awasiliane na ofisi ya Katibu wa Bunge, lakini kama kugawiwa ilishagawiwa toka Mkutano uliopita.

Mheshimiwa Iddi Azzan, Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* ananiomba niwatangazie Wabunge wanamichezo

kuwa, mazoezi yanaendelea ya kijiandaa na mashindano ya Bunge la Afrika Mashariki, yatakayofanyika nchini Uganda. Hivyo, Waheshimiwa Wabunge wanamichezo wanaombwa kuhuduria bila kukosa kujifua tayari kwa mashindano hayo na kuleta ushindi katika Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, ni taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Iddi Azzan.

Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwamba leo tarehe 4/9/2013, saa saba mchana kutakuwa na kikao katika ukumbi namba 231. Nawashauri wajumbe wa Kamati hiyo mkutane mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge.

Mheshimiwa James Lembeli, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Ardhi, Maliasili na Mazingira na yeye ameniomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kwamba watakuwa na kikao leo katika ukumbi Na. 227, ghorofa ya pili jengo la utawala. Naomba pia na wao Mheshimiwa James Lembeli kama haitakuwa na tatizo mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge mnaweza tu kukutana, tunaweza kuzisitisha muda wowote kuanzia sasa.

Mheshimiwa Juma Kapuya, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, na yeye vilevile anawaomba wajumbe wa Kamati hiyo wakutane leo katika kikao cha Kamati yao katika ukumbi wa Pius Msekwa. Naomba pia kuwashauri wajumbe wa Kamati hiyo ya

Miundombinu na wao wanaweza tu kukutana muda wowote nitakapokuwa nimesitisha shughuli hizi.

Waheshimiwa Wabunge, jana niliwapata taarifa ile ya mabadiliko ya ratiba na nimeletewa hapa maelekezo sasa kwamba kutokana na kuahirishwa kwa Miswada ile niliyoisema jana, muda wa Mkutano wa 12 wa Bunge ambao awali ultarajiwa kuwa wa wiki tatu, sasa umepungua na kuwa wa wiki mbili. Kwa maana hiyo, Bunge sasa litaahirishwa siku ya Ijumaa tarehe 6 Septemba, 2013. (*Makofi*)

Kwa hiyo, imenipasa niwape hayo maelekezo, navyowafahamu Wabunge mko imara na tayari kabisa kwa sababu kila mtu sasa atakuwa anawaza kurudi haraka Jimboni basi angalau muanze kupangapanga hiyo mipango yenu kwa kuzingatia hiyo tarehe ambayo Bunge litaahirishwa. Suala la kuhoji wanaoafiki hoja hiyo waseme ndiyo, litafanywa na Spika siku ya kuahirishwa kikao hicho cha Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge kifungu kidogo cha tatu na cha nne, kinaweka utaratibu wa Kamati ya Uongozi kupanga ratiba za kazi lakini vilevile kusimamia majukumu ya Kamati nyingine. Sasa kwa taarifa nilizopata hapa, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala bado inaendelea na shughuli ya Muswada ambao ulikuwa uingie asubuhi hii. Kwa hali hiyo, sasa nitasitisha shughuli hizi za Bunge, tutakutana tena saa kumi na moja jioni ndani ya ikumbi huu.

*(Saa 05.05 Asubuhi Bunge lilitishwa hadi Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilitrudia)*

*Hapa Naibu Spika (Mheshimiwa Job Ndugai)  
Alikalia Kiti*

## **MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa  
Mwaka 2013, (*The Constitutional Review  
(Amendment) Bill, 2013*)**

*(Kusomwa Mara ya Pilli)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Kikao chetu cha Saba cha Mkutano wetu wa Kumi na Mbili na kama alivyosema Katibu, tunaanza sasa kushughulikia Marekebisho ya Muswada wa Sheria wa Mabadiliko ya Katiba. Jambo hili ni muhimu, naomba ushirikiano wenu wote. Moja kwa moja, naomba nimwite Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Chikawe, karibu Mheshimiwa Waziri!

---

**ISSN 0856 -035X**

---

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

***BILL SUPPLEMENT***

**No. 3**

***7<sup>th</sup> June, 2013***

*to the Gazette of the United Republic of Tanzania No. 23 Vol  
94 dated 7<sup>th</sup> June, 2013*

Printed by the Government Printer, Dar es Salaam by Order of  
Government

---

## **NOTICE**

---

This Bill to be submitted to the National Assembly is published for general information to the public together with a statement of its objects and reasons.

Dar es Salaam,  
13<sup>th</sup> May, 2013  
*Cabinet*

OMBENI Y. SEFUE,  
*Secretary to the*

## **A BILL**

*for*

**An Act to amend the Constitutional Review Act, Cap.  
83.**

**ENACTED** by Parliament of the United Republic of  
Tanzania.

Constru  
ction  
Cap.83      1. This Act may be cited as the  
                 Constitutional Review (Amendment) Act,  
                 2013 and shall be read as one with the  
                 Constitutional Review Act, hereinafter

referred to as the “principal Act”.

Amend  
ment of  
section  
3

**2.** The principal Act is amended in section 3, by inserting in the appropriate alphabetical order the following new definitions:

“Draft Constitution” means the draft constitution prepared by the Commission on the basis of collected views and recommendations of the public under this Act;

“Standing Orders” means the Standing Orders of the Constituent Assembly made under this Act”.

Amend  
ment of  
section  
22

**3.** Section 22 of the principal Act is amended-

(a) in subsection (1)(c) by deleting the word “drawn” appearing in the opening phrase of that paragraph and substituting for it the words “appointed by the President”.

(b) by inserting the following provisions after subsection (2):

“(2A) The President shall invite each group specified under subsection (1) (c) to submit to him a list of not more than three names of persons for appointment as members:

Provided that, the list shall for every name proposed, indicate the age,

gender, experience, qualifications and place of abode of such person.

(2B) In appointing members of the Constituent Assembly under subsection (1)(c), the President shall have regard to:

- (a) qualifications and experience of persons nominated; and
- (b) gender balance.

Amend  
ment of  
section  
24        4. The principal Act is amended in section 24 by deleting subsection (4) and substituting for it the following:

“(4) The Clerk of the Constituent Assembly shall, upon consultation with the Deputy Clerk and relevant institutions, appoint from the National Assembly, the House of Representatives and relevant institutions, such number of staff as may be appropriate for the effective performance of functions and exercise of powers of the Constituent Assembly.”

Amend  
ment of  
section  
27        5. The principal Act is amended in section 27 by deleting subsection (2) and substituting for it the following:

“(2) There shall be freedom of opinion in the debates of the Constituent Assembly and such

opinion of the members shall not be questioned in any court or place outside the Constituent Assembly.

(3) The procedure of debates in the Constituent Assembly shall be prescribed in the Standing Orders".

Amend  
ment of section 28  
28

**6.** The principal Act is amended in section 28 by adding immediately after subsection (2) the following provision:

"(3) Without prejudice to subsections (1) and (2), the Constituent Assembly shall deliberate on the Draft Constitution within a period not exceeding seventy days from the date on which the Constituent Assembly convened.

(4) The Chairman of the Constituent Assembly, after consultation with the Vice Chairman may, upon approval by the President in agreement with the President of Zanzibar, extend the period under subsection (3) for a period of not more than twenty days."

## OBJECTS AND REASONS

---

This Bill makes legislative proposals for amending the Constitutional Review Act, Cap. 83, by defining the terms "Draft Constitution" and "Standing Orders" which are referred to in the Act, but were not defined. It also proposes the amendment of section 22 in order to provide the procedures in which 166 Members of the Constituent Assembly referred to in section 22(2)(c) will be appointed.

Section 24(4) is deleted and substituted with a new subsection (4) which intends to allow the Clerk and his Deputy to appoint staff of the Constituent Assembly from other institutions including the National Assembly and the House of Representatives. The existing subsection (4) confined the appointment of staff to the two institutions. Further, section 27 is amended by deleting subsection (2) and substituting for it new subsections (2) and (3) in order to provide freedom of opinion in the debate of the Constituent Assembly. The Bill also proposes to amend section 28 to provide for the duration of the Constituent Assembly.

Dar es Salaam,  
8<sup>th</sup> May, 2013

MATHIAS M. CHIKAWE,  
*Minister for Constitutional  
and Legal Affairs*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 ya Kanuni za Kudumu za

Bunge, Toleo la Mwaka 2013, naomba kutoa hoja kwamba Muswada uitwao Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa Mwaka 2013 (*The Constitutional Review (Amendment) Act, 2013*) sasa usomwe kwa Mara ya Pili na Bunge lako Tukufu naomba liujadili na hatimaye liupitishe kuwa Sheria ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kutoa maelezo kuhusu Muswada huu, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo na kupitia kwao niwashukuru Waheshimiwa wajumbe wote wa Kamati kwa michango na kazi kubwa waliyoifanya katika kuboresha Muswada huu. Maoni na ushauri wao kwa kiasi kikubwa yametusaidia sana sisi Serikali kuboresha Muswada huu kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho. Kwa hakika niseme, Jedwali hili la Marekebisho ni kazi ya Kamati kwa ujumla. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, Namba 8 ya Mwaka 2011 (Sura ya 83), ilipitishwa na Bunge hili na kufanyiwa Marekebisho kupita Sheria Namba 2 ya mwaka 2012. Marekebisho hayo yalifanywa katika Sehemu ya Tatu inayohusiana na Uundaji wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba kwa nia ya kuiboresha Sheria hiyo na kuwezesha kuwepo kwa Mwafaka wa Kitaifa katika kuendesha mchakato wa kuipata Katiba Mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu ni mwendelezo wa nia ya dhati ya kuwepo kwa Mwafaka wa

Kitaifa katika mchakato wa kupata Katiba Mpya. Kama Waheshimiwa Wabunge wanavyofahamu, Tume ya Mabadiliko ya Katiba, ikiongozwa na Mzee wetu, Mheshimiwa Jaji Joseph Sinde Warioba, imefanya kazi nzuri sana ya kukusanya maoni ya wananchi kuhusu Katiba Mpya na kuandaa Rasimu ya Katiba ambayo imejadiliwa kwenye Mabaraza ya Katiba. Naambiwa wataalam waliokuwa wanakusanya maoni haya, kundi la mwisho limerejea leo pale Dar es Salaam. Naipongeza Tume ya Mabadiliko ya Katiba kwa kazi hiyo nzuri iliyoifanya hadi sasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nawashukuru sana wananchi kwa kushiriki vyema katika mchakato huu. Hatua inayofuata sasa ni Tume hiyo kuandaa Ripoti na Rasimu ya Katiba ambayo itawasilishwa kwa Rais ambaye naye ataiwasilisha kwenye Bunge Maalum la Katiba ndani ya siku thelathini baada ya kuipokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili hatua hiyo ifanyike kwa ufanisi, Serikali imeandaa Muswada huu ambao unapendekeza kuifanyia marekebisho Sehemu ya Tano ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, Sura ya 83, Toleo la mwaka 2012, inayohusiana na Bunge Maalum.

Muswada huu una Sehemu Moja tu. Ni Muswada mfupi sana ambao Wizara yangu imewahi kuleta ndani ya Bunge hili. Ibara ya 1 inahusu jina la Muswada ambao tunakusudia uitwe, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa Mwaka 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 2 ya Muswada inapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 3 kwa kuingiza tafsiri ya maneno 'Rasimu ya Katiba' na neno 'Kanuni'. Katika Ibara hiyo, maneno 'Rasimu ya Katiba' yametafsiriwa kumaanisha Rasimu ya Katiba ambayo imetayarishwa na Tume chini ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba na neno 'Kanuni' limetafsiriwa kumaanisha Kanuni za Bunge Maalum. Lengo ni kutoa ufanuzi wa maneno hayo kwa ajili ya matumizi bora ya Sheria hiyo. Kwa namna Sheria ilivyo sasa, maneno hayo hayajapewa tafsiri yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 3 ya Muswada inapendekeza kukifanyia marekebisho kifungu cha 22(1)(c) ili kumpa Rais, kwa kushauriana na Rais wa Zanzibar, mamlaka ya kuteua wajumbe 166 wa Bunge Maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kifungu cha 22 pia kinafanyiwa marekebisho kwa kuongeza Kifungu kidogo kipyga cha (2A) mara baada ya kifungu kidogo cha (2). Kifungu kidogo cha (2A), kinalenga kumwezesha Rais kualika kila kundi lilitotajwa katika kifungu kidogo cha (1)(c), kuwasilisha kwake majina ya watu watatu ili wafikiriwe kwa uteuzi kuwa wajumbe wa Bunge Maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu kidogo kipyga cha (2B) kinaainisha sifa za wajumbe wa Bunge Maalum. Hapo awali, Sheria haikuainisha utaratibu wa upatikanaji wa Wajumbe wa Bunge Maalum pamoja na sifa zao. Sheria ilitaja tu makundi ambapo wajumbe hawa wanetoka lakini haikutaja watatokaje huko mpaka waingike katika Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, aya ya C ya Jedwali la Marekebisho, inapendekeza kuongeza kifungu kipyä cha 22A. Kifungu kipyä cha 22A(1) kinapendekeza kuwa Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katibu wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, wasimamie mchakato wa kumchagua Mwenyekiti wa Muda wa Bunge Maalum ili kusimamia uandaaji na upitishwaji wa Kanuni za Bunge Maalum na kuendesha uchaguzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum. Mwenyekiti huyo atakapochaguliwa, kazi zake ni hizo mbili tu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kifungu kidogo cha (2) kinaweka masharti ya kumwondolea Mwenyekiti wa Muda sifa za kugombea nafasi ya Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum kwani ndiye atakayesimamia uchaguzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum. Kwa hiyo, mwenyewe hatapata nafasi ya kugombea.

Mheshimiwa Naibu Spika, aya ya D ya Jedwali la Marekebisho, inapendekeza kufanya marekebisho katika Ibara ya 23 kwa kuongeza Ibara ndogo ya (4) mara baada ya Ibara ndogo ya (3). Lengo ni kuainisha masharti ya uteuzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum. Sifa za Mwenyekiti na Makamu wake zitaainishwa kwa kirefu zaidi katika Kanuni za Bunge Maalum ambazo zitapitishwa na Bunge hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 4 ya Muswada, inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 24

kwa kufuta Ibara ndogo ya (4) na kuweka badala yake Ibara ndogo za (4) na (5), kama inavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho. Ibara ndogo ya (4) inampa Katibu wa Bunge, kwa kushauriana na Naibu wake na Taasisi za Umma, mamlaka ya kuteua watumishi wa Bunge Maalum kutoka katika Bunge la Jamhuri, Baraza la Wawakilishi na Taasisi za Umma. Ibara ndogo ya (5), inapendekeza kuweka masharti kwa Taasisi za Umma kuwaruhusu watumishi watakaoteuliwa kutoka katika taasisi hizo kuwa watumishi wa Bunge Maalum kwa utaratibu wa kuazimwa. Hapo awali, uteuzi wa watumishi hao ulikuwa ni kwa watumishi wa Bunge na watumishi wa Baraza la Wawakilishi pekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 5 ya Muswada, inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 27 kwa kufuta kifungu kidogo cha (2) na kuweka badala yake vifungu vidogo vya (2) na (3). Kifungu kidogo cha (2) kinaweka masharti yanayotoa uhuru wa maoni katika mijadala ya Bunge Maalum. Inapendekezwa kuwa, maoni ya wajumbe katika Bunge hilo Maalum, yasihojiwe Mahakamani au sehemu yoyote nje ya Bunge Maalum. Aidha, kifungu kidogo cha (3), kinapendekeza kuwa utaratibu wa kuendesha mijadala katika Bunge Maalum, uainishwe katika Kanuni za Bunge hilo. Hapo awali, Sheria ilikuwa haijaweka kinga hii kwa Wajumbe wa Bunge Maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 26 kinafanyiwa marekebisho kwa kuongeza vifungu vidogo vya (3) hadi (7) mara baada ya kifungu kidogo cha (2), ambapo vinaweka utaratibu pale ambapo Katiba inayopendekezwa

haijaungwa mkono kwa idadi ya theluthi mbili ya idadi ya Wajumbe wote wa Bunge Maalum kutoka Tanzania Bara na theluthi mbili ya idadi ya Wajumbe wote wa Bunge Maalum kutoka Tanzania Zanzibar. Inawezekana ikatokea ndani ya Bunge hilo, theluthi mbili isipatikane ama kwa makundi yote mawili au kwa kundi moja na hapa tunaweka utaratibu nini kifanyike katika hali kama hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 6 ya Muswada, inapendekeza kufanya marekebisho katika kifungu cha 28 kwa kuongeza vifungu vidogo vipyta vya (3) na (4). Lengo la marekebisho haya ni kuweka muda ambao Bunge Maalum litatumia kujadili Rasimu ya Katiba. Inapendekezwa kuwa Rasimu ya Katiba ijadiliwe kwa muda usiozidi siku sabini (70) kuanzia tarehe ya kuitishwa kwa Bunge Maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Ibara ndogo ya (4) inampa Mwenyekiti wa Bunge Maalum, mamlaka ya kuongeza muda wa majadiliano uliotolewa na Ibara ndogo ya (3) yaani zile siku sabini, Mwenyekiti anayo mamlaka ya kuongeza muda kwa kipindi atakachoona kinafaa ili kuwezesha kukamilika kwa shughuli za Bunge Maalum. Isipokuwa, Mwenyekiti wa Bunge Maalum atatekeleza mamlaka hayo baada ya kushauriana na Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum na baada ya mashauriano hayo kupata ridhaa ya Rais ambaye naye atashauriana na Rais wa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisema Muswada huu ni mfupi sana, sasa baada ya maelezo haya, napenda, kuitia kwako, kuwaomba Waheshimiwa Wabunge,

kuujadili Muswada huu kwa kina na kuupitisha katika hatua zake zote mbili, yaani kusomwa Mara ya Pili na Kusomwa kwa Mara ya Tatu. Ninayo imani kubwa sana na Bunge lako Tukufu kwamba litaridhia Marekebisho yote yanayopendekezwa na kwamba litakubali marekebisho haya yawe sehemu ya Sheria za nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makof*)

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**  
Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki!

(*Hoja imetolewa iamuliwe*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kuwasilisha kwa umahiri mkubwa hotuba yako. (*Makof*)

Makatibu, nina hakika baadhi ya Wabunge hawana nakala za ile Rasimu ya mwanzo na nina hakika kabisa kwamba ofisini ziko za kutosha, kwa hiyo, ingefanyika juhudu kuhakikisha kwamba ambaye hana anaipata kwa haraka sana iwezekanavyo. Waheshimiwa Wabunge, tuvumiliane wakati Makatibu wangu wanafanyia kazi jambo hilo. (*Makof*)

Sasa tumwite Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, ili aweze kusoma maoni ya Kamati hiyo. Namwona Mheshimiwa Gosbert Blandes

anakuja kwa ajili ya kusoma hotuba kwa niaba ya Kamati. Karibu sana Mheshimiwa Gosbert Blandes. (*Makofî*)

**MHE. GOSBERT B. BLANDES (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI, SHERIA NA UTAWALA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana, naomba kutoa maoni ya Kamati ya Sheria na Utawala kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Katiba, 2013 yaani *The Constitutional Review (Amendment) Act, 2013*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili 2013, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria na Utawala kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Katiba, 2013 yaani *The Constitutional Review (Amendment) Act, 2013*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilikutana na Mheshimiwa Mathias M. Chikawe, Waziri wa Katiba na Sheria, pamoja na Mheshimiwa Jaji Fredrick M. Werema kwa mara ya kwanza katika Ofisi Ndogo ya Bunge Dar es Salaam, mnamo tarehe 29 Julai 2013, ili kupokea maelezo kuhusu Muswada husika. Aidha, baada ya hapo, Kamati ilikutana nao katika vikao mbalimbali vilivyofanyika kwa nyakati tofauti, Dar es Salaam pamoja na Dodoma katika Mkutano wa Kumi na Mbili wa Bunge ulioanza tarehe 27, Agosti 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maelezo yake, Waziri wa Katiba na Sheria alieleza Kamati kuwa Muswada wa

Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba 2013 unakusudia kufanya marekebisho katika baadhi ya vifungu vya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, Sura ya 83, Toleo la 2012. Marekebisho haya kwa ujumla yanalenga kuiboresha Sheria hiyo kwa kurekebisha kasoro za kisheria, pamoja na kuziba mianya iliyoachwa ili Sheria hiyo iweze kukidhi matakwa halisi ya mchakato wa kupata Katiba Mpya.

Mhehsimiwa Naibu Spika, baada ya kupokea maelezo ya Waziri, Kamati ilialika wadau mbalimbali kwa mujibu wa Kanuni ya 84(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili 2013, ili kupata maoni yao kuhusu mapendekezo ya Muswada katika vifungu vinavyofanyiwa marekebisho kwa lengo la kuisaidia Kamati katika uchambuzi wa Muswada huu.

Mhehsimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wadau wote ambao kwa nyakati tofauti waliwasilisha maoni yao mbele ya Kamati kwa mdomo na kwa njia ya maandishi. Maoni yao, michango na maelezo ya ufanuzi waliyotoa mbele ya Kamati vimesaidia kwa kiasi kikubwa kuiboresha Muswada huu.

Mhehsimiwa Naibu Spika, maoni ya Kamati. Baada ya kuelezea masuala ya awali katika utangulizi wa taarifa hii, naomba sasa niwasilishe kwako maoni ya Kamati ambayo kwa kiasi kikubwa yametokana na uchambuzi wa Wajumbe wa Kamati katika vifungu vya Muswada.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu uliposomwa kwa Mara ya Kwanza hadi kuwasilishwa katika Kamati, ulikuwa na Ibara sita (6) zilizokuwa zinakusudia kufanya marekebisho katika vifungu mbalimbali vya Sheria Mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Mtoa Hoja, kwa nyakati tofauti aliwasilisha mbele ya Kamati marekebisho na nyongeza mbalimbali kwa madhumuni ya kufanya marekebisho katika vifungu vilivyokuwa vinarekebishwa awali pamoja na marekebisho katika vifungu vingine vya Sheria Mama. Marekebisho na nyongeza hizo zimebadili mtiririko wa Ibara na idadi yake kama ambavyo Jedwali la Marekebisho linavyoainisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mjadala wa Kamati, Wajumbe walikubaliana kimsingi katika baadhi ya Ibara za Muswada kutofanywa marekebisho yoyote. Hivyo basi, maoni ya Kamati katika taarifa hii yamejikita katika Ibara ambazo zilikuwa na mjadala mrefu na mgawanyiko wa maoni baina ya Wajumbe ambapo baadaye kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, maoni yaliyokubaliwa na Wajumbe walio wengi ndio yanayowasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 2 ya Muswada inalenga kufanya marekebisho katika kifungu cha 3 cha Sheria Mama ili kuongeza maneno "Rasimu ya Katiba" na neno "Kanuni" ambayo yametumika katika Sheria hiyo lakini hayakuwa yametolewa tafsiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, baada ya uchambuzi, Wajumbe wa Kamati walipendekeza kuwa tafsri ya maneno ya "Rasimu ya Katiba" katika Muswada ifanyiwe marekebisho na itafisriwe kumaanisha, "Rasimu ya Katiba ambayo imetayarishwa na Tume kwa mujibu wa Sheria hii", ili kujumuisha maoni ya wananchi pamoja na vyanzo vingine vilivyoainishwa katika Sheria Mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanya marekebisho kama ambavyo Kamati ilishauri na marekebisho hayo yanaonekana katika Jedwali la Marekebisho ambalo limeambatishwa pamoja na Muswada huu na tafsiri ya maneno "Rasimu ya Katiba" inasomeka kumaanisha, "Rasimu ya Katiba ambayo imetayarishwa na Tume chini ya Sheria hii".

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 3 ya Muswada inapendekeza kufanywa marekebisho katika kifungu cha 22 cha Sheria Mama kwa lengo la kuweka utaratibu wa kuwapata Wajumbe 166 wa Bunge Maalum kutoka katika makundi mbalimbali ya kijamii. Muswada unapendekeza kuwa uteuzi wa Wajumbe hao ufanywe na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania baada ya kushauriana na Rais wa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo linalohusu Mamlaka ya Uteuzi, kulikuwa na mawazo mbalimbali ambapo baadhi ya wadau na Wajumbe walikuwa na maoni kwamba Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania asifanye uteuzi wa Wajumbe 166 bali Wajumbe hao wateuliwe na taasisi na asasi zao wenyewe. Mawazo

ya namna hii yalitokana na dhana kwamba, endapo Wajumbe 166 wa Bunge Maalum watateuliwa na Rais, uwakilishi wa kutoa maoni kwa uhuru na uwazi utapungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine, wapo baadhi ya wadau na Wajumbe ambao walipendekeza kuwa uteuzi wa Wajumbe 166 wa Bunge Maalum ufanywe na Rais lakini, Rais afanye uteuzi huo kwa kuzingatia kikamilifu mtiririko wa mapendekezo ya kila kundi lililoainishwa katika kifungu kidogo cha 22 (1) (c) na endapo hatazingatia mtiririko wa mapendekezo ya kundi mojawapo, Rais afanye mrejesho kwa taarifa kwa kundi husika juu ya sababu za kutozingatia mtiririko wa mapendekezo yaliyowasilishwa kwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya majadiliano na mashauriano baina ya Kamati na Serikali, Kamati ilikubaliana kwamba Rais apewe mamlaka ya kufanya uteuzi wa Wajumbe 166 wa Bunge Maalum bila kupewa masharti ya kufanya mrejesho kwa kundi ambalo hakuzingatia vipaumbele vya mapendekezo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni haya yanazingatia ukweli kwamba, uteuzi wa Wajumbe utakaofanywa na Rais katika kila kundi lililoainishwa katika kifungu cha 22(1)(c), utazingatia majina ya watu wasiozidi watatu (3) yaliyowasilishwa na taasisi yenyewe kwa Rais ili mmoja kati ya watu hao ateuliwe kuwa Mjumbe anayefaa kuiwakilisha taasisi hiyo katika Bunge Maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kitendo cha taasisi kupendekeza majina ya watu wasiozidi watatu (3) ili Rais ateue miongoni mwao, kinadhihirisha kuwa watu hao wanaaminika na taasisi hizo hivyo mmojawapo miongoni mwao akiteuliwa na Rais, kimsingi bado atakuwa ameteuliwa na taasisi yenye. Hivyo basi, Kamati inakubaliana na pendekezo la Serikali la Rais kubaki na mamlaka ya uteuzi wa Wajumbe 166 wa Bunge Maalum katika kifungu hiki. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilifanya tathmini ya kina kuhusu Muundo wa Bunge Maalum ambapo kulikuwa na maoni kwamba, dhana ya uwakilishi katika Bunge Maalum inapaswa kuzingatiwa kikamilifu na hivyo iko haja ya kuongeza makundi ya kijamii ambayo hayakuwa yametajwa katika kifungu cha 22 (1) (c) cha Sheria Mama na pia ilipendekezwa kuwa idadi ya Wajumbe hao iongezeke kutoka 166 kufikia idadi kati ya 201 – 400.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine kulikuwa na maoni kwamba, kwamba dhana ya kuongeza wigo wa uwakilishi isiwe pekee ndio msingi mkuu wa mapendekezo kuhusu Muundo wa Bunge Maalum kwani pamoja na mambo mengine, madhumuni ya Bunge hilo ni pamoja na kutunga Katiba ya nchi na hivyo utaalamu, uzoefu na busara za Wajumbe wanaouna Bunge hilo ni kitu cha kuzingatiwa zaidi kuliko kuangalia mawanda ya uwakilishi wa makundi ya kijamii peke yake. Kwa msingi huo, ilipendekezwa kuwa idadi ya Wajumbe ibaki kuwa 166 kama ambavyo Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya

Mabadiliko ya Katiba, Sura ya 83, Toleo la 2012 inatamka.  
(*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kufanya upembuzi yakinifu kuhusu suala hili, Kamati iliishauri Serikali kufanya marekebisho katika kifungu cha 22 (1) (c) cha Sheria Mama kwa kuongeza makundi mengine ya kijamii ambayo hayakuwa yametajwa awali ili kupanua wigo wa uwakilishi katika Bunge Maalum kwa sababu dhana ya uwakilishi wa kila kundi la kijamii katika Bunge Maalum, ni suala ambalo linapaswa kuzingatiwa kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa madhumuni ya kuweka uwiano, Kamati ilipendekeza kuwa idadi ya Wajumbe 166 wa Bunge Maalum ibaki kama ilivyo bali uteuzi wa Wajumbe hao uzingatie kikamilifu kutoka katika makundi mbalimbali ya kijamii ambayo yatakuwa yameainishwa katika Sheria. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanya marekebisho kama yanavyoonekana katika Jedwali la Marekebisho ambalo limeambatishwa pamoja na Muswada huu lakini Kamati haijaridhishwa na marekebisho hayo na inapendekeza kwa Jedwali la Kamati la Marekebisho (*Committee's Schedule of Amendment*), kwamba kifungu cha 22 (1) (c) cha Sheria Mama kifanyiwe marekebisho ambayo yatataja makundi ya kijamii kama ifuatavyo:-

- (i) Asasi za kitaifa za wataalam wa masuala mbalimbali zilizosajiliwa kisheria.
- (ii) Umoja katika ngazi ya Taifa wa asasi za kiraia zilizosajiliwa kisheria.
- (iii) Vyama vya siasa vyenye usajili wa kudumu.
- (iv) Wawakilishi kutoka taasisi za elimu ya juu.
- (v) Jumuiya za kitaifa za watu wenye ulemavu.
- (vi) Wawakilishi kutoka umoja katika ngazi ya taifa wa vyama vya wanafunzi kutoka taasisi za elimu ya juu.
- (vii) Asasi za kitaifa za kidini.
- (viii) Jumuiya za kitaifa za Vyama vya Wafanyakazi.
- (ix) Umoja wa kitaifa wa vyama kutoka sekta binafsi
- (x) Jumuiya za kitaifa za vyama vya waajiri vyenye usajili.
- (xi) Jumuiya za kitaifa za wakulima zenye usajili kisheria.
- (xii) Jumuiya za kitaifa za wafugaji zenye usajili kisheria.
- (xiii) Jumuiya za kitaifa za wavuvi zenye usajili kisheria.
- (xiv) Jumuiya za kitaifa za wanawake zenye usajili kisheria.
- (xv) Jumuiya za kitaifa za umoja wa vijana zenye usajili kisheria.
- (xvi) Vyama vya wastaifu vyenye usajili kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 4 ya Muswada, ambayo baada ya marekebisho inasomeka kuwa Ibara ya 8 kwa mujibu wa Jedwali la Marekebisho, inapendekeza kufanya kwa marekebisho katika kifungu cha 24 cha Sheria Mama ambacho kinaweka utaratibu wa kumpata Katibu, Naibu Katibu pamoja na Watumishi wa Bunge Maalum. Hapo awali, Sheria Mama ilimpa madaraka Katibu na Naibu Katibu wa Bunge Maalum kufanya uteuzi wa

Watumishi wa Bunge Maalum kutoka katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Baraza la Wawakilishi kwa idadi watakayoona inafaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo ya awali ya Muswada yalikuwa ni kwamba, marekebisho yafanyike katika Sheria Mama ili Katibu na Naibu Katibu wa Bunge wafanye uteuzi wa Watumishi wa Bunge Maalum na "taasisi husika" kwa idadi watakayoona inafaa kwa utekelezaji wa majukumu na mamlaka ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili, kulikuwa na mawazo tofauti ambapo wapo waliopendekeza kuwa maneno "Taasisi husika" kama yanavyosomeka katika Ibara hii ya Muswada yatolewe ufanuzi na taasisi hizo zitajwe bayana. Maelezo ya Serikali yalikuwa ni kwamba 'taasisi husika' ni zile taasisi za umma ambazo kwa namna moja au nyingine zina mchango katika uendeshaji wa Bunge Maalum kama ambavyo uzoefu unaonesha katika utendaji wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mabunge mengine duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo waliopendekeza kwamba, Bunge Maalum lihudumiwe na Watumishi kutoka Bunge la Jamhuri ya Muungano pamoja na Baraza la Wawakilishi peke yake kwa sababu watumishi hao ndio wenye utaalami na uzoefu wa masuala ya uendeshaji wa shughuli za Bunge. Aidha, watumishi hao wanaongozwa na Sheria ambazo zinawataka kutopokea maelekezo kutoka kwa mtu yejote nje ya Bunge wakati wa utekelezaji wa majukumu yao, kitu ambacho hakitakuwa halisi iwapo

watumishi kutoka nje ya taasisi hizo wataajiriwa kutekeleza majukumu ya Kibunge katika Bunge Maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine walipendekeza kuwa marekebisho yafanyike katika Muswada ili Katibu na Naibu Katibu wa Bunge wafanye uteuzi wa Watumishi wa Bunge Maalum lakini pia wapewe mamlaka ya kufanya uteuzi wa Watumishi wengine kutoka katika "taasisi husika" kwa masharti ya kuazimwa kulitumikia Bunge Maalum. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, awali, Serikali ilifanya marekebisho katika Ibara hii kwa Jedwali la Marekebisho na kuja na pendelekezo jipya kwamba, Katibu wa Bunge Maalum baada ya kushauriana na Naibu Katibu wa Bunge Maalum na Waziri, atateua idadi ya Watumishi kama atakavyoona inafaa kwa idadi ya "watumishi wa umma".

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilijadili pendelekezo hili na hatimaye ikaamua na kushauri kwamba, marekebisho yafanyike katika Muswada ili Katibu na Naibu Katibu wa Bunge wafanye uteuzi wa watumishi wa Bunge Maalum na kupewa mamlaka ya kufanya uteuzi wa watumishi wengine kutoka katika "watumishi wa umma" kwa masharti ya kuazimwa kulitumikia Bunge Maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendelekezo hili limefanyiwa kazi na Serikali kama ambavyo linaonekana katika Ibara mpya ya 8 katika Jedwali la Marekebisho lililoambatishwa na Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa vikao vya Kamati katika Mkutano huu wa Bunge hapa Dodoma, Serikali iliwasilisha mapendekezo mapya ya kuongeza Ibara mpya ya 4, katika Muswada ambayo inafanya marekebisho katika kifungu cha 22 cha Sheria Mama kwa kuongeza kifungu kipywa cha 22A.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu kinachopendekezwa cha 22A kinaweka masharti ya kwamba, Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katibu wa Baraza la Wawakilishi wataweka utaratibu wa namna ya kumpata "Mwenyekiti wa Muda" ambaye hatakuwa mgombea wa nafasi ya Mwenyekiti wa Bunge Maalum au Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum. Majukumu ya "Mwenyekiti wa Muda" yatakuwa kusimamia zoezi la kupitisha Kanuni za Bunge Maalum na kuendesha uchaguzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilitafakari mapendekezo haya na ikakubaliana nayo kwa madhumuni ya kurahisisha mchakato muhimu wa kupitisha Kanuni za Bunge Maalum lakini pia kusimamia zoezi zima la uchaguzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti kwa sababu masuala haya mawili yanahitaji mtu ambaye ana utaalam, weledi na uzoefu katika kusimamia shughuli za kibunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati inaona kuwa ni vyema masuala yote yanayohusu taratibu za chaguzi zote katika Bunge Maalum, yawekwe wazi na kufafanuliwa kikamilifu katika Kanuni za Bunge Maalum ambazo zitajadiliwa na kupitishwa na Wajumbe wa Bunge hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati inapendekeza kuwa, katika Kanuni hizo, viwekwe sifa na vigezo vya jumla kwa wagombea wa nafasi ya Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum, ambapo Wajumbe wenyewe sifa hizo watawasilisha maombi ya kugombea kwa Katibu wa Bunge Maalum ambaye kwa kushirikiana na "Mwenyekiti wa Muda" wataorodhesha majina ya wagombea wote waliokidhi matakwa ili kugombea.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchaguzi ukifanyika, mgombea atakayepata kura nyingi (asilimia hamsini (50%) au zaidi) ndiye awe mshindi katika kila nafasi inayoshindaniwa. Endapo mshindi asipopatikana katika hatua hiyo, aidha kwa mshindi kutofikisha asilimia hamsini za kura au kwa wagombea kufungana katika kura, duru ya pili ya uchaguzi itafanyika kwa wagombea waliopata kura nyingi au waliofungana ili kumpata mshindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imewasilsha mapendekezo mapya kwa kwa Ibara mpya ya 7 ili kufanya marekebisho katika kifungu cha 26 cha Sheria Mama. Kifungu hiki kinazungumzia masharti kuhusu Bunge Maalum. Kifungu kidogo cha 26(2) kinaweka sharti kwamba ili Katiba inayopendekezwa iweze kupitishwa katika Bunge Maalum, itahitaji kuungwa mkono kwa wingi wa theluthi mbili ya idadi ya Wajumbe wote wa Bunge hilo kutoka Tanzania Bara na theluthi mbili ya idadi ya Wajumbe wote wa Bunge hilo kutoka Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inapendekeza kuongezwa kwa vifungu vidogo vya (3), (4), (5) na (6) ambavyo vinaweka masharti ya marudio ya upigaji kura, endapo theluthi mbili ya idadi ya Wajumbe kutoka Tanzania Bara, au theluthi mbili ya idadi ya Wajumbe kutoka Tanzania Zanzibar au pande zote mbili kwa wakati mmoja haitafikiwa, kabla Katiba inayopendekezwa kama itakavyokuwa, kupelekwa kwa wananchi ili kwa kura ya maoni, waamue kuipitisha au kutoipitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika pendekozo hilo, kulikuwa na mjadala mrefu ulioibua mapendekezo tofauti lakini hatimaye Kamati iliamua kwa maoni ya walio wengi kukubaliaka na pendekozo hilo kwamba, pale ambapo theluthi mbili ya idadi ya jumla ya Wajumbe haijafikiwa kama invyotakiwa chini ya kifungu kidogo cha (2), Mwenyekiti wa Bunge Maalum, atabainisha suala au masuala yaliyoainishwa kwa madhumuni ya kupigiwa kura kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala au masuala yaliyoainishwa chini ya kifungu kidogo cha (3) yatapitishwa na Bunge Maalum kwa kuzingatia kuungwa mkono kwa theluthi mbili ya Wajumbe wote kutoka Tanzania Bara na theluthi mbili ya wajumbe wote kutoka Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale ambapo kuungwa mkono kwa theluthi mbili hakujafikiwa kama inavyotakiwa, katika kifungu kidogo cha (4), Bunge Maalum litapiga kura kwa mara ya tatu na suala au masuala yataamuliwa kwa

wingi wa idadi ya jumla ya Wajumbe kutoka Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupiga kura chini ya kifungu kidogo cha (5), Katiba inayopendekezwa itachukuliwa kuwa imepitishwa na Bunge la Katiba na masharti ya Sheria ya Kura ya Maoni yatatumika. Vilevile, utaratibu wa kupiga kura chini ya kifungu hiki utakuwa kama utakavyoelezwa katika Kanuni za Bunge Maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ibara ya 6 ya Muswada ambayo inasomeka kuwa Ibara mpya ya 9, Kamati inashauri kuwa, Mwenyekiti wa Bunge Maalum, baada ya kushauriana na Makamu Mwenyekiti, anaweza kwa ridhaa ya Rais baada ya kukubaliana na Rais wa Zanzibar, kuongeza muda uliotolewa chini ya kifungu kidogo cha (3) kwa idadi ya siku kwa kadri atakavyoona inafaa ili kuweka uhuru wa kuongeza muda kwa kadri uhitaji wa shughuli za Bunge Maalum utakavyojitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati, nampongeza Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mathias M. Chikawe (Mb) na Naibu wake Mheshimiwa Angellah J. Kairuki (Mb); Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ikiongozwa na Mheshimiwa Jaji Frederick Werema (Mb) pamoja na watumishi wa Wizara ya Katiba na Sheria chini ya uongozi wa Katibu Mkuu Ndg. Fanuel E. Mbonde kwa kuleta Bungeni Muswada huu ambao kwa kiasi kikubwa umefanya marekebisho ya msingi katika Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, Sura ya 83, Toleo la 2012. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho haya, pamoja na changamoto zake, yamekuja katika muda muafaka kwa kuzingatia kuwa mchakato wa kupata Katiba Mpya uko katika hatua muhimu kuelekea katika Bunge Maalum la Katiba, litakalojadili na kupitisha Rasimu ya Katiba ambayo itapigiwa Kura ya Maoni na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii vilevile, kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kuchambua kikamilifu maoni yaliyowasilishwa na wadau kuhusu Muswada huu na kuchambua Muswada wenyewe Ibara kwa Ibara pamoja na maudhui yake kikamilifu. Nawashukuru kwa ushirikiano wao na kwa maoni yao ambayo kwa sehemu kubwa yamefanikisha kuboresha Muswada huu pamoja na marekebisho yote yaliyofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima, naomba kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana, Mwenyekiti, Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mheshimiwa Abbas Zuberi Mtemvu, Mheshimiwa Nimrod Elirehema Mkono, Mheshimiwa Felix Francis Mkosamali, Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine, Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomari, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, Mheshimiwa Mustapha Boay Akunaay, Mheshimiwa Ramadhan Haji Saleh, Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mheshimiwa Tundu

Antiphas Mughway Lissu, Mheshimiwa Deogratias Aloyce Ntukamazina, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe, Mheshimiwa Abdallah Sharia Ameir na Mheshimiwa Halima James Mdee.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha napenda kuishukuru Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah, kwa kuratibu shughuli zote za Kamati hadi kuandaliwa kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Blandes, ahsante sana kwa kusoma maoni hayo kwa niaba ya Kamati. Niwaombe radhi Waheshimiwa Wabunge, baadhi yenu hamjapata hotuba hiyo mpaka sasa na ni kutokana na kwamba shughuli hii kwa ijamla wake, kazi ya Kamati ilikuwa ni kazi kubwa sana ambayo imefanywa na wenzetu upande wa Serikali. Kwa hiyo, mpaka mchana wa leo walikuwa bado wanaendelea kuweka sawa baadhi ya vifungu. Kwa hiyo, tuvumiliane baada ya muda si mrefu, tutapata nakala za kutosha kila mmoja wetu. Muhimu na cha kushika ni kwamba Kamaati *ime-move amendment* katika baadhi ya maeneo vilevile. (*Makof*)

Kabla sijamwita Msemaji wa Upinzani, niseme tu kwamba mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Pindi Chana na mchangiaji wa pili atakuwa Mheshimiwa David Silinde, kwa kuanzia.

Mheshimiwa Tundu Lissu sasa, Msemaji wa Upinzani.  
*(Makofi)*

**MHE. TUNDU A. M LISSU - MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI, WIZARA YA SHERIA NA KATIBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipate maji kama inawezekana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yafuatayo ni maoni ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Wizara ya Sheria na Katiba juu ya Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya Mwaka 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni Muswada wa Marekebisho ya Pili ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, Sura ya 83 ya Sheria za Tanzania. Kama Bunge lako Tukufu litakavyokumbuka, Sheria hii ilifanyiwa marekebisho ya kwanza kwa kupitishwa kwa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, Na. 2 ya mwaka 2012, mwezi Februari ya mwaka jana. Mabadiliko hayo ya kwanza yalihusu Sehemu ya Tatu na ya Nne ya Sheria hii na yalilenga vifungu mbalimbali vinavyohusu Tume ya Mabadiliko ya Katiba na utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada huu wa sasa unalenga kufanya marekebisho katika Sehemu ya Tano ya Sheria inayohusu 'Kuitisha Bunge Maalum.' Sambamba na mapendekezo haya, kuna mapendekezo ya kufanya marekebisho katika Sehemu ya Sita kwa kufuta vifungu vya 32 hadi 36 vya Sheria vinavyohusu utaratibu wa kura ya

maoni kwa ajili ya kuhalalisha ‘Katiba inayopendekezwa.’ Marekebisho haya yamewekwa katika aya ya 57 ya Muswada wa Sheria ya Kura ya Maoni, 2013. Mapendekezo ya Muswada huu ni muhimu lakini yana utata mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza majukumu yake ya kuuchambua Muswada huu, Kamati ya Bunge lako Tukufu ya Katiba, Sheria na Utawala ilikutana na wadau wengi mbalimbali. Hivyo, kwa mfano, Kamati ilipata maoni ya taasisi za kidini na za kiraia; taasisi za elimu ya juu na za kitaaluma; vyama vya siasa na asasi nyingine. Kwa sababu ambazo Kamati haikuelezwa vizuri na uongozi wa Bunge hili Tukufu, mapendekezo ya Kamati kwenda Zanzibar kwa lengo la kukusanya maoni ya wadau wa Zanzibar juu ya Muswada huu muhimu kwa mustakbala wa Jamhuri ya Muungano yalikataliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, ni muhimu Bunge lako Tukufu lifahamu ukweli huu kwamba wadau pekee walioshirikishwa kutoa maoni yao juu ya Muswada, ni Watanzania Bara peke yao. Wazanzibari hawakupatiwa fursa hiyo na hawakushirikishwa kabisa, licha ya Sheria yenyewe kuwa na mambo mengi yanayoihusu Zanzibar. Kwa vile wadau wa Zanzibar walishirikishwa kikamilifu kutoa maoni yao kuhusu Muswada uliopelekea Sheria hii kutungwa mwaka 2011, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua ni kwa nini uongozi wa Bunge na wa Serikali umeona si busara na sahihi kuwapatia Wazanzibari fursa ya kutoa maoni yao kuhusu Muswada huu wa kurekebisha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ambayo inawahu pia Wazanzibari na nchi yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Urais wa Kifalme kwa mara nyingine tena!!!! Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imepigia kelele jitihada za Serikali hii ya CCM kudhibiti mchakato wa Katiba Mpya kwa kuendeleza kile tulichokiita miaka miwili iliyopita, "... *kivuli kirefu cha Urais wa Kifalme katika mchakato wa upatikanaji wa Katiba Mpya.*" Hapo tulikuwa tunazungumzia mamlaka ya Rais ya uteuzi wa Wajumbe na watendaji wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba na tulisema kwamba mamlaka hayo yalikuwa na lengo moja tu: "*kuhakikisha kwamba matokeo ya kazi ya Tume hiyo ni yale tu yanayotakiwa na Rais na Serikali yake na chama chake cha CCM.*" (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maoni yetu wakati wa kutungwa kwa Sheria hii mwezi Novemba mwaka 2011, Kambi Rasmi ya Upinzani ilipinga vikali mapendekezo ya kumwezesha Rais kuteua Wajumbe wa Bunge Maalum wasiotokana na Bunge lako Tukufu na Baraza la Wawakilishi Zanzibar. Tulisema yafuatayo kuhusiana na jambo hili: "... *wajumbe ... wanaopendekezwa kuteuliwa kwenye Bunge la Katiba kwa mujibu wa Ibara ya 20(2)(e) na (4) ya Muswada Mpya sio, na hawawezi kuwa, wawakilishi wa wananchi. Kwanza, hawajachaguliwa na mtu yejote na wala taasisi zao kuwawakilisha katika Bunge la Katiba kwa sababu Muswada Mpya unapendekeza wateuliwe na Rais.*"

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya upinzani huo, mapendekezo ya kumfanya Rais kuwa mteuzi wa wajumbe wa Bunge Maalum wasiokuwa Wabunge na Wawakilishi

yaliondolewa katika Muswada huo wa Sheria hii. Badala yake, kifungu cha 22(1) (c) cha Sheria iliyotungwa na Bunge lako Tukufu kiliweka wazi kwamba "wajumbe mia moja sitini na sita [watasteuliwa] kutoka ..." taasisi zilizotajwa katika kifungu hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, Kifungu cha 22(1)(c) kama kilivytungwa, kilileta giza badala ya mwanga katika suala la uteuzi wa Wajumbe hao. Kama tulivyoieleza Timu ya Wataalamu wa Serikali kufuatia mukutano wetu na Rais Jakaya Kikwete, uliofanyika lkulu, tarehe 26 Novemba, 2011: "*Toleo la Kiswahili la Sheria linasema kwamba, wawakilishi wa makundi mengine watakaoteuliwa kutoka kwenye makundi yaliyoorodheshwa. Toleo la Kiingereza linasema Wajumbe hao watakuwa drawn from (kwa tafsiri ya Kiswahili watachukuliwa kutoka).* Maana za maneno haya hazifanani na wala hayako wazi kuhusu nani atakayewateua au kuwachukua Wajumbe hao kutoka kwenye taasisi zao." (Makofi)

Kwingineko, katika mukutano wetu na Rais Kikwete tulimweleza kwamba, Wajumbe 166 wengine wanaowakilisha taasisi nje ya Wabunge na Wawakilishi hawajachaguliwa na mtu yejote na wala na taasisi zao kwani Sheria haisemi ni nani atakayewateua na/au kuwachagua. Kwa sababu hiyo, tulipendekeza kwamba, Sheria iweke wazi kwamba Wajumbe hawa watateuliwa na taasisi zilizotajwa. Hii itaondoa utata juu ya uwakilishi wao na juu ya mamlaka yao ya uteuzi.

Mheshimwia Naibu Spika, mapendelekezo ya marekebisho yaliyoko kwenye Muswada huu, yanaonesha wazi kwamba, ushauri wetu kwa Rais Kikwete na kwa Timu yake ya Wataalamu umepuuzwa. Badala yake, Serikali hii sikivu ya CCM imeamua kuturudisha nyuma kwa zaidi ya miaka miwili kwa kuibua tena pendelekezo la kumfanya Rais kuwa mteuzi wa Wajumbe wa Bunge Maalum wasiotokana na Wabunge au Wawakilishi wa Zanzibar. Hii ni kwa sababu aya ya (3) ya Muswada inapendeleza kwamba, Wajumbe hao sasa wateuliwe na Rais. Hii ni sawa na kusema kwamba, kilichokuwa hakifai miaka miwili iliyopita sasa kinafaa na kilichokataliwa wakati ule sasa kinakubalika! (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuficha ukweli kwamba, mwenye mamlaka ya uteuzi wa Wajumbe wa Bunge Maalum wasiokuwa Wabunge au Wawakilishi ni Rais, ambaye pia ni Mwenyekiti wa CCM, Muswada unapendeleza kuongezwa kwa vifungu vidogo vipyta viwili katika Kifungu cha 22. Kwanza, inapendelekezwa kuwe na kifungu kidogo cha (2A) ambacho kitamruhusu Rais kualika kila kundi lilioainishwa katika kifungu kidogo cha 1(c), kuwasilisha kwake orodha ya majina ya watu wasiozidi watatu ili kuteuliwa kuwa Wajumbe. Pili, inapendelekezwa kuwe na kifungu kidogo cha (2B) kitakachomlazimu Rais kuzingatia sifa na uzoefu wa watu waliopendelekezwa na usawa wa jinsia wakati wa kufanya uteuzi wa Wajumbe hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mapendelekezo ya kumpa Rais mamlaka ya kuteua Wajumbe wa Bunge Maalum

hayakubaliki na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaliomba Bunge lako Tukufu lisiyapitishe kuwa Sheria. Kwanza, mapendekezo haya yanarudisha dhana kwamba, Wajumbe hao watakuwa watu wa Rais ambaye pia ni Mwenyekiti wa CCM. Rais Kikwete na Chama anachokiongoza ni wadau wakubwa wa mchakato wa Katiba Mpya na wana masilahi halisi na makubwa ya kuhakikisha kwamba, matakwa ya Chama chao ndiyo yanakuwa Katiba Mpya ya nchi yetu. (*Makofii*)

Ushahidi wa masilahi haya ya CCM ni kile kinachoitwa Ufafanuzi Kuhusu Rasimu ya Kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Wanachama na Viongozi wa CCM uliotolewa na Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM, tarehe 10 Juni, 2013. Katika Ufafanuzi huo, CCM imekataa mapendekezo yote muhimu yaliyoko kwenye Rasimu ya Katiba iliyotolewa na Tume. *Needless to say*, Rais Kikwete ni Mwenyekiti wa vikao vyote vya Kamati Kuu na Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM. Kumpa Rais na Mwenyekiti wa CCM Taifa, mamlaka ya kuteua Wajumbe wa Bunge Maalum litakalojadili na kuikubali au kuikataa Rasimu ya Katiba ambayo chama chake kimekwishaikataa ni sawa na kuipa CCM fursa nyingine ya kujaza Bunge hilo na makada wake kwa lengo la kutekeleza matakwa ya Chama hicho. (*Makofii*)

Pili, hata bila Wajumbe hawa kuteuliwa kwa namna inayopendekezwa, tayari CCM peke yake ina zaidi ya 72% ya Wajumbe wote wa Bunge Maalum wanaotokana na Wabunge na Wawakilishi. Kumpa Mwenyekiti wa CCM mamlaka ya kuteua Wajumbe wengine zaidi, kama

inavyopendekezwa katika Muswada huu, ni kutoa mwanya kwa CCM kutumia kivuli cha makundi ya kiraia, taasisi za kidini na makundi mengine ili kujiongezea Wajumbe wengine zaidi na hivyo kuhakikisha kwamba, Bunge Maalum litatekekeleza matakwa ya kuendeleza *status quo*.

Kwa maneno mengine, Serikali hii ya CCM na Wabunge wake, inataka Mwenyekiti wao wa Taifa ayachagulie makanisa na awachagulie Wakristo wawakilishi wao katika Bunge Maalum; awachagulie Waislamu wa BAKWATA, Baraza Kuu, JUMAZA na Taasisi nyingine za Kiislamu wawakilishi wao katika Bunge hilo; avichagulie Vyama vya Siasa vinavyoipinga CCM wawakilishi wao; awachagulie wafanyakazi, wakulima, wafugaji, wahadhiri, wanafunzi, wafanyabiashara, walemavu na makundi mengine ya kijamii wawakilishi wao katika Bunge Maalum! Kama ni hivyo, hilo halitakuwa Bunge Maalum la Watanzania, bali litakuwa Bunge Maalum la CCM na Mwenyekiti wao. Hili halikubaliki kwa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni na tunaamini halitakubalika kwa Wananchi wa Tanzania katika ujumla wao. (*Makofii*)

Tatu, kwa jinsi yalivyo kwa sasa, mapendelekezo haya hayawezi kutekeleza matakwa ya kifungu cha 22(1)(c) cha Sheria kinachotaka Wajumbe wa Bunge Maalum wasiotokana na Wabunge au Wawakilishi kuwa mia moja sitini na sita. Hii ni kwa sababu, hata kama watu wote waliopendekezwa na makundi yaliyoainishwa na kifungu hicho watateuliwa kuwa Wajumbe, bado idadi yao itakuwa Wajumbe ishirini na saba kwa kuwa makundi yenyewe yako tisa tu! Muswada uko kimya juu ya Wajumbe wengine mia

moja thelathini na tisa watatoka wapi na watateuliwa na nani na kwa utaratibu upi. (*Makofî*)

Kuna hoja kwamba, utaratibu wa uteuzi wa Wajumbe unaopendekezwa na Muswada unafanana na uteuzi wa Wajumbe wa Tume ulioko kwenye kifungu cha 6(6) cha Sheria, ambapo Rais alialika Vyama vya Siasa, Jumuiya za Kidini, Asasi za Kiraia na kadhalika, kuwasilisha orodha ya majina ya watu ili kuteuliwa kuwa Wajumbe wa Tume. Hoja hii siyo sahihi; kwanza, Tume ya Katiba siyo sawa na Bunge Maalum. Tume ni chombo cha kitaalamu chenye majukumu ya kitaalamu ya kukusanya maoni ya Wananchi, kuandaa Ripoti pamoja na Rasimu ya Katiba. Uhalali wa Tume unatokana na utaalamu wa Wajumbe wake na weledi wao katika kutekeleza majukumu yao ya kitaalamu. (*Makofî*)

Kwa upande mwingine, Bunge Maalum ni Chombo cha Uwakilishi ambacho Wajumbe wake wana majukumu ya kisiasa ya kuwakilisha Wananchi wa makundi mbalimbali kwenye kazi ya kisiasa ya kuandika Katiba Mpya. Uhalali wa Bunge Maalum unatokana na upana na ubora wa uwakilishi wake wa makundi mbalimbali ya kisiasa na kijamii. Chombo cha Uwakilishi cha aina hii lazima kitokane na wananchi na/au makundi ya kijamii kinachoyawakilisha ili kiwe na uhalali wa kisiasa. Dhana ya Rais na Mwenyekiti wa CCM kuteua Wajumbe wa Bunge Maalum, inavuruga au kuondoa kabisa dhana ya uwakilishi wa Wananchi na uhalali wa kisiasa katika mchakato wa Katiba Mpya.

Pili, kumpa Rais mamlaka ya kuteua Wajumbe wasiokuwa Wabunge au Wawakilishi wa Zanzibar kunaleta dhana ya ubaguzi. Hii ni kwa sababu, Rais hana mamlaka ya kuteua Wajumbe wa Bunge Maalum watakaotoka kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano na Baraza la Wawakilishi Zanzibar. Hawa wataingia katika Bunge Maalum kwa mujibu wa nafasi zao Bungeni au katika Baraza na siyo kwa fadhila za Rais. Swali la kujiuliza hapa ni kwa nini Rais awe na mamlaka ya kuteua Wajumbe wasiokuwa Wabunge au Wawakilishi wakati hana mamlaka hayo kuhusu Wabunge na Wawakilishi? *Needless to say*, ubaguzi huu unaenda kinyume na matakwa ya Ibara ya 13(2) ya Katiba ya sasa na kwa hiyo, haukulbaliki.

Tatu, uteuzi wa Wajumbe wa Tume uliofanywa na Rais na ambao unatumia kama mfano wenyewe ulikuwa na walakini mkubwa. Katika hili, kuna ushahidi wa Wawakilishi wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (*TEC*), Baraza la Kikristo Tanzania (*CCT*) na asasi mbalimbali za kiraia zikiwemo za walemavu, waliowasilisha maoni ya taasisi zao kwa Kamati juu ya Muswada huu. Wawakilishi hao waliiambia Kamati kwamba, ijapokuwa waliandikiwa na Rais kuwasilisha majina ya Wajumbe wao kwa ajili ya kuteuliwa kwenye Tume na walifanya hivyo, hakuna hata moja ya majina waliyopendekeza aliyeteuliwa na Rais kuwa Wajumbe wa Tume. (*Makofi*)

Badala yake, Rais aliteua watu aliowaona yeye na washauri wake wanafaa. Kama taarifa za wadau hawa ni za kweli, maana yake ni kwamba, Rais na Mwenyekiti huyu wa CCM Taifa, hawezi kuaminika tena kuteua Wajumbe

halisi wa Taasisi hizi katika Bunge Maalum ambalo ndilo litakalojadili na kuipitisha au kuikataa Rasimu ya Katiba Mpya ambayo tayari CCM na wapambe wao wametamka wazi kwamba, wanaikataa! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika Naibu, ili kutatua mkanganyiko huu, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza Bunge lako Tukufu lirejee na kukubali mapendekezo yetu kwa Timu ya Wataalamu wa Serikali ya Januari mwaka jana:

- (i) "*Sheria iweke wazi kwamba Wajumbe hawa watateuliwa na taasisi zilizotajwa. Hii itaondoa utata juu ya uwakilishi wao na juu ya mamlaka yao ya uteuzi;*
- (ii) "*Sheria itaje kwamba idadi ya Wajumbe wa Bunge Maalum watakaotokana na kila taasisi iliyoorodheshwa katika kifungu cha 22(1)(c) itakuwa 354 kama walivyoorodheshwa hapa chini:*
  - (a) "*Asasi zisizokuwa za kiserikali zilizotajwa katika aya ya (i) zifafanuliwe kuwa ni makundi yanayounganisha asasi hizo, yaani ANGOZA ya Zanzibar, TANGO, TACOSODE na Jukwaa la Katiba na kila moja ya makundi hayo itakuwa na Wajumbe watano kwa jumla ya Wajumbe 20;*
  - (b) "*Asasi za kidini zilizotajwa katika aya ya (ii) zifafanuliwe kuwa ni makundi yanayounganisha asasi hizo, yaani BAKWATA, Baraza Kuu, JUMAZA, TEC, CCT na PCT na kila moja ya makundi hayo*

itakuwa na Wajumbe watano kwa jumla ya Wajumbe 30. Aidha, Waadventista wa Sabato (SDA), Hindu, Shia Ithnaasheri na Sikh watakuwa na Mjumbe mmoja mmoja, kwa jumla ya wawakilishi 35 wa taasisi za kidini;

- (c) "Vyama vyta siasa vyenye usajili wa kudumu vilivytajwa katika aya ya (iii) vitakuwa na Wajumbe 72 watakaogawanywa katika makundi mawili: (1) vyama vyote vyta siasa vyenye usajili wa kudumu vitakuwa na Wajumbe 42 ikiwa ni Wajumbe wawili kwa kila chama; (2) vyama vyta siasa vyenye uwakilishi Bungeni vitakuwa na Wajumbe 30 ikiwa ni CCM 18, CHADEMA 7, CUF 3 na NCCR-Mageuzi, TLP na UDP 3 kwa ujumla wao. Hii ni kufuatana na uwiano wa kura zote za Wabunge ambazo vyama hivyo vilizipata kwenye Uchaguzi Mkuu wa 2010;
  
- (d) "Taasisi za Elimu ya Juu zilizotajwa katika aya ya (iv) zifafanuliwe kuwa ni Vyuo Vikuu 28 vinavyotambuliwa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) na Vyuo vyta Elimu ya Juu 16 vinavyotambuliwa na Baraza la Elimu ya Ufundis la Taifa (NACTE). Taasisi hizi zitakuwa na Mjumbe mmoja kwa kila moja kwa jumla ya Wajumbe 44;
- (e) "Taasisi za elimu ya juu zinahusisha pia vyama vyta wanafunzi wa vyuo vyta elimu ya juu ambavyo vitakuwa na Mjumbe mmoja mmoja kwa kila chama cha wanafunzi kwa jumla ya Wajumbe 44;

- (f) *Taasisi za Elimu ya Juu zinahusisha pia vyama wahadhiri au wakufunzi wa vyuo vya elimu ya juu ambavyo vitakuwa na Mjumbe mmoja mmoja kwa kila chama kwa jumla ya Wajumbe 44;*
- (g) *"Makundi yenyе mahitaji maalum yaliyotajwa katika aya ya (v) yafafanuliwe kuwa ni mashirika yanayowakilisha wenyе ulemavu wa macho, ngozi, viziwi/bubu, viwete na walemvu wa aina nyingine ambayo yatakuwa na Wajumbe 10 kwa ujumla wao;*
- (h) *"Vyama vya wafanyakazi vilivyotajwa katika aya ya (vi) vifafanuliwe kuwa ni vile vilivyo sаjiliwa na vitakuwa na Wajumbe 40 ikiwa ni Wajumbe wawili kutoka kila chama cha wafanyakazi kilichosajiliwa;*
- (i) *"Jumuiya ya wakulima iliyotajwa katika aya ya (vii) itakuwa na Wajumbe 10 watakaotokana na vyama vya wakulima wa mazao kama vile pamba, kahawa, korosho, chai, katani, karafuu, miwa na wavuvi;*
- (j) *"Jumuiya ya wafugaji iliyotajwa katika aya ya (viii) itakuwa na Wajumbe 10 watakaotoka Baraza la Mashirika yasiyo ya Kiserikali ya Wafugaji na Wawindaji au wakusanya matunda ya porini (PINGOS Forum);*

(k) "Vikundi vingine vya watu wenye malengo yanayofanana vilivyotajwa katika aya ya (ix) vifafanuliwe kumaanisha Chama cha Waajiri Tanzania (ATE), Chama cha Wenye Viwanda Tanzania (CTI), Chama cha Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA), Chama cha Wafanyabiashara Wanawake Tanzania (TWCC); Chama cha Wafanyabiashara wa Madini na Nishati (TCME); vyama au mashirika ya wachimbaji madini wadogo wadogo; Chama cha Wamiliki wa Vyombo vya Habari (MOWAT), Chama cha Waandishi Habari au Jukwaa la Wahariri Tanzania, Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS), Chama cha Mawakili Zanzibar (ZLS), Chama cha Madaktari Tanzania (MAT), Taasisi ya Wahandisi Tanzania (IET) na Chama cha Wakandarasi Tanzania (CATA). Makundi haya yatakuwa na Wajumbe wawili kwa kila moja kwa jumla ya Wajumbe 26."

Mheshimiwa Spika Naibu, kwa mujibu wa Kifungu cha 22(1) cha Sheria kama ilivyo sasa, Bunge Maalum litakuwa na jumla ya Wajumbe 604, yaani Wabunge 357, Wawakilishi 76 na Wajumbe 166 wanaowakilisha makundi mbalimbali. Mapendekezo haya ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni yatafanya uwakilishi katika Bunge Maalum kupanuka hadi Wajumbe 792 kwa Tanzania yenye idadi ya watu milioni 45 kwa takwimu za sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012. (Makofi)

Hili, kwa vyovoyote vile ni ongezeko kubwa la Wajumbe wa Bunge Maalum. Hata hivyo, ukubwa huu unaopendekezwa hauna tofauti kubwa sana na Mabunge Maalum ya nchi nyingine ambazo zimekamilisha utungaji wa Katiba Mpya kwa kutumia utaratibu huu. Kwa mfano, Bunge Maalum la Jamhuri ya Nepal la mwaka 2011 lilikuwa na Wajumbe 601 kwa nchi yenye idadi ya watu milioni 26; Bolivia (2009) lilikuwa na Wajumbe 255 katika nchi yenye watu milioni 9; Kenya (2005) lilikuwa na Wajumbe 627 kwa idadi ya watu milioni 31; Eritrea (1997) lilikuwa na Wajumbe 527 kwa idadi ya watu milioni 3.2, wakati Bunge Maalum la Ufaransa ya Mapinduzi ya 1789 lilikuwa na Wajumbe 1145 katika nchi iliyokuwa na idadi ya watu milioni 28. (*Makof*)

Kikubwa na muhimu zaidi kwa mapendekezo haya ni kwamba, Bunge Maalum la Katiba litakuwa na sura ya Kitanzania zaidi badala ya utaratibu wa sasa unaolifanya Bunge Maalum kuonekana la ki-CCM zaidi. Kwa kuongeza tu, wadau karibu wote waliota maoni yao kwenye Kamati, walipendekeza kuongezwa kwa idadi ya Wajumbe wa Bunge Maalum kwa kigezo chochote kile. Kwa hiyo, mapendekezo haya ni ya kidemokrasia na tunaliomba Bunge lako Tukufu liyaunge mkono ili kuiwezesha nchi yetu kujipatia Katiba Mpya, yenye sura halisi ya kitaifa kuliko inavyopendekezwa sasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Mabadiliko ya Katiba imekwishatoa Rasimu ya Katiba kwa mujibu wa kifungu cha 19(1)(d) cha Sheria. Rasimu hiyo imependekeza mabadiliko makubwa katika muundo wa Jamhuri ya Muungano kwa kupendekeza muundo wa shirikisho lenye

Serikali tatu. Baada ya kukamilika kwa mchakato wa kutoa maoni juu ya Rasimu hii kwa mujibu wa kifungu cha 18, Tume itawasilisha Ripoti kwa Rais na kwa Rais wa Zanzibar kwa mujibu wa Kifungu cha 20(1). Baada ya hapo, Rais, atachapisha Rasimu ya Katiba katika Gazeti la Serikali na kwenye magazeti mengine pamoja na maelezo kwamba, Rasimu ya Katiba itawasilishwa kwenye Bunge Maalum kwa ajili ya kupitishwa Katiba inayopendekezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutimiza matakwa haya ya Sheria na kwa kuzingatia mapendelekezo ya Rasimu ya Katiba iliyotolewa na Tume, Bunge lako Tukufu linahitaji kuangalia upya suala la uwakilishi wa Zanzibar katika Bunge Maalum. Kwa mujibu wa Kifungu cha 22(2) cha Sheria, idadi ya Wajumbe wa Zanzibar katika Bunge Maalum watakaotokana na makundi yaliyoainishwa katika Kifungu cha 22(1)(c), haitapungua theluthi moja ya Wajumbe hao. Hii ina maana kwamba, kwa uchache kabisa, Wajumbe hao wa Zanzibar hawatapungua 55.

Rasimu ya Katiba itakayojadiliwa na Bunge Maalum inahusu Katiba ya Jamhuri ya Muungano peke yake. Rasimu hiyo imependelekeza kwamba, masuala yote yasiyo ya Muungano ya Washirika wa Muungano, yaani ya Tanzania Bara na Zanzibar, yashughulikiwe na Katiba za Washirika hao.

Kwa sasa Wabunge wanaotoka Zanzibar katika Bunge la Jamhuri ya Muungano ni 83, wakati Baraza la Wawakilishi Zanzibar lina Wajumbe 76. Kwa ujumla, ili kutekeleza matakwa ya Kifungu cha 22(1) na (2) cha Sheria, Zanzibar

itakuwa na Wajumbe 214 katika Bunge Maalum lenye Wajumbe 604, sawa na takribani 36% ya Wajumbe wote. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua kama ilikuwa busara na sahihi kwa nusu ya Wajumbe wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba kutoka Zanzibar; kwa nini isiwe busara na sahihi vilevile kwa nusu ya Wajumbe wa Bunge Maalum litakaloijadili na kuipitisha Katiba Mpya hiyo kutoka Zanzibar au ndiyo kusema kwamba hoja za usawa kati ya nchi Washirika wa Muungano huu ni kelele za majukwaani tu? (Makof)

Mheshimiwa Spika, Profesa Palamagamba J.A.M. Kabudi wa Shule ya Sheria ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Mjumbe wa Tume, aliwahi kusema kwenye Semina ya Wabunge Juu ya Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Katiba iliyofanyika hapa Dodoma tarehe 12 Novemba, 2011 kwamba: "*Katika kuandika Katiba mpya, wabia wa Muungano wanarudi kwa usawa.*" Kwa sababu hiyo na kwa kuzingatia mapendelekezo ya hadhi na haki sawa baina ya Washirika wa Muungano yaliyoko katika Rasimu ya Katiba, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kwamba, idadi ya wawakilishi wa Zanzibar katika Bunge Maalum iongezwe hadi kufikia nusu ya Wajumbe wote wa Bunge Maalum. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili linawezekana kwa namna mbili. Kwanza, kwa kuongeza idadi ya Wajumbe walotajwa katika Kifungu cha 22(1)(c) hadi 354 kama tulivyopendekeza katika Maoni haya. Pili, kwa kurekebisha Kifungu cha 22(2) ili kisomeke kwamba, idadi ya Wajumbe kutoka Zanzibar haitapungua asilimia hamsini na tano ya

Wajumbe hao. Kama pendelezo hili litakubaliwa na Bunge lako Tukufu, Wajumbe wa Bunge Maalum kutoka Zanzibar wataongezeka kutoka 214 kwa mujibu wa Sheria ilivyo sasa hadi 323. Muhimu zaidi, Bunge Maalum litakuwa limetimiza matakwa ya usawa wa Washirika wa Muungano kwa kuwa na idadi sawa ya Wajumbe katika Bunge hilo. Hili litaondoa manung'uniko yanayoweza kujitokeza baadaye kwamba, Wazanzibari hawakutendewa haki sawa katika Bunge la Katiba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Watumishi wa Bunge Maalum: Muswada unapendekeza marekebisho mengine katika Sheria ya Mabadiliko ya Katiba. Hivyo basi, aya ya 4 inapendekeza marekebisho ya kifungu cha 24(4) kama ifuatavyo: "*Katibu wa Bunge Maalum baada ya kushauriana na Naibu wake na taasisi husika, atateua kutoka katika Bunge, Baraza la Wawakilishi na taasisi husika idadi ya watumishi kama itakavyoonekana inafaa kwa utekelezaji wa majukumu na mamlaka ya Bunge Maalum.*" Kama ilivyo hivi sasa, kifungu hicho kinasomeka kama ifuatavyo: "*Katibu wa Bunge Maalum baada ya kushauriana na Naibu Katibu wa Bunge Maalum, watateua watumishi kutoka kwenye Bunge na Baraza la Wawakilishi kwa idadi watakayoona inafaa kwa ajili ya kutekeleza kwa ufanisi majukumu ya Bunge Maalum.*"

Mheshimiwa Naibu Spika, kama inavyoonekana wazi, mabadiliko pekee yanayopendekezwa na Muswada ni maneno 'taasisi husika'. Maneno haya hayajatafsiriwa mahali popote katika Sheria na Muswada uko kimya juu ya maana yake. Hata Maelezo ya Mheshimiwa Waziri wa

Katiba na Sheria mbele ya Kamati, yako kimya juu ya maneno hayo.

Ukimya huu una mwangwi mkubwa. Kama pendelezo hili litakubaliwa, kutakuwa na uwezekano wa Watumishi wa Bunge Maalum la Katiba kuteuliwa kutoka katika Taasisi na Idara mbalimbali za Serikali au hata Taasisi zisizokuwa za Kiserikali. Kwa sababu Bunge Maalum litatekeleza majukumu yake kwa muda maalum unaopendekezwa katika aya ya 6 ya Muswada huu, ni wazi watumishi hao watatumikia Bunge Maalum *on secondment* kutoka kwenye taasisi zao za mwanzo. Kwa maana hiyo, watumishi hao watawajibika kwa taasisi zao na wanaweza kutumiwa na taasisi zao kutoa taarifa au siri muhimu juu ya shughuli za Bunge Maalum kwa taasisi zao.

Kwa upande mwingine, Watumishi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, wamepewa kinga ya Kikatiba inayowakataza kupokea maelekezo kutoka taasisi nyingine nje ya Bunge. Kama kifungu cha 4(3) cha Sheria ya Uendeshaji Bunge, Na. 14 ya 2008, inavyoweka wazi, katika utekelezaji wa majukumu yao, Watumishi wa Bunge hawatapokea maelekezo kutoka mahali popote nje ya Utumishi (wa Bunge). Katika mazingira haya, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kwamba, mapendekezo ya kurekebisha kifungu cha 24(4) hayakidhi matakwa ya uhuru wa Bunge Maalum na kwa sababu hiyo, yasikubaliwe na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja kubwa zaidi juu ya pendelezo hili. Hoja hii inahusu mamlaka ya Katibu wa

Bunge Maalum na Naibu wake, kuteua watumishi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano na Baraza la Mapinduzi Zanzibar kuwa Watumishi wa Bunge Maalum chini ya kifungu cha 24(4) cha Sheria na pendeleko la Muswada la kukifanyia marekebisho.

Kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Bunge, Katibu wa Bunge hana mamlaka ya kuteua Watumishi wa Bunge peke yake. Hayo, kwa mujibu wa Sheria hiyo, ni mamlaka ya pamoja kati ya Katibu na Tume ya Utumishi wa Bunge na utekelezaji wake unahitaji mashauriano kati ya vyombo hivyo viwili. Kwa sababu hiyo na kwa kuzingatia utaratibu wa Sheria hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza Watumishi wa Bunge Maalum wateuliwe kutoka miongoni mwa Watumishi wa Bunge na Baraza la Wawakilishi baada ya mashauriano kati ya Katibu wa Bunge Maalum na Naibu wake pamoja na Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum. Pendeleko hili lina faida kwamba, Watumishi wa Bunge Maalum watakuwa wameteuliwa na watawajibika kwa Bunge Maalum na siyo kwa taasisi nyingine nje ya Bunge Maalum. Kwa maana hiyo, pendeleko la Muswada juu ya uteuzi wa Watumishi wa Bunge Maalum nje ya Bunge la Jamhuri ya Muungano na Baraza la Wawakilishi Zanzibar halina umuhimu na linapaswa kukataliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada unapendekeza marekebisho ya Kifungu cha 3 cha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba inayohusu tafsiri ya maneno mbalimbali. Mapendekezo ya Muswada yanahu tafsiri ya maneno 'Rasimu ya Katiba' na 'Kanuni.' Pendeleko la kutafsiri neno

'Kanuni' halina utatanishi wowote na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaliunga mkono. Kwa upande mwingine, Kambi Rasmi Upinzani Bungeni inapinga tafsiri inayopendekezwa ya maneno 'Rasimu ya Katiba.' Kwa mujibu wa aya ya 2 ya Muswada, maneno 'Rasimu ya Katiba' yatakuwa na maana ya Rasimu ya Katiba ambayo imetayarishwa na Tume kutokana na maoni na mapendekezo ya Wananchi chini ya Sheria.

Pendekezo hili linapingana na maudhui ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba. Kwanza, pamoja na kwamba, maoni ya Wananchi ni chanzo muhimu cha Ripoti ya Tume na Rasimu ya Katiba, maoni hayo siyo chanzo pekee cha Ripoti ya Tume na Rasimu ya Katiba. Kwa mujibu wa kifungu cha 17(4) cha Sheria, Tume inatakiwa kupitia na kuchambua michango, mawazo, maoni, taarifa na mapendekezo yaliyokusanywa na kufanyiwa tathmini siku za nyuma. Kifungu hicho kimeorodhesha nyaraka nyingi muhimu na za kihistoria ambazo zimejenga taswira ya Kikatiba ya nchi yetu tangu Uhuru wa Tanganyika mwaka 1961. Tume inawajibika kuzipitia na kuzichambua nyaraka zote hizo katika kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria hii.

Pili, Tume pia inawajibika kutumia tafiti za kiuchambuzi na kitaalam zitakazofanywa na Tume na nyaraka nyingine zozote ambazo Tume itaona ni muhimu. Vyanzo vyote hivi vinatakiwa kutumika katika matayarisho ya Rasimu ya Katiba. Kwa maana hiyo, madhara ya mapendekezo ya Muswada juu ya tafsiri ya maneno 'Rasimu ya Katiba' ni ya wazi na mabaya. Kama yatakubaliwa na kuwa Sheria,

vyanzo vyote hivi vya Ripoti ya Tume na Rasimu ya Katiba vitakuwa *redundant*. Aidha, mapendekezo ya Tume na Rasimu ya Katiba yanayotokana na vyanzo hivyo yatakuwa kinyume cha Sheria na yatabidi yaondolewe kwenye Ripoti na Rasimu ya Katiba. Kwa sababu hizi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kwamba, maneno 'Rasimu ya Katiba' yatafsiriwe kumaanisha Rasimu ya Katiba ambayo imetayarishwa na Tume kwa mujibu wa Sheria hii. Tafsiri hii inayopendekezwa inajumuisha maoni ya Wananchi pamoja na vyanzo vingine vyote vya Ripoti ya Tume na Rasimu ya Katiba vilivyoainishwa kwenye Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada unapendekeza marekebisho katika kifungu cha 31 cha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba kinachohusu uendeshaji wa kura ya maoni. Inapendekezwa kwamba, kifungu hicho kifutwe na badala yake kiwekwe kifungu kipyga kitakachosema kwamba, masharti yote yanayohusu uendeshaji wa kura ya maoni utawekwa na Sheria ya Kura ya Maoni. Kwa vile tayari kuna Muswada wa Sheria ya Kura ya Maoni, 2013, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inakubaliana na pendekezo hili. Hata hivyo, kifungu cha 31 siyo kifungu pekee katika Sheria hii chenye masharti ya uendeshaji wa kura ya maoni. Kuna vifungu vingine vinavyotaja au kuweka utaratibu wa kura ya maoni. Ukweli ni kwamba, Sehemu ya Sita yote inayohusu uhalalishaji wa Katiba inayopendekezwa inahusika na masuala mbalimbali ya kura ya maoni. Vilevile, kifungu cha 4(1)(n) na (2) navyo pia vinataja kura ya maoni. Kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, vifungu hivi pamoja na Sehemu ya Sita yote, vinahitaji kurekebishwa kwa kufutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada unapendekeza kufanya marekebisho katika Kifungu cha 27(2) cha Sheria kinachohifadhi uhuru wa mawazo, majadiliano na utaratibu katika Bunge Maalum, kwa kuweka kinga ya mashtaka dhidi ya Wajumbe wa Bunge Maalum. Zaidi ya hayo, Muswada unapendekeza muda usiozidi siku sabini kwa Bunge Maalum kujadili Rasimu ya Katiba. Muda huo unaweza kuongezwa kwa siku nyingine zisizozidi ishirini kwa ridhaa ya Rais, baada ya kukubaliana na Rais wa Zanzibar. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inakubaliana na mapendekezo yote haya ya Muswada kwa *caveat kwamba*, pendektezo la muda wa nyongeza lisiwekewe muda mahususi. Hii ni kwa lengo la kuwezesha muda kuongezwa kulingana na hali halisi ya majadiliano ndani ya Bunge Maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliwasilisha Jedwali la Marekebisho ya Muswada huu mbele ya Kamati, ikipendekeza marekebisho kadhaa katika Muswada na katika Sheria mama. Mapendekezo haya ni ya aina mbili. Kwanza, ni mapendekezo ya marekebisho ya Muswada uliosomwa mbele ya Bunge lako Tukufu katika Bunge la Kumi na Moja na ambayo yalijadiliwa na Kamati na wadau mbalimbali. Haya ni marekebisho yanayopendekezwa katika sehemu A, B na D ya Jedwali la Marekebisho ya Serikali. Marekebisho haya yanaenda sambamba na matakwa ya Kanuni ya 84(3) na (4) ya Kanuni za Kudumu na kwa hiyo yanakubalika kikanuni.

Kwa upande mwingine, marekebisho yanayopendekezwa katika sehemu C na E za Jedwali la Marekebisho ya Serikali ni mambo mapya, ambayo hayakuwepo kwenye Muswada uliosomwa kwa Mara ya Kwanza katika Bunge liliopita. Marekebisho haya hayakujadiliwa na wadau wa nje ya Bunge na hayajulikani kwa Wabunge wasiokuwa Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Kwa sababu hiyo, marekebisho haya yanakiuka masharti ya Kanuni ya 86(7) ya Kanuni za Kudumu inayoelekeza kwamba, mjadala wakati wa Muswada wa Sheria Kusomwa Mara ya Pili utahusu ubora na misingi ya Muswada huo tu. Ili kulinda heshima ya Bunge lako Tukufu, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inakuomba, Mheshimiwa Naibu Spika, utekeleze wajibu wako chini ya Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Kudumu kwa kufutilia mbali sehemu C na E za Jedwali la Marekebisho ya Serikali kwa sababu zinakiuka matakwa ya kanuni tajwa ya Bunge lako Tukufu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu C ya Jedwali la Marekebisho ya Serikali, tunaokuomba uifutilie mbali, inapendekeza kuongezwa kwa kifungu kipyga cha 22A katika Sheria. Katika pendekezo la awali kuhusu kifungu hicho, ilikuwa inapendekezwa kumfanya Spika wa Bunge hili Tukufu kuwa Mwenyekiti wa Muda wa Bunge Maalum kwa ajili ya kutengeneza Kanuni za Kudumu za Bunge Maalum na kwa ajili ya uchaguzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum.

Baada ya Kamati kuhoji na kuelezwu kwamba, Spika au Mwenyekiti wa Muda atakuwa pia na haki ya

kugombea kuwa Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum na hivyo kutengeneza mgongano wa wazi wa masilahi, Kamati ilielekeza kwamba, Katibu na Naibu Katibu wa Bunge Maalum watasimamia uchaguzi wa Mwenyekiti wa Muda ambaye hatakuwa na haki ya kugombea nafasi ya Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum. Hata hivyo, hoja ya msingi kwamba hili ni pendelekezo jipya ambalo halikuwepo kwenye Muswada uliosomwa Mara ya Kwanza inabaki pale pale.

Kuhusu sehemu E ya Jedwali la Marekebisho ya Serikali, sehemu hiyo inapendekeza kufifiisha matakwa ya kifungu cha 26(2) cha Sheria inayoweka masharti ya kupitisha Katiba inayopendekezwa kwa theluthi mbili ya Wajumbe wote wa Bunge Maalum wanaotoka Tanzania Bara na idadi hiyo hiyo ya Wajumbe wanaotoka Zanzibar. Pendelekezo jipya ni kupunguza idadi ya uungwaji mkono hadi wingi wa kawaida (*simple majority*) ya Wajumbe wote wanaotoka Tanzania Bara na idadi hiyo hiyo ya Wajumbe wanaotoka Zanzibar endapo Bunge Maalum litashindwa kupitisha Katiba inayopendekezwa kwa theluthi mbili baada ya kupiga kura mara mbili. Pendelekezo hili nalo linakiuka matakwa ya Kanuni ya 86(7) na linapaswa kuondolewa katika mjadala wa Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo mengine ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ambayo, kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, yanahitaji kufanyiwa marekebisho ili kuwezesha utekelezaji bora wa Sheria hii. Eneo mojawapo ni masharti ya Kifungu cha 28(2) yanayoruhusu Bunge Maalum kuitishwa tena baada ya

kukamilisha majukumu yake kwa mujibu wa Sheria na kuvunjwa chini ya Kifungu cha 28(1) cha Sheria hii.

Kifungu cha 28(1) kinasema: “*Baada ya kutunga Katiba inayopendekezwa, masharti yatokanayo na masharti ya mpito, Bunge Maalum litavunjwa na mamlaka ya kutunga masharti ya Katiba inayopendekezwa, masharti yatokanayo na masharti ya mpito yatakoma.*” Kwa upande mwingine, Kifungu cha 28(2) kinatengua masharti ya Kifungu cha 28(1) kwa maneno yafuatayo: “Kuvunjwa na kukoma kwa mamlaka ya Bunge Maalum hakutachukuliwa kuwa kunaondoa mamlaka ya Rais kuliitisha tena Bunge hilo kwa lengo la kuboresha masharti yaliyomo kwenye Katiba inayopendekezwa.”

Mheshimiwa Naibu Spika, misingi mikuu ya tafsiri za kisheria inaelekeza kwamba, chombo chenye mamlaka au majukumu ya kisheria ya kufanya jambo fulani kikishakamilisha kutekeleza mamlaka au majukumu yake hayo, kinakuwa *functus officio* katika jambo hilo, yaani kinakuwa hakina mamlaka tena kisheria juu ya jambo hilo. Huu ndiyo msingi wa Kifungu cha 28(1) cha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba. Athari ya Kifungu cha 28(2) ni kulifufua kutoka katika wafu, Bunge Maalum, ambalo kwa mujibu wa Kifungu cha 28(1), linakuwa limekuwa *functus officio* baada ya kuitisha Katiba Mpya na masharti ya mpito. Hii inafanywa na Rais, ambaye na Chama cha siasa anachokiongoza ni mdau mkubwa wa mchakato wa Katiba Mpya.

Katika Maoni yetu wakati wa mjadala wa kupidishwa kwa Sheria hii mwezi Novemba, 2011, tulisema yafuatayo juu ya kifungu hiki: "Maana halisi ya maneno haya ni kwamba, Rais atakuwa na mamlaka ya kuliita tena Bunge la Katiba ili lifanye marekebisho ya mambo ambayo yeye au Serikali yake au Chama chake hawayapendi katika Katiba Mpya kabla haijapigiwa Kura ya Maoni na Wananchi! Kama Chombo huru cha Wananchi, Rais hawesi kujipa madaraka ya kupingana na kauli ya Wananchi kupitia Bunge la Katiba."

Katika mapendekezo yake kwa timu ya Wataalam wa Serikali iliyoundwa kufuatia mkutano wa tarehe 26 Novemba, 2011 kati ya CHADEMA na Rais Jakaya Kikwete, CHADEMA ilipendekeza kwamba, Kifungu cha 28(2) kifutwe kabisa. Huu ni wakati mwafaka kukiangalia upya kifungu hiki ambacho kinaweza kuleta mgogoro usiokuwa na sababu endapo Rais ataamua kuliitisha tena Bunge Maalum kwa sababu Serikali au Chama chake hakikubaliani na Katiba Mpya iliyopitishwa na Bunge Maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mchakato wa Katiba ya Tanganyika na Zanzibar: Tarehe 3 Juni, 2013 Tume ilichapisha Rasimu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 2013. Kwa kufanya hivyo na kwa mujibu wa Kifungu cha 18(5) cha Sheria, Tume imekamilisha jukumu lake la kwanza baada ya kukamilisha zoezi la kukusanya maoni ya Watanzania juu ya Katiba Mpya.

Rasimu hii inapendekeza mambo mengi na muhimu kwa mustakabali mzima wa nchi yetu na tayari imezua mjadala mkali wa kitaifa. Mwanazuoni mmoja maarufu nchini ameyaita mapendekezo ya Rasimu ‘Mapinduzi ya Kimya Kimya’; wakati mwingine amehoji kuwa Rasimu hii ni Mwarobaini au Sanduku la Pandora? Aidha, Profesa Issa G. Shivji, ambaye pengine ni msomi maarufu wa masuala ya kikatiba katika sehemu hii ya Afrika, ameonesha kile ambacho amekiita utatanishi na ukimya katika Rasimu ya Katiba Mpya.

Kwa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kama ilivyo kwa wadau wengine ambao wamezungumzia Rasimu hiyo ya Katiba, eneo muhimu pengine kuliko yote ni muundo wa Jamhuri ya Muungano kama shirkisho lenye Serikali tatu. Kwa sababu hiyo, Rasimu ya Katiba iliyotolewa na Tume imejikita katika masuala ya Muungano tu. Kwa mujibu wa Mwenyekiti wake, Tume haikushughulikia masuala yasiyokuwa ya Muungano ya Tanganyika na Zanzibar, kwa sababu mambo hayo yanatakiwa kushughulikiwa na Katiba za Washirika wa Muungano.

Kwa maana hiyo, masuala haya sasa itabidi yashughulikiwe kwa utaratibu mwingine wa kisheria Zanzibar na Tanganyika vilevile, ambao utakuwa tofauti na utaratibu uliowekwa na Sheria ya Mabadiliko ya Katiba. Kutokana na mapendekezo ya Rasimu ya Katiba, mchakato wa Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano hautakamilika bila ya kuwepo na kukamilika, kwa mchakato wa Katiba Mpya kwa masuala yasiyokuwa ya Muungano ya Tanganyika na ya Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanza na kukamilika kwa mchakato wa Katiba Mpya kwa mambo yasiyokuwa ya Muungano ya Tanganyika na Zanzibar ni suala muhimu kwa muundo wowote wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano au hata bila Muungano kuwepo, kwa sababu zifuatazo: Kwanza, hata kama muundo wa Muungano utakuwa wa Serikali moja au mbili za sasa au tatu zinazopendekezwa na Rasimu, ni lazima masuala yote yanayoihusu Tanganyika yaingizwe kwenye mchakato wa Katiba Mpya. Hii ni kwa sababu Rasimu inahusu masuala saba ya Muungano tu na Zanzibar ina Katiba yake tayari.

Pili, hata kama Wananchi wa Tanzania watakataa kuendelea na Muungano wa aina yoyote na kudai uhuru kamili wa Washirika wa Muungano, bado masuala ya Katiba Mpya ya Tanganyika na Zanzibar yatahitajika kufanyiwa kazi.

Tatu, bila masuala ya Tanganyika kuamuliwa katika Katiba Mpya, mchakato mzima hautakamilika na kwa maana hiyo, hakuwezi kukawa na uchaguzi wowote wa Jamhuri ya Muungano kwa upande wa Tanganyika.

Kwa vyovypole vile, *constitutional gridlock* hii lazima ipatiwe suluhisho. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kwamba, mchakato wa Katiba Mpya ya Tanganyika na marekebisho ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 uanze mara moja ili uendane sambamba na mchakato wa Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano. Kwa vyovypole vile, kwa maoni yetu, Sheria ya

Mabadiliko ya Katiba kama ilivyo sasa haiwezi kutumika kwa ajili ya mchakato huo kwa sababu Sheria hiyo ilitungwa kwa ajili ya mchakato wa Katiba ya Muungano tu.

Tume ya Mabadiliko ya Katiba iliundwa kwa ajili ya mchakato wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Tume yenye we imekiri kwamba, haikujishughulisha na masuala yasiyokuwa ya Muungano kwa sababu hayakuwa sehemu ya majukumu iliyokabidhiwa kisheria. Kwa muundo wake, Tume hiyo haiwezi kujibadilisha na kuwa Tume ya Katiba ya Tanganyika. Kwa maana hiyo, mchakato wa Katiba ya Tanganyika unatakiwa kuwekewa utaratibu mpya na tofauti kabisa wa kisheria na wa kitaasisi. Hii itahitaji kutungwa kwa sheria mpya kwa ajili ya mchakato huo.

Sambamba na mchakato wa Katiba ya Tanganyika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kuanzishwa kwa mjadala juu ya masuala ya mpito, kwa sababu kuna uwezekano mkubwa kwamba Katiba Mpya, ya Muungano peke yake au ya Muungano na za Washirika wake, yaani Tanganyika na Zanzibar, zisiwe tayari kabla ya Uchaguzi Mkuu wa 2015; au hata kama zitakuwa tayari kabla ya Uchaguzi Mkuu, kuna uwezekano mabadiliko makubwa ya kisheria na ya kitaasisi yatakayohitajika kwa ajili ya utekelezaji wa Katiba Mpya, yasiwe tayari kabla ya Uchaguzi Mkuu ujao. Kwa kuangalia mfano wa Kenya, Katiba Mpya ya nchi hiyo ilikamilika mwezi Agosti, 2010. Hata hivyo, mabadiliko mbalimbali ya kisheria na kitaasisi kwa ajili ya utekelezaji wa Katiba hiyo, yalichukua zaidi ya miaka miwili na nusu hadi Uchaguzi Mkuu wa mwezi Machi, 2013.

Ikumbukwe kuwa, Kenya haikuwa na suala la Muungano kama Tanzania. Sisi tuna Muungano wa muundo ambao upande mmoja wa Muungano huo una Dola yenye Katiba na Taasisi kamili za Dola, wakati upande mwingine hauna Dola wala Katiba na taasisi kamili za Dola. Hii ina maana kwamba, maandalizi yetu ya kisheria na kitaasisi yanaweza kuhitaji muda mrefu zaidi kuliko ilivyokuwa kwa Kenya. Hatuna budi kuanza kuyafikiria na kuyajadili mambo haya muhimu kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naomba nikushukuru na ninaomba kuwasilisha. Ahsante sana. (*Makof*)

Kwa yale ambayo sikuyasema, naomba yaingie kwenye *Hansard*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu, nakushukuru sana. Mheshimiwa Tundu Lissu ni Waziri Kivuli na ni Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Katiba na Sheria. Tunakushukuru sana.

Naona kuna Wabunge wawili wamesimama; kuna mwingine?

Haya naomba nifunge orodha, tuanze na Mheshimiwa Eng. Mnyaa!

## **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:**

Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama hapa kwa heshima na taadhima, kuomba mwongozo wako, kwa Kanuni ya 68(7) kuhusu mambo ambayo yametokea hivi karibuni hapa katika Maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani na Maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kulizungumza jambo halisi ambalo nataka mwongozo wako, naomba nilikumbushe Bunge lako na ninaomba ninukuu *Hansard* ya Mkutano wa Tatu, Kikao cha Kwanza cha Tarehe 5 Aprili, 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika *Hansard* hiyo, ni mimi Mnyaa niliyesimama hapa kama leo nilivyosimama, nikaomba Mwongozo wa Spika. Nanukuu, baada ya kusema hivyo, Spika ananiuliza; Mwongozo wa Spika kuhusu maneno yangu? Nikamjibu, Mheshimiwa Spika, ndiyo, kuhusu maneno yako, ambayo yametufurahisha sana, lakini kuna tatizo dogo tu kwamba, umeagiza hii Kamati ya Katiba na Sheria, kusikiliza Wadau hapa Dodoma na Dar es Salaam, lakini hili suala ni la nchi nzima, la Muungano wa Tanzania. Zanzibar tuna Ofisi ya Bunge, ambayo haijafanya kazi. Nikaendelea, kwa nini Kamati hii ya Katiba na Sheria kikundi kimoja kisiende Ofisi ya Bunge Zanzibar, wakasikiliza maoni ya wadau wako ili kukamilisha Jamuhuri nzima ya Muungano mbali ya Mikoa? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa leo tuko hapa tunataka kujadili Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya

Mabadiliko ya Katiba. Kwa maoni ya Kamati ya Sheria na Katiba, wamesikiliza Wadau wengi, lakini hawakwenda kusikiliza Wadau wa Zanzibar. (*Makofi*)

Hili suala zima la mambo haya ya Katiba linahitaji *equality* ya *partner states*. Tunazungumza kitu kinachohusiana na Zanzibar na hapa Tanganyika kupata kitu cha maoni ya Katiba vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna uhalali gani wa Bunge hili kuendelea na mjadala huu, wakati upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano hawajasilizwa na hili ni jambo la maoni ya Katiba? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako kuhusu suala hili.

## TAARIFA

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa Mheshimiwa Pindi Chana.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, bila kuathiri maelezo yaliyotolewa mwanzo, *without prejudice*, naomba kwa mujibu wa Kifungu cha 68(8), kutoa taarifa kwa Bunge lako Tukufu kwamba; Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ilialika Wajumbe mbalimbali mbele ya Kamati.

Miongoni mwa Wajumbe walioalikwa ni pamoja na Wajumbe wa Zanzibar. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima zote na taadhima ya Jamhuri ya Muungano, miongoni mwa Wajumbe walioalikwa ni pamoja na Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Taarifa.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Pamoja na Wadau mbalimbali ambao walikuja mbele ya Kamati na ratiba ya kazi ipo kwenye mihtasari.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Kuhusu utaratibu.

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi pamoja na Maafisa wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, walialikwa kutoa maoni mbele ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, naomba mkae chini na tusikilizane. Mheshimiwa Halima Mdee na wengine wote, kaeni chini na tusikilizane. Naomba kila mmoja wetu atulie.

Jambo lililo mbele yetu ni muhimu na kubwa, linalohusu masilahi na hatima ya nchi hii. Tunategemewa na tunatazamwa na Watanzania wote, kwamba, tutatuliza vichwa na kuhakikisha tunaonesha njia. Nimeombwa mwongozo, nitatoa majibu hayo baadaye. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mnyika!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 5(2), ambayo naomba noisome: "Spika atawajibika kutilia nguvu Kanuni zote za Bunge na Mbunge yeyote atawezaka kusimama mahali pake na kumwarifu Spika kuwa Mbunge fulani amekiuka Kanuni." Kanuni ya 66(7), kwamba, mjadala wakati wa Muswada wa Sheria Kusomwa Mara ya Pili, utahusu ubora na misingi ya Muswada huo tu.

Naomba mwongozo wako kwa kurejea mamlaka yako ya Kanuni ya 68(7), kuhusu jambo linaloruhusiwa au ambalo haliruhusiwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda mfupi uliopita, Mheshimiwa Waziri wakati anawasilisha hoja na baadaye tumepewa nakala ya Jedwali la Marekebisho ya Sheria, ambalo lina sehemu C ya Sheria inayohusu kifungu kipya kabisa cha 22(a), ambacho hakikuwepo kabisa katika Muswada wa awali, ambayo ndiyo hoja ya msingi inayojadiliwa hivi sasa.

Pamoja na Sehemu E ya Jedwali la Marekebisho ya Sheria, ambayo imeongeza Kifungu cha 26,

kinachokwenda kuchakachua mamlaka ya upitishwaji wa Katiba, ile mbili ya tatu na badala yake kuweka mfumo wa *simple majority* kwenye upitishaji wa awamu ya tatu.

Hoja ya msingi hapa ni kwamba, mapendekezo yote haya ni mapya kabisa ambayo yamewasilishwa kinyume na Kanuni ya 86(7) ya Bunge na mapendekezo haya hayajajadiliwa na Wadau. Ninaomba nithibithishe hili kwa sababu mimi nilikwenda mbele ya Kamati kwa niaba ya Chama cha CHADEMA na Vyama vingine vikiwepo, haya mapendekezo hayakuwepo kabisa mbele ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako, kama jambo hili linaruhusiwa na utumie madaraka yako sasa kwa mujibu wa Kanuni ya 5(2) kama ilivyopendekezwa na Kambi Rasmi ya Upinzani, uitake Serikali kuondoa hayo marekebisho ya kwenye kipengele cha (c) na (e) ili yasiendelee kujadiliwa kwa sababu yamewasilishwa kinyume na Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako.  
*(Makof)*

**NAIBU SPIKA:** Napokea ushauri wako, nitaufanyia kazi. Tunaendelea na utaratibu, yote mawili nitayatolea maelezo baada ya kuwa yamefanyiwa kazi kwa kina, pamoja na timu yangu ya wataalam. Niwahakikishie, pamoja na kwamba tunaongea hapa, lakini nina *machinery* ambayo inafanya kazi vizuri sana na katika muda mwafaka, nitakuwa na maelezo ya kutosha, kuhusiana na nini ni sahihi na nini si sahihi.

Kwa sasa kwa utaratibu wetu, tunaendelea na mjadala. Ninawaomba Waheshimiwa Wabunge, kwa mara nyingine, jambo hili ni muhimu sana kwetu sote na ninawaomba, kila mtu anayejadili hapa ndani aheshimike, asikilizwe na mwisho tutafika salama tu. Kila maoni yanayotolewa hapa ndani, hapatakuwa na upendeleo wa aina yoyote kutoka kwenye Kiti, tutakuwa na ushirikishaji wa kutosha na tutafika mahali salama kabisa kwamba jambo hili twende vipi au vinginevyo; naomba ushirikiano wenu.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Natumaini ni jambo lingine, kama ni jambo lingine karibu.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako kuhusu jambo ambalo limetokea sasa hivi, natumia Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani kusoma Hotuba yake, nimepokea *Memo* hapa kutoka kwa mmoja wa Wabunge aliyemo humu Bungeni, akinieleza hivi; unashabikia mambo ya Tundu Lissu leo, endelea ila mtashughulikiwa, mimi na Barwany.

Mheshimiwa Naibu Spika, haisemi imetoka wapi lakini aliyeileta, *page boy*, yupo. Ninaomba mwongozo wako juu ya jambo hili. (*Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Kwanza, naiomba hiyo karatasi ije Mezani, lakini pili ni mojawapo ya mambo ambayo nayachukua ili tuyafanyie kazi.

Waheshimiwa Wabunge, tuendelee. Sasa ni vizuri tunapokuwa tunashughulika na Mwongozo wakasimama wote na ndiyo maana nikasema jamani ni wawili tu. Vinginevyo, atakuwa yule, atakuwa yule, atasimama Mheshimiwa Tundu Lissu, atakapokaa chini atasimama mwingine, itakuwa tabu kidogo. Haya, uwe wa mwisho kwa heshima yako, tafadhalii!

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, huu Muswada ni muhimu sana na unaweza ukatujenga kama Bunge na kama Taifa na unaweza ukatugawa vibaya sana. Huu ni Muswada unaohusu Sheria ya Muungano, inayohusu sehemu zote mbili za Muungano; Zanzibar na Tanzania Bara. Wadau wa Zanzibar hawajashirikishwa, hatujaenda Zanzibar. Naomba ... (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu, naomba ukae chini. Nakuomba sana, hoja imekwishatolewa, nimeipokea na nimesema nitaifanyia kazi. Yako mambo hapa yanayohusu Kanuni, tuna Kamati yetu ya Kanuni, itabidi niitishe inishauri. Yako mambo hapa yanayohusu Uongozi, tuna Kamati ya Uongozi ya Bunge inasikia, tuna namna mbalimbali za kushughulikia haya mambo.

Tunaendelea na mjadala, katika wakati mwafaka mambo haya yatafanuliwa, kabla hatujafika kwenye

maamuzi, hatua hii tuliyonayo siyo hatua ya maamuzi, mnanielewa ndugu zangu; siyo hatua ya maamuzi. Hii ni hatua tu ya mchakato tunaendelea, hatuwezi kufika kwenye maamuzi mpaka tumeelewana kuhusu haya mambo.

Nawaombeni sana, ni vizuri tuheshimiane, haipendezi kabisa, mnapokuwa mnaongea ninyi Bunge zima linasikiliza, wenzenu wakiongea ninyi inakuwa ni fujo; siyo vizuri hata kidogo. Hakuna cha kugombana hapa, hakipo! Baada ya muda si mrefu tutapata ufanuzi wa haya mambo, sasa hivi tunaendelea na uchangiaji kama kawaida. (*Makofi*)

Nilishawataja wachangiaji wangu wa kwanza, Mheshimiwa Pindi Chana, atafuatiwa na Mheshimiwa Silinde.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote, naunga mkono hoja, lakini pia namuunga mkono sana Mheshimwia Rais Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuridhia mchakato huu wa Katiba uanzishwe Tanzania, kwa sababu akiwa ni Mwenyekiti wa Chama, angeweza kuahirisha jambo hili, lakini yeze aliamua. (*Makofi*)

*(Hapa baadhi ya Wabunge wa Upinzani  
walitoka Ukumbini)*

**WABUNGE FULANI:** Kama kawaida hao, endelea. Mmezoea, tokeni. Rudini haraka.

**NAIBU SPIKA:** Ninawaomba mnaotoka nje mtoke taratibu. Niwahakikishie ninawaona na mnanifahamu vizuri.

**MBUNGE FULANI:** Kwendeni zenu, tokeni. (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** *Tizono kwidohya!* Tokeni, tokeni. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mliotulia hapa ndani, nawaomba msiongee chochote. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge na wote wanaotuangalia, mambo yapo salama, yapo sawasawa, hii ni demokrasia. Kama nilivyosema, mara nyingi zimewahi kutolewa hoja za Mwongozo na Kanuni ya Mwongozo ipo wazi, jibu linaweza kutolewa hapo hapo au baadaye kidogo; na kwa hoja zilizotolewa, upo umuhimu wa Kiti kupata ushauri hapo baadaye kidogo wa namna ya kushughulikia na kwa ratiba yetu jambo hili haliishii hapa leo, tunaendelea nalo mpaka kesho. Kwa hiyo, tuna nafasi ya kutosha na hata ikibidi mpaka kesho kutwa Ijumaa na hata ikibidi mpaka Jumamosi, tunaweza kuendelea na jambo hili bila wasiwasi wowote. (*Makofi*)

Kwa hiyo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, tupo salama, tuendelee na uchangiaji. Mheshimiwa Pindi Chana; kabla ya Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Waziri wa Nchi!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nilifikiri nitoe taarifa kidogo kwamba, kama historia tulivyoitoa wakati tunawasilisha Muswada huu wa msingi mwanzoni, Muswada huu umeshirikisha makundi yote muhimu na hasa Viongozi Wakuu wa Vyama vyta Siasa, akiwemo Mheshimiwa Freeman Mbewe. Wameshiriki kuanzia kutayarisha Muswada huu tena mbele ya Mheshimiwa Rais, lakini hata katika Marekebisho ya Sheria mbili hizi; hii tunayoipitia leo na ile ambayo tumeahirisha ya kura ya maoni, mimi na Waziri wa Katiba na Sheria, tumekwenda Zanzibar, tumekutana na Viongozi wote na Waheshimiwa Mawaziri wanaohusika na ndiyo maana tumeahirisha hata ule Muswada kwa sababu ya heshima, hayo ni marekebisho, lakini wenzetu wamesema kwa utaratibu wa Serikali, ile ni Serikali ndiyo na wao lazima wapitie kwa Wawakilishi wa upande ule, Baraza la Wawakilishi, wapate maoni halafu waturudishie.

Nilifikiri huu ni utaratibu wa kiungwana, wenzetu wametushauri kwa sababu wanaojua maoni na kuweza kuratibu vizuri upande ule ni Baraza la Wawakilishi, tumewaachia watatuletea. Hivi ndivyo ilivyofanyika hata hii, wakati tunaanza kutafuta maoni ya Muswada huu wa pili, mimi nilikuwa Mwenyekiti wa Kamati niliyeagizwa na Mheshimiwa Rais, kuitisha makundi haya ya Vyama vyta Siasa na kwa upande wa CHADEMA, alikuja Mheshimiwa John Mnyika, Chama cha CUF na Vyama hivi ni vyta Kitaifa, alikuja Naibu Katibu Mkuu wa CUF na NCCR-Mageuzi walikuja. Kwa hiyo, ushirikishwaji huu na wenyewe kwa

Sheria hii tumekwenda tukawaambia na Viongozi wa Zanzibar, Mawaziri wanaohusika na maeneo haya ya Sheria na Katiba wamearifiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kutoa taarifa kuwa mimi nimehusika kidogo katika suala hili la kufuatilia. Hata huu Muswada ambao tumeuahirisha, tumeuahirisha kwa nia njema kwa sababu wenzetu kule wana utaratibu wao na tumeambiwa na Waziri wa Katiba na Sheria kule kwamba, Muswada ule ili upate maoni ya Wananchi lazima uende kwenye Baraza la Wawakilishi. Kwa hiyo, maoni tutayapata na huu nao Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wanaujua na walishiriki na wametoa maoni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikuhakikishie kuwa, mimi nimehudhuria kwenye hizo Kamati, wamejadili vizuri sana kwenye Kamati. Sasa haya yanayotokea kama ni sarakasi ya kisiasa sawa, lakini kwa utaratibu tumejitahidi sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Pindi Chana!

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza, niunge mkono kama nilivyosema mwanzoni na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kukubali kutuletea mchakato huu wa Katiba na huu ni mwendelezo. Marekebisho haya yapo kwa Mujibu wa Katiba na mimi ninayaunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na suala la Kamati kwenda Zanzibar. Kulikuwa kuna maombi ya Kamati kutembelea maeneo mengi, kuna watu waliomba Kamati pia iende Dodoma, Kamati pia iende katika maeneo mbalimbali kama Morogoro kwa ajili tu ya marekebisho haya ya fungu la sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilialika wadau mbalimbali wakiwemo Vyama vya Siasa kutoka Zanzibar, Mwakilishi wa Jahazi Asilia na Vyama vyote kutoka Zanzibar. Pia *Law Society* ya Zanzibar nayo ilialikwa, wakiwa pamoja na Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi, ambaye alikaa na sisi kwa muda wa wiki nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako haliwezi kutumika kutimiza matakwa ya kisiasa ya watu mbalimbali. Hapa kazi yetu ni kutunga Sheria na kama kuna maoni yoyote yale yanaruhusiwa kuletwa, muda bado upo kama tulivyoambiwa; lakini Bunge lako Tukufu haliwezi likatumika kufikisha matakwa binafsi ya kisiasa ya watu mbalimbali. Naomba katika hilo tuwe makini sana. (*Makofij*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala ambalo limezungumzwa kuhusiana na suala zima la idadi, idadi ya watu 166. Katika idadi ya watu 166 kulikuwa na maoni tofauti; wapo wadau waliokuja wakasema kwamba Wabunge wapunguzwe, kwa sababu katika Bunge la Katiba wanaingia Wabunge wa Jamhuri ya Muungano na Wabunge wa Zanzibar na 166 amba siyo Wabunge. Kuna wadau waliokuja kusema kwamba, Wabunge wapunguzwe na Kamati ilihoji kwamba unaposema

Wabunge wapunguzwe ili wadau kutoka nje waongezeke tutatumia vigezo gani. Wadau wengi waliomba jambo hilo wakalifanyie kazi. Wapo wadau walisema kwamba, idadi ya 166 ibaki vilevile, lakini izingatie suala zima la ushirikishwaji wa Taasisi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia kuwa Bunge hili lina Wajumbe 357, ukijumlisha Baraza la Wawakilishi 81, ukijumlisha 166, Bunge la Katiba litakuwa na watu 604. Baada ya kutafakari kwa kina, Kamati iliridhia kwamba, idadi ya watu ibaki ile ile ya kuingia Bunge la Katiba 166 ambapo Bunge la Katiba litakuwa na watu 604. Sababu za kubakisha 604 ni kwamba, baada ya Bunge la Katiba, suala hili linaenda kwa Wananchi (*Referendum*). Kwa hiyo, hakuna Mwananchi atakayeachwa mwisho wa siku. Kwa hiyo, suala la kuongeza 166 kwa kuwa suala hili mwisho wa siku linaenda kwa Wananchi wote, tukaona linakidhi. Wapo Wabunge wa Jamhuri ya Muungano, Wabunge wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar na Wabunge 166.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo na mimi ninaunga mkono mapendekezo ya Serikali kwamba, Wabunge waingie 166, kwa sababu suala hili mwisho wa siku kila Mtanzania, mwenye umri zaidi ya 18, mwenye haki ya kupiga kura, atapiga kura ya maoni ambayo ni *referendum*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie kuhusu suala la uteuzi. Sheria iliyopita ilisema kwamba, kutakuwa na Wajumbe 166 watakaoingia Bunge la Katiba, lakini Sheria ile ilikuwa haijataja watapatikana vipi. Serikali safari hii imekuja imesema wapatikane kwa kuteuliwa na Rais.

Sasa kuna maoni mbalimbali; mimi ninaungana na suala la uteuzi wao utokane na Rais kwamba, Vyama husika, Taasisi na Mashirika ya Dini, watachagua *list* ya majina watapeleka kwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili naomba ielewewe kwamba, Rais siyo *individual* ni Taasisi. Rais ni *machinery*, ni Chombo siyo *individual*. Majina yale yanapopelekwa ina maana wanaochagua ni Taasisi husika, kama ni Chama cha Siasa, *NGO*, Mashirika ya Dini, Rais anachofanya ni kuyachukua kutokana na ile *list* aliyopelekewa. Kwa nini lipo hivi?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Taasisi mbalimbali kupendekeza majina, mwisho wa siku ni lazima kuwepo na chombo *kitakacho-gazette*, kwa neno la Kiingereza wanatumia kutangaza. Una-*gazette* kwenye Gazeti la Serikali kwamba, Bunge la Katiba litakuwa na Wajumbe wafuatao. Hivyo, lazima kuwepo na chombo ambacho kitatamka wale watu ni akina nani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina swal; endapo hatutakubaliana kwamba Rais atue wale Wajumbe 166 ni nani atakaye-*gazette* yale majina ya Wajumbe wanaoingia kwenye Bunge la Katiba? Maana kama kila Taasisi itachagua watu wake na endapo kuna Taasisi imemuweka mtu ambaye uraia wake siyo Mtanzania, ana tatizo moja au lingine ambalo halikidhi kuwa na sifa za kuingia katika Bunge la Katiba; kwa mfano, ana *unsound mind*, amekana uraia wa Tanzania na amependekewa; kusipokuwepo chombo watu hawa itakuwaje mbele ya safari? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia maoni yangu haya, mimi ninaungana kabisa kwamba, kama tulivyofanya katika Bunge wakati wa kukusanya maoni ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba, tulikubaliana kwamba Rais ateue wale Wajumbe. Kwa hiyo, katika hili naungana kabisa kwamba, Rais pia atumike kuteua yale majina 166 kwa sababu Vyama mbalimbali, Asasi za Kidini zitapeleka na yeze atatumika pale kuteua majina yale 166.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ni muhimu naomba niseme kwamba, katika Muswada huu tumekubaliana kwamba, theluthi moja watatoka Zanzibar. Ninaungana mkono na kukubaliana kwamba, theluthi moja ya Wajumbe watoke Zanzibar kama ilivyopendekezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaungana kwa sababu katika Wajumbe watakaoingia kwenye Bunge la Katiba, hapa tunafuata *proportional to the population*. Kwa hiyo, ninaungana asilimia 100 kwamba, theluthi moja ya Wajumbe watoke Zanzibar kama ilivyopendekezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lilikuwepo suala la kuongeza idadi ya siku. Muswada umependelekeza kwamba, endapo Mwenyekiti wa Bunge la Katiba ataona inafaa, kwa kushauriana na Rais, ataongeza siku zisizozidi 20.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupendekeza kwamba, idadi ya siku tusiziwekee *limitation*, kwa sababu

Bunge la Katiba unaweza ukahitaji siku zaidi ya 20 na endapo Sheria ikitumia ataongeza siku 20, basi itabidi tufanye utaratibu wa kuirekebisha kwanza Sheria. Hivyo, naungana na mapendekezo ya Serikali kwamba, isomeke endapo Bunge la Katiba litahitaji kuongeza muda, litaongeza muda kadiri itakavyofaa kwa kushirikiana Mwenyekiti na Rais Jamhuri ya Muungano na hapa wanasema ni Mwenyekiti wa Bunge la Katiba kwa kushirikiana na Rais, kwa sababu kuna suala la bajeti, ambayo ni lazima ijadiliwe juu ya matumizi ya Bunge la Katiba ambapo kwa mujibu Sheria, Bajeti hiyo inatoka *Consolidated Fund*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niunge mkono hoja na maoni yangu mengine yapo kwenye maandishi. Ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Nashukuru sana. Tunaendelea na uchangiaji, lakini naomba nifafanue tu kidogo. Tukumbuke kuna Watanzania wanaotufuatilia kwa karibu, ni kwamba, Kamati zetu kwa kawaida zinapokuwa na Muswada zina vituo viwili tu vya kufanya kazi navyo huwa ni Dodoma na Dar es Salaam. Wadau huwa wanaalikwa nchi nzima kuja ama Dodoma au Dar es Salaam.

Kwa hiyo, kwa Muswada uliopo mbele yetu na kazi ambayo ilifanywa na Kamati ilifanywa sahihi kabisa kama Sheria nyingine ambazo zimefanyika huko nyuma na ndivyo itakavyokuwa hata huko mbele ya safari. Vituo vyetu vimeduwa ni Dodoma na Dar es Salaam lakini tunaalika

wadau kutoka nchi nzima na nchi hii ni moja, kupitia Sheria zetu na Miswada yetu.

Kwa hiyo, nilifanya busara tu nikasema mambo haya nitayatolea ufanuzi zaidi baadaye, hasa baada ya kupata ushauri mwagine, lakini *so far* hakuna tatizo kubwa kiasi hicho. Tutashauriana mbele ya safari kuona namna gani hasa katika jambo kama hili. Kwa kadiri ambavyo sisi huwa tunafanya kazi, hakuna aliyebaguliwa wala hakuna chochote. Hili ni jukumu la Kamati kutangaza na kuwaalika wadau, tena Zanzibar kuja Dar es Salaam ni karibu kuliko Bukoba, kuliko Mwanza au kuliko Dodoma.

Mchangiaji wetu wa pili atakuwa ni Mheshimiwa Ester Bulaya na Mheshimiwa Nchambi kama yupo tayari na Mheshimiwa Betty Machangu ajiandae. Mheshimiwa Ester Bulaya!

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru nami kwa kunipa nafasi niweze kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa umri wangu mdogo, najua kuna watu ambao wamenizidi, ningependa niongee maneno mawili, matatu, kwa uchungu mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania wafahamu kitu kimoja na vijana wenzangu wanaonisikiliza ambao mimi na wao kama tusipokufa na maradhi haya mengine, kama tusipokufa na ajali, tuna maisha marefu sana ya kuishi katika Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania hii ni zaidi ya CUF, Tanzania hii ni zaidi ya CHADEMA, Tanzania hii ni zaidi ya TLP, ni zaidi ya NCCR-Mageuzi, ni zaidi ya Chama cha Mapinduzi. Tanzania hii ni yetu sote, tukijumuisha upande wa Zanzibar na upande wa Tanganyika. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningependa kwa moyo wa dhati, kama wenzangu, Wazee, Viongozi wa Vyama vyaa Siasa wanavyonisikia, hatima ya nchi hii, amani ya nchi hii, tumeibeba sisi Wanasiasa. Sikatai kwamba, wote sisi tuna watu huko nyuma, lakini tusi-*take advantage* ya kutumia wafuasi wetu kuliparaganyisha Taifa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naongea haya kwa uchungu wa kuona tulitengeneza mazingira ya kuanza pamoja, tunatengeneza mazingira ya kutugawa *unnecessarily*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo umesema, suala hili linajadilika, Katiba ya Nchi hatususiani, hatuviziani. Kama Viongozi wenyewe maono, kama Viongozi ambao tunalitakia mema Taifa hili, tunatakiwa tukae pamoja, tuzungumze pamoja. Hivi vitu tunaweza tukafanya kwenye bajeti, lakini siyo kwenye hatima ya Taifa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Waheshimiwa Mawaziri, mnanisikia kama ambavyo umesema, bado tuna nafasi, siyo vibaya pia mkitoa tena nafasi ya pili kama alivyosema Mheshimiwa Lukuvi, kukaa tena na Viongozi hawa wa kisisa tuone tunaendaje. Kwa sababu tuna dhamira njema na wala siyo kwamba eti haya matakwa

yote ni ya Chama cha Mapinduzi hapana, ingekuwa hivyo tungeenda na msimamo wa kwanza mbona watu walirudi na wakajadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi kwanza ningependa kuzungumzia kipengele cha Muswada ambacho Serikali imefanya mabadiliko ambapo jambo la kwanza lile lilikuwa linasema kwamba, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikuwa anapaswa kuwa Mwenyekiti wa Bunge Maalum, lakini nimeona Serikali imeleta marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami kwa mtazamo wangu bado kipengele hiki kingepaswa kuwa vilevile. Kwa sababu Mwenyekiti wa muda kazi yake kubwa ni kusimamia tu lile zoezi la kutunga Kanuni kwenye Bunge Maalum, lakini mamlaka ya kutunga na kubadilisha yote yanabaki katika Bunge Maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza kwamba, Mwenyekiti wa muda kutokana na *experience* yake ya kuendesha Shughuli za Bunge na masuala ya Kanuni, bado ingetakiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano angekuwa tu Mwenyekiti wa Bunge Maalum, hatoathiri chochote, kwa sababu mwisho wa siku wenye mamlaka ya kupitisha Kanuni bado yatabaki kwa Bunge Maalum. Hili nilikuwa naomba kulisisitiza sana kutokana na *experience* ya utungwaji Kanuni wa Bunge letu.

Katika hili mimi pia nitaleta Jedwali la Marekebisho kuona ni bado kuna umuhimu wa Mwenyekiti tu wa muda,

kwa sababu hatoingilia chochote, kwani bado Ukurugenzi wa Uchaguzi utabaki kwa Katibu wa Bunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na utabaki kwa Katibu wa Bunge la Baraza la Wawakilishi.

Yeye atakachofanya ni kusimamia tu, kwa sababu wote ambao watakuwepo siyo wote ambao wana utaalal wa masuala ya Kanuni. Yeye atakachofanya atasimama tu lile zoezi, lakini pia siyo mbaya akitoa ushauri wake kama mtaalam pia wa masuala ya Kanuni. Kwa hiyo, mimi pia nitaleta Jedwali la Marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nitaleta Jedwali la Marekebisho katika kifungu cha 23 cha Sheria mama. Kifungu cha 23 ambacho kinasema, na hii naomba niiseme wazi kabisa kwamba Mwenyekiti akitoka Bara, Makamu atoke Zanzibar. Hii yote ndiyo inayotuletea haya! Kama sisi wote ni wamoja, achaguliwe mtu kwa sifa zake. Tukianza kujigawa hapa U-bar, U-tanganyika sijui U-zanzibar, mwisho wa siku hatutafika salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani kama kuna sifa ya Mwenyekiti wa Bunge Maalum la Katiba kutoka Zanzibar, achaguliwe. Kama kuna sifa za Mwenyekiti kutoka upande wa pili wa Muungano achaguliwe, kuliko kuanza kubaguana moja kwa moja kwenye sheria. Wenyeewe tunaanza kujigawa kwenye sheria, kwa nini tusiache ili mwenye sifa apate? Mapendelekezo yangu haya pia yanakwenda katika kifungu cha 24(2) na yenyeewe pia nitaleta mapendelekezo. Mapendelekezo yenyeewe yanasema: "Kama Mwenyekiti akitoka upande mmoja wa Muungano,

basi Katibu atoke upande mwingine." Kwa nini tunayaleta haya? Haya ndiyo yanatuletea sababu ya kupata matatizo yote. Tuache watu wapate hizi nafasi kwa sifa zao, tusianze kujibagua hapa U-zanzibar na U-baru bila sababu ya msingi, tena tunakwenda kuweka kwenye kanuni. Je, kama wote wakitoka Zanzibar, kuna tatizo gani? Si wana sifa? Mimi hilo nitaleta katika jedwali langu la marekebisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ningependa kuongelea kifungu kipyu ambacho kimeletwa na Serikali, ni kweli kwenye Sheria mama kilikuwa kimeleta utata. Kama Bunge Maalum lisipofikia makubaliano kwa yale ambayo yamejadiliwa, na Serikali imeleta marekebisho mazuri tu kwamba tusipofikia theluthi mbili kila upande, kikubwa, yale ambayo yamechukua muda katika kubishaniwa, tutoe nafasi ya *ku-debate* mara ya pili. Ikishindikana twende kwa *simple majority*. Mimi hili naliunga mkono kwa asilimia kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini unapozungumzia suala la uteuzi, huwezi tena kurudi kuweka masharti. Wenyewe wadau wameamua kwamba, *fine!* Rais atue, mnampelekea majina matatu. Sasa leo hii Rais atakapoteua, useme kwa nini umemwacha huyu namba moja umemchukua namba mbili? Hebu turudishie *feedback*; hicho kitu hakipo! Kwa sababu mwisho wa siku mpaka unampeleka namba moja, mbili na tatu ina maana sifa na vigezo vyote vinafanana. *Unless otherwise wangesema hatutaki* Rais atue. Lakini kama wamemwamini katika hilo, kuna dhambi gani akiteua kati

ya hao? Kwa hiyo, hilo pia ningependa sana kulisisitiza.  
(*Makofî*)

Vile vile suala la hizi siku 20 kuongezwa, kuwepo kwenye Kanuni, hili na lenyewe siyo sahihi. Ni bora likaachwa wazi. Kama kutakuwa na mahitaji ya muda kuongezwa, basi hawa watu ambao wamependekeza kushauriana na Rais wa Zanzibar na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania waone ni jinsi gani ambavyo watashauriana kuongeza siku za Wajumbe wa Bunge la Katiba kuendelea ku-*discuss issue* ambayo iko mbele yetu, kuliko kusema tujifunge kabisa kwenye sheria siku 20. Zisipotosha hatutakuwa na mamlaka ya kisheria kuongeza tena siku. Lakini ikiwa wazi, hii pia itasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasisitiza sana, Taifa hili linatutegemea. Tuna uwezo wa kulibomoa sisi wenyewe na tuna uwezo wa kulijenga sisi wenyewe. Tanzania inatutegemea sisi kama viongozi. Ni bora twende sambamba kuliko kuachana njiani kama hivi watu ambavyo wanaanza kuonyesha hizi ishara. Machafuko siyo mazuri. Leo hii tuna maadui ambao wanatuzunguka. Kwa nini tutake tena kutengeneza maadui wa ndani tujimalize wenyewe kwa wenyewe? Jambo hili siyo zuri. Tunahitaji kujengenchi yetu kwa amani na upendo na mshikamano wa dhati. Katika suala la Katiba, tunahitaji kuwa *sober*, tuache hivi *vi-element* vya itikadi zetu, ndivyo vinavyotupeleka hapa, tuone ni jinsi gani ambavyo tutalifikisha hili gurudumu salama na nchi ikibaki na amani. Kama ambavyo amesema Mwenyekiti wa Kamati, mwisho wa siku Watanzania wote watashiriki katika kura ya maoni.

Nilikuwa naomba sana tuzingatie hayo kama Watanzania tuna haja ya kuwa pamoja katika suala zima la Katiba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mungu ibariki Tanzania. Naamini tutafika salama. Naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Ester Bulaya kwa maneno yako ya busara sana. Sasa namwita Mheshimiwa Suleiman Nchambi, atafuatiwa na Mheshimiwa Betty Machangu.

**MHE. SULEIMAN MASOUD NCHAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nami nipate fursa ya kuleta mawazo ya wananchi wa Kishapu na Watanzania kwa ujumla waliotubariki sisi na kutuombea tushinde ili tuje tuwawakilishe na kuleta mawazo yao, kwa sababu Bunge hili lisingeweza kuingiza Watanzania milioni 45 na badala yake limetuamini sisi Wabunge wachache ili tuweze kuleta mawazo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza ninukuu maneno machache sana kwa ruhusa yako *widohya*, kujishusha. Sisi Wasukuma kule, Wabantu tuna maneno mazuri sana lazima ujishushe. Watanzania wametuamini sisi Wabunge kutoka maeneo mbalimbali tuje tufanye kazi ambayo wametutuma, Bunge likiwa ni chombo muhimu sana cha kuwawakilisha Watanzania wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachowea kusema, kwanza ni juu ya mashaka ya Wajumbe watakaokuja

kuchangia suala zima la Katiba, katika Bunge Maalum la Katiba. Sidhani kama kuna Mbunge yejote humu ndani ama Mwakilishi yejote atalishwa maneno aje afungue mdomo wake kama *radio cassette* na kusema yale aliyolishwa. Atatoa mawazo kwa uhuru na Watanzania wataangalia kile ambacho anakisema, na mawazo yetu sisi Watanzania hata katika uwakilishi huo hayatalingana kama vilivyo vidole vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilichotaka kusema ni kwamba, shaka ya uwakilishi naomba tuiondoe. Sisi wenyewe Watanzania tuliochaguliwa kuja kuwawakilisha Watanzania, leo tunaonesha shaka kubwa sana na wasiwasi kwa Watanzania. Walitutuma tuje tuwasemee humu, lakini watu wanakimbia kuwawakilisha Watanzania waliowachagua. Hiyo ni shaka kubwa sana. Naomba niseme tu kidogo kwamba tusifanane na wale wanafunzi wa Yesu waliosinzia katika milima ya Mizaituni. Sasa hawa hawasinzii, ila wametoroka kabisa katika milima ya Mizaituni na kuacha chombo muhimu kisitoe maamuzi na mawazo ya Watanzania. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, liko neno hapa limesemwa kwamba uchaguzi hautafanyika. Msidharau! Aliyesema neno hilo, kwa sababu mawazo yake na mawazo ya watu waliomchagua yanahitilafiana. Kwa hiyo, shaka juu ya Uchaguzi mwaka 2015 pengine hatarudi Bungeni humu kwa sababu hafanyi kazi ya watu waliomchagua, ni kubwa sana. Ndiyo sababu anatoa angalizo na kuomba uchaguzi usifanyike, usogezwe. Uchaguzi hausogezwi, mwaka 2015

tunapiga kura na Watanzania watatoa maamuzi yao kwa wale waliofanya kazi ya uwakilishi wa kweli. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wako watu wanatumia Bunge kama jukwaa la kisiasa kujenga chuki kubwa ya Uzanzibar na U-tanganyika. Sisi wote ni Watanzania. Naomba sana chuki hii inayoletwa hapa Bungeni, inayosemwa Bungeni, Watanzania na nchi yetu ni miongoni mwa nchi ambazo kwa kweli zinaongoza kwa utulivu wa hali ya juu. Sasa tusianze kuchukua maneno machache ya kupandikiza chuki kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoweza kusema, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete ni muungwana sana, ana mapenzi makubwa na Watanzania na ndiyo sababu aliridhia hata Katiba, akasema Katiba iliyoko sasa haiendani na matakwa ya Watanzania. Lazima tuingie katika mchakato wa kutafuta Katiba mpya. Ameridhia, sasa maamuzi na vikao mbalimbali vinafanyika, wanahudhuria, wanatoa mawazo, lakini inapofika suala la kuja hapa Bungeni, kwa sababu wanaonekana kwa Watanzania sana, kwa kweli wanahitilafiana na mawazo ya watu waliochangia na wao wakiwa miongoni mwa watu ambao wamechangia vizuri sana. Kwa hiyo, nilitaka nitoe angalizo kwa Watanzania wenzetu walioko nje ya Bunge hili, tuepuke sana Bunge hili kutumika kwa ajili ya kutaka kutugawa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Mwenyekiti wa CCM siyo dhambi. Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kuwa

Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi siyo dhambi. Mbona Mheshimiwa Mbewe amegombea mara mbili na ameshindwa akiwa Mwenyekiti wa CHADEMA? Dhambi yetu sisi iko wapi? Hakuna dhambil! Katibu Mkuu wa CHADEMA aligombea. Kuna dhambi gani? Kwa hiyo, naomba tuondoe hitilafu zetu na kama tunatamani madaraka, basi Watanzania wanatuona, watachagua watu walio makini. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu idadi ya Wajumbe 604, kama Wabunge hawa wachache tu wamechaguliwa na Watanzania na wanalikimbia Bunge hili, hawa 604 tuna mashaka gani? Mashaka yako wapi? Wingi wa watu siyo wingi wa mawazo. Kwa kweli idadi hii nadhani inatosha na inafaa na idadi hii nina imani wale wote watakaokuwa wakiwakilisha Watanzania kupitia idadi hii watakuwa na mawazo mazuri na uchungu na Watanzania kama alivyo Mbunge wa Jimbo la Kishapu Suleiman Nchambi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuendelee kuziheshimu na kuzitii mamlaka zilizoko duniani kwani ni mfano wa mamlaka zilizoko Mbinguni. Haya ni maandiko na kila Mbunge hapa ana imani na dini yake. Sina imani na mashaka kabisa kwamba Watanzania hawatatendewa ndivyo sivyo. Mwisho wa yote, Watanzania watakwenda na wao kupiga kura za maoni ikiwa ni ile huruma ya Rais na Serikali yake ya kuhakikisha kila Mtanzania anashiriki vyema juu ya Katiba mpya ya nchi yetu.

Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, mapendekezo ya Taasisi yana dosari gani? Kama alivyo eleza Mheshimiwa

Ester Bulaya imepelekwa orodha ya watu kumi, amechaguliwa mmoja au wawili, au watatu wameachwa wengine; dhambi ama makosa ya Mheshimiwa Rais yako wapi? Wale wote waliokwenda wanafaa kama ilivyo taratibu wakati wa Uchaguzi. CCM yanarudi majina matatu, yote yanafaa, tunachagua moja; CHADEMA ndivyo ilivyo. Tume ya Uchaguzi ya Taifa wanachukua fomu, mko kumi, Watanzania wanachagua mmoja. Hili halina mashaka na wala siyo dhambi. *Sizano kwidohya nalibhabhila bhakujija bha CHADEMA, sizano kwidohya. Kwigwa gombolo mpaka mi ni nguma tu.* Kusikia kwa kenge mpaka umpige mwili, masikio yatoe damu ndiyo atasikia. Watanzania hawahitaji kauli hiyo. Watanzania ni wasikivu, wanahitaji Wawakilishi ambao ni wasikivu. *Kwidohyagi!* Jishusheni kabisa katika kuwawakilisha Watanzania, na msipofanya hivyo kwa kweli Watanzania wanawashangaa sana. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuja kuwawakilisha Watanzania humu, mnakimbia nje ya Bunge, mnawaacha Watanzania wameduwaa, lakini naomba tu, siku zinakwenda, Mungu atatusaidia tutafika katika hatua nyingine ya kuwachagua Wawakilishi ambao watashinda humu Bungeni na kuwawakilisha Watanzania kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ninalotaka kusema ni kuangalia amani ya nchi yetu. Amani ndicho kitu ghali duniani kuliko mambo yoyote. Leo hii tunaingia Bungeni, kama kweli Serikali ya Mheshimiwa Rais ina matatizo, isingewapa uhuru wa kuongea humu ndani ya Bunge.

Amani yetu ya CCM ndiyo imelikisha Bunge hili mpaka kwenye mchakato wa kuongelea, kujadili mchakato mzima wa Katiba hii. Tusichezee amani ya nchi yetu, tusibaguane sisi Watanzania, Viongozi tusiwe vinara wa kuwagawa wananchi, kuwajengea na kutia chuki miyo ya Watanzania.

Waheshimiwa Wabunge, naomba sana suala hili la amani kila mmoja atakaposimama hapa kwa nafsi yake aombe nchi hii tumalize suala hili kwa amani, tuiombee amani kwa nchi yetu. Wachache watakaotaka kuvuruga nchi yetu, mambo yakiharibika, wataruka na helikopta na sisi tulioko katika ardhi hii ya Watanzania tutakosa pa kukimbilia. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, naomba suala hili tulipe kipaumbele. Naomba Watanzania, baada ya hatua nyingi na kubwa ambazo zimepitiwa, tena kwa gharama kubwa ili kupata uwakilishi wa wakulima, wafugaji, wafanyakazi na Taasisi mbalimbali, waendelee kuamini Serikali yao imezingatia hasa mawazo na matakwa ya Watanzania wa jamii na maeneo yote ambayo yameletwa hapa na kuridhiwa na Serikali hiyo hiyo ya Chama cha Mapinduzi, Serikali sikuvi, Serikali inayowapenda Watanzania, Serikali inayowatumikia Watanzania na kuhakikisha inaharakisha kazi za maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *Wabeja* sana mtani wangu. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Nchambi kwa mawazo yako ya busara sana. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Betty Machangu, atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Nkamia.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami naomba nishukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia. Napenda niseme kwamba kama kila Mtanzania ataweka hii *slogan* ya Tanzania kwanza, kwenye kichwa chake, hakika tutatengeneza Katiba nzuri. Unamwona hata mzee wangu Mheshimiwa Mrema, kwake ni Tanzania Kwanza, *TLP* baadaye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, labda ndiyo maana ukikaa na makundi, wanakwambia mnaharakisha nini? Mtamaliza, ili ikija 2015 tuwe hatuna Katiba. Naomba tuwaambie, hatudanganyiki!

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye vifungu. Kifungu cha 22 (1) (c), wako wale Wajumbe 166. Wajumbe hawa wameainishwa kutoka kifungu cha kwanza, *roman* (i) mpaka (ix). Mimi nilikuwa nashauri, Wajumbe hawa waende kama ambavyo wameandikwa kwenye Sheria mama. Kwa nini? Kwa sababu Wajumbe hawa wako wa aina nydingi sana. Kwa mfano, ukisema Asasi zisizo za Kiserikali, yako makundi mengi sana; Ukisema Asasi za Kidini, yako makundi mengi sana. Mwisho wa siku, yako makundi ambayo yataachwa na jinsi ambavyo leo yametajwa na wasomaji waliosoma, Msemaji wa Kamati ya Katiba na hata Msemaji wa Kambi ya Upinzani, wale

waliotajwa, nakuhakikishia kesho utaona kwenye magazeti kuna ambao watakuwa wamelalamika wameachwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ili kuondokana na tatizo hilo, nashauri kifungu hicho kiende kama kilivyo. Mheshimiwa Rais ana madaraka yake yeye na Taasisi yake, ana mamlaka yake, ana dola, anaweza kuchambua majina yao akajua na tabia zao na kama kweli wanawakilisha makundi hayo waliyotaja. Hatuna haja ya kumpangia Mheshimiwa Rais. Tunaamini kabisa kwamba kama alivyochagua Tume ya Katiba ya watu wenyewe weledi na busara za hali ya juu na hili nalo watalifanya vizuri. Kwa hiyo, naona hakuna haja sisi tumpangie Mheshimiwa Rais. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niongelee kifungu cha 24(4) katika marekebisho yake. Naungana na Serikali kwa yale marekebisho waliyosema kwamba Katibu wa Bunge aruhusiwe kuteua Watumishi wa Bunge, lakini inawezekana pia akaruhusiwa kuteua Watumishi wa Umma kwa wale ambao wataonekana wanafaa na kwa idadi ambayo inafaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu kingine ambacho napenda niunge mkono, ni marekebisho ya kifungu cha 26. Kifungu hiki kilikuwa hakipo na kwa bahati nzuri mtoa hoja ameleta *amendments*. Naungana na Serikali kwa hiki kifungu. Nilikuwa na hofu toka mwanzo, nikasema sasa kama tukifanya uchaguzi *round* ya kwanza, halafu hatukupata theluthi mbili, itakuwaje? Lakini kwa bahati nzuri, hiki kifungu kimekuja, nashukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilikuwa najiuliza, kama tukipiga *round* ya kwanza tukakosa theluthi mbili, tunaendelea kupiga *round* ya pili kabla hatujapumzika? Kama tukipiga *round* ya pili haikuwezekana, ikabidi twende *round* ya tatu, nako tunaendelea moja kwa moja au inakuwaje? Nikafikiria nikasema, hili Bunge litakutana wapi? Nikasema, kama ni Dar es Salaam na joto lile ukimweka mtu Dar es Salaam kwa siku 70 na anapiga kura inashindikana halafu anakaa anaendelea, nikafikiri labda kunahitajika kuwe na kipindi cha watu kupumua. Pengine watu wakipiga kura ikishindikana kuwepo na kama wiki moja ndipo kura irudiwe. Naomba kuishauri Serikali hivyo, kama inawezekana Serikali ije na muundo wa namna ambavyo itakuwa. Lakini nina hofu kwamba, kwa joto la Dar es Salaam kama itakuwa ni Dar es Salaam, inawezekana kabisa watu wakawa wamechoka na kuwaweka pamoja kwa muda wote na kupiga kura yenye ufanisi ikashindikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata ikiwa Dodoma, watu pengine hawajakaa siku 70 mahali pamoja, Wabunge mnakaa kwenye Bunge la Bajeti, lakini wao hawajakaa. Kwa hiyo, nataka ku-*imagine* kwamba inawezekana pia kukawa na watu kutoroka na mwisho wa siku usiwe na *quorum* ya kutosha. Naomba kifungu hiki kiangaliwe kwamba endapo tumekosa *round* ya kwanza, *round* ya pili tunaendelea moja kwa moja au inakuwaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kifungu cha 28, naungana na marekebisho ya Serikali kwamba rasimu ijadiliwe kwa siku 70 na siyo zaidi kama nilivyosema hapo

mwanzo. Pamoja na hilo, name naona ni gharama pia kama watu wote watakaa wengi mahali pamoja na kulipwa fedha; lakini kama nilivyosema toka mwanzo kwamba Wajumbe inawezekana wakachoka kama siku zikiwa ni nyingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.  
*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Betty Machangu kwa mchango wako. Sasa namwita Mheshimiwa Juma Nkamia, atafuatiwa na Mheshimiwa Subira Mgatu.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nimekaa eneo ambalo pengine watu wanashituka kidogo, lakini niliona nihadie huku pamoja na wenzangu kwa sababu viti hivi mara nyingi watu wamekuwa wakikimbiakimbia, kwa hiyo ni vizuri na sisi tuvipashe joto kidogo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mionganini mwa watu ambao mwanzoni nilikuwa kwenye kundi la kutaka Katiba Mpya. Lakini kutokana na mazingira ambayo nilikuwa nikifanya kazi, mambo mengine nilikuwa ninalazimishwa tu kufanya. Nachukua nafasi hii kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania – Mheshimiwa Dkt. Kikwete kwa uamuzi aliofanya wa kuanzisha huu mchakacho wa Katiba Mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na Serikali kwamba Mheshimiwa Rais aendelee kubaki kuwa ndio Mteule wa wale Wajumbe 166. Kwa nini nampongeza Mheshimiwa Rais? Kelele nyingi sana zilikuwa ni kuhusu Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania miaka nenda, miaka rudi. Miswada ukaletwa ndani ya Bunge, wenzetu wakakimbilia Ikulu, Rais huyo huyo ambaye leo wanambeza humu ndani ya Bunge akawakaribisha, wakanywa chai, wakala sambusa, lakini leo kwa mastaajabu kabisa, wanakuja humu ndani ya Bunge, wanamsema vibaya kwamba eti hatatenda haki kwenye uteuzi wa Wajumbe. Lakini ni hawa hawa waliompelekea jina la Prof. Baregu na akamteua. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwanafalsafa mmoja anaitwa Mark Aveli, karibu miaka 800 iliyopita aliwahi kusema kuwa "Dhima ya Chama chochote cha siasi ni kushika dola. Lakini ni namna gani unashika dola, ndiyo jambo la msingi." Unaweza kushika dola kwa kuwadanganya watu kama wenzetu wanavyotaka kufanya na unaweza kushika dola kwa kuua. Sasa kama wenzetu hawa CHADEMA na hawa rafiki zao ambao leo wamekuwa marafiki kwa muda mfupi, wanataka kushika dola kwa kutumia njia ambazo siyo sahihi, nadhani Watanzania wana akili, wana busara na hawatafanya makosa kama hayo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Katiba ni jambo la msingi sana na Miswada yote ya Sheria inajadiliwa ndani ya Bunge. Nilikuwa naangalia juu kule, wenzangu Waandishi wa Habari, ni kitu ambacho kimenishangaza kidogo! Wakati

CHADEMA na CUF wanatoka, Waandishi karibu wote walikimbia kule juu wakaenda nje. Nilikuwa najiuliza, ni habari gani wanayokwenda kuandika wakati tayari habari imetokea ndani ya Bunge? Kwa sababu kwa vyovyote, ukimkamata mtu pale mlangoni, ehe, kwa nini umetoka? Wakati unajua fika kwamba kwa nini ameamua kutoka kwenye ukumbi wa Bunge! Kwa hiyo, *the story was already made*. Mimi nashangaa kidogo! (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waandishi wa Habari wenzangu, najua wengi wanaweza kunichukia, lakini ni bora kulaumiwa kwa kusema ukweli kuliko kulaumiwa kwa kukaa kimya. Habari kubwa leo ni huu Muswada wa Katiba. Habari kubwa siyo mtu kutoka nje! Kama ugali unaletwa mezani, tuule hapa, siyo twende jikoni. Hakuna kitu kule! Mheshimiwa Lusinde ananiambia walishamaliza ku-sign karatasi za posho ndiyo maana wakatoka. Vyema! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tumetumwa na Watanzania wenzetu kuwawakilisha katika Bunge hili. Wanapotoka, halafu baadhi ya vyombo vya habari vinaona kwamba yale waliyofanya wenzetu ndiyo ya maana, na haya tunayofanya humu ndani hayana maana, maana yake ni kuwa tumeshapotoka. Tumeshakuwa mufilisi! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kusema hilo kwamba bahati nzuri mimi nimefanya kazi katika *big media* katika dunia hii. *Media* zote zile kubwa nimepita. Hizi siyo habari kwamba wenzetu wanakimbia kwenda kujadili jambo la

msingi hili ambalo linaangalia maisha ya Watanzania katika miaka mingi ijayo, wanakimbia, halafu Waandishi wa Habari wanaona kwenda kule ndiyo habari! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nikiwa Mhariri wa hicho chombo cha habari, siwezi kutoa hiyo habari! Lakini hutashangaa kwamba *lead story* ya leo ni "CHADEMA, CUF Watoka Bungeni." Nimeona niliseme hili kwa kuwa mimi ni mwandishi na ninatoa rai tu kwa Waandishi wenzangu kuwa tutakuwa tunawapotosha Watanzania. Naunga mkono sana suala hili, kama alivyosema mwandishi mwenzangu Mheshimiwa Ester Bulaya pale kwamba kibaiolojia sisi bado tunaendelea kuishi. Tuna miaka mingi! Tunatengeneza kitu kwa ajili ya watoto wetu na sisi wenyewe. Kwa hiyo, túsitumie *cheap popularity* ya kutaka kuonekana kwa watu kuwa kila kinachofanywa na Serikali humu ndani ni kibaya. Nami nitashangaa sana! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kule walikokimbilia baada ya kukimbia mwanzoni hapa mwaka 2012 kwa Mheshimiwa Rais, leo wamekuja wamemshambulia huku. Leo wametoka wanakwenda wapi? Sasa kama wote wamehusika kwenye jambo hili, mimi nilikuwa namshangaa jirani yangu Mheshimiwa Tundu Lissu, alipokuwa anamshambulia Mheshimiwa Rais kwenye taarifa yake! Kwa heshima tu, Bwana Mkubwa huyu aliwakaribisha, akachukua maoni yake na yakafanyiwa kazi. Mnakuja hapa leo mnamtukana, mnamshambulia, hivi kesho mtamwomba tena? Haiwezekani! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nikikukaribisha nyumbani kwangu nikakuonyesha uani ni pale, ukajisaidia nje, siku nyingine siwezi kukuonesha. Nitakwambia maji hayatoki. Niliona niongelee hilo. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimalizie tu kwamba Mheshimiwa Rais atue wale watu. Kama Wanasheria walivyosema kwamba kwenye Gazeti la Serikali Mheshimiwa Tundu Lissu hawezi kupeleka habari pale akazi-*gazette*. Kwa hiyo, ni lazima chombo cha Serikali kifanye kazi hiyo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais lazima atue watu hawa. Ninarudia tena, alivyomteua Prof. Baregu. Nimi sielewi, mwanzoni walipoteuliwa, hakuna mtu aliyelalamika, na Mwenyekiti wao Bwana Mbewe alipeleka jina hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Watanzania wenzangu huko nje, ni lazima tuwe makini na jambo hili. Tuangalie kwanza Taifa badala ya *propaganda* za kwenye Vyombo vya Habari. Wakati Iraq inavamiwa, mimi nilikuwa kwenye Kitengo cha *propaganda BBC* kwa kuwaaminisha Waingereza wote kuwa kule kuna silaha na hivi na hivi. Lakini baadaye vilivyoanza kuja kutoka vitu vingine na mimi nikasema *anyway I was doing my job*. Nilikuwa nataka watoto wangu waende shule. Nawaomba Watanzania wenzangu kwamba hizi *propaganda* tuziweke pemberi, tuangalie mustakabali wa Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni eneo la kufanya Bunge la Katiba. Amesema pale Mheshimiwa Machangu, lakini mimi ukiniliza tufanyie wapi Mkutano huu? Ningesema Dodoma. Kuna sababu chache tu. Dar es

Salaam kuna msongomano mkubwa sana wa magari, *concentration* ni ndogo, joto nalo ni kali na kipindi hicho cha Novemba ni mvua. Lakini Chimwaga pale kuna ukumbi mkubwa na mzuri. Unafanyiwa marekebisho tu, unatosha. *Parking security iko safe.* Kwa hiyo, naomba wale wanaoshughulikia jambo hili, tufanyie Dodoma. Sisemi kwa kuwa mimi natoka Dodoma, hapana. Nasema kutokana na mazingira, *concentration!* Itakuwa imetuisaidia sana sisi kukaa. Kwa Dar es Salaam sisemi, watani zangu Waunguja kuwa kila siku mtakuwa mnavuka, hapana. Lakini ukiwa hapa, ni mahali pazuri, *concentration* itakuwa kubwa. Naomba Mheshimiwa Waziri, hebu hili mlitafakari kwa kina sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono kwa heshima kubwa sana. Tunahitaji Katiba mpya itakayowasaidia Watanzania na siyo Katiba itakayowasaidia watu wachache. Hata hao wanaokimbia, lengo lao wanajua kabisa kwamba Katiba hii ya Watanzania, walishaanza kuzunguka nchi nzima, kupiga *propaganda* za uongo, kudanganya na kufanya kila kitu. Sasa wameona mbinu za kudanganya nje zimeshindikana, wameamua sasa kudanganya kwenye Vyombo vya Habari. Nami nawaomba Waandishi wenzangu tuandike habari badala ya kuandika taarifa. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nakushukuru sana Mheshimiwa Juma Nkamia kwa mchango wako. Sasa namwita Mheshimiwa Subira Mgusu, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Titus Mlengeya Kamani.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, natanguliza kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunipa pumzi na ninakushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa ya kuendelea kuandika historia ya kuwa na mimi ni mshiriki katika kuchangia jambo kubwa hili kwa maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze moja kwa moja kusema kwamba naunga mkono hoja iliyowasilishwa hapa Mezani. Lakini nianze kama walivyoanza wenzangu kwa namna ya pekee kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuridhia mchakato huu, lakini pia kwa namna ambavyo alivyouridhia mchakacho kwa aina ya pekee kwanza kulishirikisha Bunge kutunga Sheria, lakini kuwasikiliza wadau mbalimbali na hatimaye kuunda Tume iliyopokea maoni ya Watanzania wote, ikawasilisha Rasimu, ikajadiliwa katika Mabaraza yetu mbalimbali ya Katiba na hatimaye, hatua inayokuja ya kuwasilisha kwenye Bunge la Katiba, na pia mwishoni kupata ridhaa ya wananchi wa Tanzania. Kwa mara ya kwanza kabisa jambo hili linatokea kwa nchi yetu, kwa hiyo, naomba nimpongeze sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na mimi kwa kusema kwamba jambo tunalolijadili ni kwa maslahi ya Taifa letu. Nawaomba Watanzania wenzangu kwamba tunapowachagua Wawakilishi na Wabunge waingie ndani ya Bunge na kupigania hoja zao kwa namna ambavyo itafaa, hakuna kurudi nyuma na hawawezi kushindwa vita; inashangaza kwamba hoja inawasilishwa, maoni yanachangiwa, lakini unapoanza mjadala, wenzetu labda kwa kuamini tena kuwa Mheshimiwa Rais atawafungulia

mlango tena, wanatoka na kujipanga upya, ni jambo la kushangaza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, inashangaza zaidi kwamba wenzetu kwa namna ambavyo wote mwaka 2010 tulishiriki katika Uchaguzi, kila Chama kiliomba ridhaa kwa Watanzania, lakini nongwa hii isiyokwisha ya kukionea nongwa Chama cha Mapinduzi kilichoingiza Wabunge wengi, hawakujichagua wenyewe, wamechaguliwa, na wao walijinadi wakaonekana hawatoshi, wanatosha asilimia hiyo waliyoipata; nongwa ya nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, inaonesha kuwa msamati huu wa Chama cha Mapinduzi, Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, msamati huu wao unawanyima usingizi. Kinachoshangaza, jambo linalotajwa ni kwamba CCM walikuwa na mwongozo wao. Lakini ni kweli *CUF* walitoa mwongozo wao juu ya Rasimu iliyotolewa, CHADEMA walikuwa na mwongozo wao na kwa namna ya pekee na wao wakaamua kutumia *style* yao ya Mabaraza yao, lakini sisi ambao tuna nchi, tuna mamlaka, tuna dola, tuliona kuwa na wao wanafanya siasa, na hakuna ambaye aliwanyooshea vidole. Sasa inashangaza tunapoingia ndani ya Bunge inanesha wao ni waoga. Kwa nini wanaogopa vita? Tupambane! Wakae ndani ya Bunge tupambane kwa hoja! (*Makofi*)

Kwa hiyo, nawaomba tusubiriane mwaka 2015. Nimeshaona wameanza kupata wasiwasi, wanaanza kuota ndoto ambazo hazipo. Sisi tunachosema ni kwamba kama ambavyo utaratibu umewekwa, tunategemea sherehe za

Muungano miaka 50, Katiba yetu izinduliwe na tunamwomba Mwenyezi Mungu aujalie mchakato ufile salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi wangu huo, naunga mkono marekebisho yaliyoletwa hasa kifungu cha 22 (2)(a), 22 (2)(b), na 22(1)(c) kwamba hawa Wajumbe wengine wa Bunge Maalum 166 wateuliwe na Mheshimiwa Rais. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata wakati huu bado tunayo Katiba ya mwaka 1977 ndiyo inayotumika na Mheshimiwa Rais amepewa mamlaka katika Katiba hii na Mheshimiwa Rais ni Taasisi na ina mamlaka yake. Sasa leo linapokuja suala kwamba tumnyang'anye mamlaka yake wakati Katiba ya kuongoza nchi ipo, juu kufanya teuzi mbalimbali kama ambavyo imedhihirishwa kwenye Katiba, haiwezekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono kwamba Vyama na Taasisi zipendekeze. Nashangaa kwa nini wakati wanapendekezwa Wajumbe wa Tume, Vyama mbalimbali vilipendekeza wakiwemo wenzetu ambao leo wameona labda mjadala huu ni mkali hawatauweza, wakatoka nje; lakini nashangaa, unaposema kwamba ukipendekeza majina, kwa mfano, kwenye Taasisi zisizokwu za kiserikali wanapendekeza majina kumi, wanaotakiwa, wanaotakiwa ni watano; umwekee utaratibu Mheshimiwa Rais! Mambo haya ya wapi? Wasubirie fursa yao ikipatika Mwenyezi Mungu akiwajaalia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, linge, nashangaa urafiki wa leo wa Kambi Rasmi ya Upinzani ya kusema kwamba Zanzibar kwenye Bunge la Katiba watakuwa wachache, theluthi moja. Nashangaa kwa sababu wakati tunapitisha sheria ya kuwateua Wajumbe wa Tume ya Katiba, hao hao walipinga Wajumbe wa Tume ya Katiba wasiwe sawa kwa sawa kwa kigezo cha kwamba Tanzania Bara tupo wengi. Kwanini Zanzibar na wao waingize Wajumbe sawa kwa sawa wale 30? Leo iweje waunde urafiki wa muda wawe wasemaji wa Zanzibar? Natambua Bunge hili limekuwa likishuhudia Kambi Rasmi ya Upinzani ikiishambulia Zanzibar kwenye mijadala mbalimbali. Leo urafiki huu wa muda una mashaka! Kutafuta mapenzi haya ya muda, mapenzi ya dharura haya, tuwe makini nayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba Wazanzibar msidanganyike! Mapenzi haya ya dharura; Baba wa kambo akikupenda sana wewe mtoto, ujue anampenda mama yako, siyo wewe! Kwa hiyo, tujihadhari. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kweli walikuwa na nia njema, kama kweli ni wasemaji wa kusema ubia wa Muungano, sikatai walivyomnukuu Prof. Kabudi aliposema kwenye semina yetu. Lakini wao walipinga na ndiyo maana Prof. Kabudi akanukuu akasema, wabia wa Muungano ni lazima wawe sawa. Lakini leo mimi nadhani kama alivyosema Mwenyekiti wa Kamati, waliwaita Wadau mbalimbali kutoka Zanzibar, walitoa maoni yao, nadhani hili limekubalika; na *issue* pale ni Bunge la Wananchi, kwa sababu katika uwakilishi wa Tume iliyokusanya maoni, uwakilishi ni hamsini kwa hamsini. Lakini inapokuja kwenye

Bunge la Jamhuri ya Muungano, leo tunaweza tukajiuliza, mbona Bunge la Jamhuri ya Muungano ni kubwa kuliko Baraza la Wawakilishi la Zanzibar? Ndiyo tunakokwenda huko? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitahadharishe mapenzi haya ya dharura; mapenzi haya ya ghafla wawe makini nayo! Yana namna yake! Wameshaona huko Zanzibar hawakubaliki, hawana fursa, kwa hiyo, wameamua watumie marekebisho ya Muswada huu kutafuta huruma za Wazanzibar baada ya kuona Wazanzibar wanalamika mara kwa mara. Mbona kuna Chama hapa kwanza hakina wanachama wengi, lakini mara nyigi kimekuwa kikipinga maslahi ya Wazanzibar katika mambo mbalimbali? Wamewahi kueleza hapa namna Muungano ulivyo, wakauchakachua ndani humu kwa maoni yao, leo naona mambo yanakuwa mazuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia naunga mkono mapendekezo mengine ambayo yamewasilishwa. Pamoja na kwamba sina hakika kama ulivyosema utatolea mwongozo baadaye na kanuni zilizotumika, lakini wakati mwingine ni lazima busara itumike. Bunge liliobaki tumebakiwa na Bunge hili na Bunge la Novemba la wiki mbili, tunaingia Bunge la Katiba. Kama Serikali imeona kuna ombwe katika sheria hasa itakapofika upigaji wa kura, endapo haitafikia hiyo theluthi mbili, ni nini cha kufanya? Hizi kanuni siyo msahafu! Kanuni hizi siyo Biblia! Yaani kuleta jambo lenye maslahi ya kutazama kesho, hivi ikitokea mazingira haya tutafanyaje? Kwa hiyo, walitaka tusubirie kwamba lije Bunge la Novemba tena la wiki mbili, na

Miswada mingine, tuongeze kifungu kimoja tena kidogo, kwanini tunafanya hivyo? Kwa nini tusitumie busara wakati mwingine?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili pamoja na kwamba linasubiri mwongozo wako, lakini naunga mkono kwamba kuwepo na kifungu kinacholeta mbadala kwamba endapo theluthi mbili haitapatikana, nini kifanyike? Nadhani Serikali ilikuwa na mapendekezo mazuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kwamba, kwa kuwa Wazanzibar wenyewe wameshiriki; na kwa kuwa uzoefu wa Bunge letu kupitia Kamati zetu, Kamati zinakaa Dar es Salaam na Dodoma na hakukuwa na malalamiko yoyote; na kwa kuwa mabadiliko yenyewe haya vifungu vilivyokuwa vinahusika havizidi sita; hata pia ukipima na thamani ya muda na kadhalika, mimi nadhani wasiwase mee watu ambao hawajawatuma kusema jambo ambalo wamelisema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono mapendekezo yote, naunga mkono marekebisho haya, nawaomba Watanzania, mmetuchagua kuwawakilisha. Sisi kwetu Pwani tuna msemo maarufu unaosema "paka hasusiwi kikaango." Ukimsusia, minofu inaondoka. Sisi hatupo hapa kususa, tupo hapa kujadili hoja kwa maslahi yenu, kusema hata yasiyotarajiwa, kupingana kwa hoja, ndiyo kazi mliyotutuma. Labda kama kuna kazi nyingine za ziada kama mmetutuma, nadhani ninyi ni waamuzi. Nadhani mtumie busara, muamue kwamba sisi kwa kweli

kazi yetu kubwa ni kutoa maoni yetu, kupingana kwa hoja, kukubaliana kutokukubaliana ndani ya Bunge hili Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, nakushukuru kwa fursa uliyonipa. Pia nawashukuru Kamati kwa kazi waliyoifanya, naishukuru Serikali pia kwa mapendekezo haya kwa kuona ni namna gani ya kuzihuisha hizi sheria kadri muda unavyokwenda na kwa kutupa heshima Bunge kufanya kazi yetu iliyokusudiwa ili kuisaidia Serikali, mwisho wa siku tupate Katiba kwa maslahi ya Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwahakikishie Watanzania, huu unaosemwa wingi wa CCM, sisi tunajadili hoja kwa maslahi yao kutegemea na maoni ambayo wameyatoa na pia kwa mustakabali wa Tanzania yetu inayokuja baada ya miaka hamsini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, nashukuru. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Subira Mgusu kwa maneno yako ya hekima kubwa. Sasa Mheshimiwa Titus Mlengeya Kamani ndiye anayefuata.

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia na mimi nafasi kuchangia katika Muswada huu muhimu sana katika mustakabali wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu kuwakumbusha Wabunge wenzangu na Watanzania kwa ujumla, kuna ule utamaduni wa kawaida tu, japo unatafsiriwa vilevile katika hesabu, kitu kinaitwa *proportionality*, unakuta kitu kingine kinaitwa *normal distribution*. Yaani unapokuwa katika mgawanyo wa jamii ya watu, utakuta kuna idadi kubwa itapenda kitu fulani halafu wachache wanakuwa tofauti kabisa na wenzao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia hesabu ya Watanzania katika uchaguzi uliopita, idadi kubwa ilikichagua Chama cha Mapinduzi kuongoza Taifa hili. Lakini kuna Watanzania wengine ambao walikuwa na maono tofauti kabisa na ndiyo maana tuna Wabunge wa Vyama vya Upinzani. Lakini ukiangalia hesabu ilivyokaa kat i ya Wabunge 355 ni Wabunge 262 wa Chama cha Mapinduzi na 93 wa Upinzani ambao ni asilimia 26 tu ya Wabunge wote. Hii inamaanisha kwamba Watanzania wengi wana imani na Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii imetafsiriwa vile vile hata katika muundo wa Mabaraza ya Katiba. Huwezi ukashangaa kukuta Wajumbe wengi wa Mabaraza ya Katiba ni wakereketwa au ni washabiki au ni wanachama wa Chama cha Mapinduzi. Ni kwa sababu ya uwiano huo huo! Sasa nashangaa wenzangu wanashindwa kuliona hili ambalo ni jambo la kawaida tu katika jamii yoyote. *Sample* yoyote ukichukua ni lazima kutakuwa na uwiano wa namna hiyo. Kwa hiyo, ningeomba tu hata kama wana mawazo tofauti na mawazo ya wengi, hawastahili kupata chuki, kupata uchungu kwa sababu hawajapata uungwaji mkono

mkubwa. Kwa sababu bado Watanzania ndio wanaamini hivi! Sasa huwezi ukawalazimisha kwa nguvu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa tu kuwashawishi Wabunge wenzetu wa Upinzani, lakini na Watanzania wengi ambao hata wana muono tofauti na wa Watanzania wengi, waelewe kwamba bado tuna imani na utawala na uongozi wa Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, hata mapendekezo yanayokuja tuyaunge mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nasikiliza hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani, nilishangaa sana kubeza au kupuuza mamlaka ya Mheshimiwa Rais. Nchi hii haiko kwenye vita na nchi hii inayo Katiba ambayo inaendelea sasa hivi ambayo inaongoza nchi hii. Sasa unapotaka kusema unachukua watu tu, unawaokota kutoka sehemu yoyote na hatimaye hawana mtu yejote ambaye anawajibika, tutakuwa nchi ya aina gani? Tunataka tuwe Misri sasa hivi?

### **MBUNGE FULANI: Ajabu!**

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Ndiyo mfano wa kufurahia, Misri inavyojiendesha! Ndiyo kitu cha kujivunia Libya ilivyoendesha Serikali yake! Hiki ndiyo kitu cha kujivunia ambacho Watanzania tunataka twende? Hivi tunasahau gharama ya kuwa na amani!

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi juzi hapa tulikuwa na lundo la Wakongo walioingia Tanzania kwa sababu hakukaliki kule kwao. Tulikuwa na Wanyarwanda lundo na

Warundi Lundo hakukaliki kwao! Ndiyo tunataka Tanzania twende namna hiyo kwa kuibezza Katiba hii iliyotusimamia kwa miaka hamsini, Katiba ambayo ndiyo imetuongoza tukasema sasa tulete Muswada wa kutengeneza Katiba mpya kwa sababu tunafikiri wakati huu iko haja ya kuwa na Katiba mpya? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii iliingia kwenye mfumo wa Vyama Vingi kutokana tu na maoni ya Watanzania chini ya asilimia 20, lakini hekima za Baba wa Taifa, akasema hapana hata wachache tuwape nafasi ya kusikilizwa. Tukaingia mfumo wa Vyama Vingi, na ndiyo maana tunao hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mabadiliko ya tabia za watu huwa yanachukua muda, ndiyo maana bado hatujawa na wawakilishi wengi wa Upinzani kwa sababu Watanzania, *it is a gradual process*. Watu watabadilika taratibu kutokana na mfumo ambao umekuwepo kwa muda mrefu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukikubali kupuuza nafasi ya Rais kuteua Wawakilishi japo wamepewa nafasi wenyewe, yale makundi mbalimbali yapendekeze halafu Rais atue, tutakuwa kama ilivyotokea Kenya juzi wakati wanatengeneza Katiba yao. Wamechukua miaka mitatu kuunda Katiba kwa sababu walikuwa hawawezi kuelewana, pale *Bomas of Kenya* palikuwa panawaka moto! Mpaka wanashindana, viti vinarushwa huko kwenye Bunge la Katiba, watu wanapata ngeu, wanasema tuondoke kwanza tukaanze upya. Ndiyo tunataka kufanya

namna hiyo wakati *machinery* au mfumo tunao tayari ambao unaweza ukatupeleka tukatengeneza Katiba vizuri tu bila tatizo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika na Watanzania kwa ujumla, hivi unapoteuliwa kushika nafasi fulani, uadilifu wako na tabia yako vinabadilika? Labda siwezi kulitafsiri vizuri katika Kiswahili. *Integrity* ya mtu inabadilika tu kwa sababu ameteuliwa na Rais?

Mheshimiwa Naibu Spika, Upinzani wenzetu waliwasilisha jina kwa mfano la Prof. Baregu, msomi aliyetukuka katika Taifa letu, lakini ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha CHADEMA. Waliwasilisha jina lake akateuliwa. (*Makofi*)

### **MBUNGE FULANI:** Ndiyo!

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Sasa walitaka aache ile kazi ambayo ametumwa kufanya na Taifa hili kwa niaba ya Watanzania wote, akafanye kazi kwa niaba ya Chama kimoja? Hii Tume ni ya Chama au Tume ya Taifa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana wenzetu tusiwe tunapotosha wananchi. Tume hii ni ya Taifa, inatengeneza Katiba ya nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nani hamfahamu Mheshimiwa Jaji Sinde Warioba ambaye alikuwa Waziri Mkuu wa Nchi hii? Ni Mwana CCM imara! Lakini mnaona mapendekezo ya Rasimu ya Katiba, imekuja na hoja nyingi

ambazo zinatofautiana kabisa na mawazo na msimamo wa Chama cha Mapinduzi. Kama ingekuwa huyu anaenda kufanya Katiba ya Chama cha Mapinduzi, haya mapendekezo hata ya Serikali Tatu mngeyaona? Mbona tunabadilika tunakuwa vinyonga? Hawa watu wanafanya kazi ya Taifa ndiyo maana kila Chama kuna eneo fulani kimekwazwa, kuna eneo fulani kimeunga mkono, na hata Chama cha Mapinduzi hakijayakataa mapendekezo yote ya kwenye Rasimu, tofauti na huyu Msemaji wa Upinzani alivyokuwa anasema kwamba tumeyakataa mapendekezo yote. Siyo kweli! Mimi ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama cha Mapinduzi. Kuna mengine mengi tu tumeyaunga mkono na mengine bado tuna nafasi ya kujadiliana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni Katiba ya Taifa letu, siyo ya Chama. Katika Katiba, ni muafaka wa Watanzania wote. Kuna kupata na kupoteza. Huwezi ukapata vyote! Ni lazima tuwe tayari. Hata Chama changu kuna mengine ambayo kinaweza kikapoteza na wao Wapinzani wawe tayari kupoteza mengine. Wasifikiri wao mawazo yao ndio Mungu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilitaka kabisa kimsingi tukubaliane, tujadiliane hapa Bungeni, tutumie hii fursa ambayo tumepewa, tumedhaminiwa na Watanzania wenzetu, tuisimamie. Sheria inajadiliwa Bungeni, haijadiliwi lkulu wala haitajadiliwa kwenye maandamano barabarani kule. Sheria itatungwa hapa hapa! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wiki iliyopita na hii wiki mwanzoni tumepitisha Miswada hapa, kulikuwa na mchuano mkali kweli kwenye Miswada hii iliyopitishwa hapa. Tumepitisha Muswada wa Umwagiliaji na tukapitisha Muswada wa Ushirika. Kulikuwa na mchuano, watu wametoa hoja zao, lakini hatimaye tumeafikiana. Kuna waliopoteza na kuna waliopata katika maoni yao, lakini haiwezi kabisa kila kitu wewe unachowasilisha Bungeni kikubaliwe na wote. Haiwezekani! Wewe sio malaika! (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nafikiri mapendekezo yaliyoletwa na Serikali yana msingi na yameletwa wakati muafaka tu. Kwa sababu hatuwezi tukasubiri mpaka muda ule ambapo sasa mambo yamebanana, maamuzi yanatakiwa kufanywa, halafu ndiyo tunagundua kwamba hiki kitu hakipo, sasa mnaanza kuvurugana tena. Ndiyo inaanza kuja, wameleta Muswada huu kwa sababu kuna hiki, kuna hiki. Lakini sasa Serikali imeyaona mapema haya, ikabaini upungufu huu, ndiyo maana imeleta Muswada huu. Kwa hiyo, naipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu. Vile vile naipongeza Kamati ambayo imeangalia sana kwa kina mapendekezo haya. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mapendekezo haya, kuna lile suala la idadi ya Wajumbe. Kimsingi lile halina mashaka, mimi naliunga mkono mia kwa mia, na ninaamini kabisa limewekwa kwa nia njema ili kuhakikisha kwamba Wajumbe wote wanakuwa na utulivu na imani kwamba tunatengeneza Katiba ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile katika kipengele cha 22 cha Spika na Katibu wa Bunge kuendesha, kusimamia lile Bunge la Katiba ni sahihi kabisa. Kwa sababu kwanza tayari wao wanao weledi, wanafanya kazi hii katika Bunge hili. Lakini vile vile inakuwa kazi ngumu unapoanza kutafuta tena mtu mwingine kwa sababu Spika hapa anafanya kazi hii kwa kipindi cha miaka mitano, anapata uzoefu. Sasa mnaanza kuchukua sijui Spika kutoka sijui sehemu gani aanze kujifunza Uspika kwenye Bunge la Katiba, mpaka akapate weledi, hii sasa hatufanyi majaribio hapa! Tunakuja kufanya kazi! Kwa hiyo, ni sahihi kabisa Spika akafanya hivyo na Spika amechaguliwa kidemokrasia, kwa hiyo, hamna shaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika Kifungu cha 26 suala la upigaji kura; ni vizuri wamechukua hii tahadhari mapema, kwa sababu inaweza ikatokea kabisa katika upigaji ule wa kura, ile theluthi mbili haipatikani sawasawa kwa Bara na Zanzibar. Ni lazima muwe na njia ya kutokea. Hamwezi mkaacha hivyo hivyo. Mtaendelea kuwa mnapiga kura hizo mnazirudia hata kwa miaka mingapi? Ni lazima kuwe na njia ya kutokea. Ni sahihi kabisa kwamba hatimaye ule wingi wa kura uwe ndiyo mwamuzi wa mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, napongeza na ninaunga mkono mapendekezo haya ya mabadiliko ya sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimebaini katika kikao hiki, kushabikia sana ubaguzi wa aina fulani katika Taifa letu. Kushabikia ubaguzi wa Bara, sasa jina la Tanganyika linatamkwa kwa wingi zaidi, na kushabikia Zanzibar kama maeneo huru tofauti. Sasa tunaweza tukawa tunafanya mchezo mchezo, tunachokonoa, lakini tunasahau kuna madhara makubwa zaidi ya hapo. Sisi tunaochokonoa ni kwa sababu tumeshaonja utamu wa madaraka, tunatafuta nafasi fulani. Lakini ikifika ikatokea pande hizi mbili zikatengana kwa maoni haya ambayo yanajaribu kujengwa hapa, kuna watu wengi hata hawa wanaosema na kushabikia watakuja kujuta sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nihitimishe kwa kuunga mkono hoja hii. Ahsante sana. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Titus Mlengeya Kamani kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na michango kesho, nitawaomba wale ambao mtakuwa na nia ya kuchangia kesho wakati wa maswali tuendelee kukumbushana, tutaendelea na uchagiaji kama kawaida.

Niseme tu kwa Watanzania ambao wanashangaa mambo haya yanapotokea; ni kwamba tunapoona watu wanatoka nje, huwa wameshapanga kufanya hivyo kabla ya kikao.

**MBUNGE FULANI:** Sawa sawa.

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, siyo kutokana na kwamba Kiti hiki kimefanya jambo lolote la kustahili watu watoke nje eti kwa sababu kuna jambo fulani wameonewa, hapana. Ni mpango tu! Kama ulikuwa huna nia ya jambo ambalo linaendelea mbele, wasingesimama hata kusoma maoni yao, maana kama huu ushirikishi hawakushirikishwa tangu huko, sasa maoni walikuwa wanasoma ya nini? (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Sawa sawa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, lakini muhimu ni lazima tuelewane kuhusu mchakato wa utungaji wa sheria. Ufafanuzi nitautoa kesho wa haya waliyoyatoa. Ni kwamba kazi ya kutunga sheria kikatiba ni kazi yenu ninyi Wabunge, na Wabunge hapa mnawakilisha nchi nzima! Hakuna sehemu ya nchi ambayo haina Mwakilishi hapa ndani! Kwa hiyo, Muswada ukiwa kwenye Kamati inapokutana Dodoma au Dar es Salaam, wadau wataitwa wowote wale wanakuja kuhudhuria; wakitaka wanakuja, wasipotaka hawaji na Kamati ile ina wajibu wa kumaliza kazi na kuleta hapa. Kwa sababu ni kazi yao kama Kamati. Ndiyo maana katika maoni hapa anasoma Waziri, anafuata Mwenyekiti wa Kamati, inafuata Upinzani. Vinginevyo kungekuwa na maoni ya wadau hapa! Kwanini hakuna maoni ya wadau hapa? Kwa sababu ni kazi ya Kamati kutaka kupata maoni zaidi na inapofika hapa ni kazi yetu sisi Bunge.

Hivi wa kutoka Kongwa waliokuja kwenye Kamati hiyo ni wangapi? Kwanini mnauliza upande fulani tu? Wakongwa nao walikuwa wangapi? Ndiyo maana nipo mimi hapa, na ndiyo maana na wewe upo hapa! Kwa hiyo,

hiyo ni michakato tu, kushirikishana, ni utaratibu wa kidemokrasia zaidi. Lakini haufanyi kazi ya Bunge isimame kwa ajili hiyo. Waliotoka Jimboni kwako wewe ni wangapi waliokwenda kwenye hiyo Kamati? Hata baadhi ya waliotoka kwenye Majimbo yao kwenda kwenye hiyo Kamati ni wangapi?

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, kesho tutaelezana vizuri ili tuweze kuweka sawasawa mambo haya. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, naomba kusisitiza kuhusu mahudhurio. Ni tabia ambayo Watanzania wanaichukia sana. Tabia ambayo Bunge linapoendelea, Mbunge upo sehemu nyingine ya Tanzania unaonekana huko, inawaudhi sana wapiga kura wako. Nisisitize mahudhurio kwa Waheshimiwa Wabunge, nisisitize mahudhurio kwa Waheshimiwa Mawaziri. Kuna utoro usiokuwa na sababu! Kuna baadhi ya Waheshimiwa Mawaziri hapa huwaoni hata wiki mbili zote! Hivi kweli wewe uko *busy* kiasi hicho kweli? Tufike mahali tuseme hivi vitu. Ah, basi bwana! (*Kicheko/Makofi*)

Ni lazima kuwe na *discipline!* Muswada huu ni wa Serikali. Inapokuwa Serikali wenyewe hawaii, maana yake nini? Wanamwachia Waziri mwenza peke yake! Ni lazima wawepo na Wabunge na sisi tuwepo, ndiyo wajibu wetu, tuwawakilishe wananchi kuhakikisha kwamba tunaitendea haki hii Miswada. Kwa hiyo, mahudhurio ni muhimu na ndiyo maana vikao vyetu ni vifupi, wiki mbili tu. Hawa watu ambao hawapati muda wa wiki mbili na Muswada mingine ni muhimu sana, kwa mfano huu ni wa Katiba; sasa hao

ambao hawapo wana jukumu gani la maana zaidi kuliko Katiba? Lipi? (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, mwisho, kwa Wabunge wa CCM, kuna kikao baada ya hapa ukumbi wa Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maneno hayo, na kwa vile muda wetu umekwisha kabisa, naomba niahirishe shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.41 usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi,  
Tarehe 5 Septemba, 2013 Saa Tatu Asubuhi)*